# Wajibu wa Jeshi la Polisi katika Chaguzi za Kidemokrasia

Programu ya Mafunzo Inayohusu Haki za Binadamu, Jinsia na Wajibu wa Jeshi la Polisi Katika Uchaguzi wa Kidemokrasia Mwaka 2015

# Wajibu wa Jeshi la Polisi katika Chaguzi za Kidemokrasia

## Programu ya Mafunzo Inayohusu Haki za Binadamu, Jinsia na Wajibu wa Jeshi la Polisi Katika Uchaguzi wa Kidemokrasia Mwaka 2015

Kwa Hisani ya Kitengo cha Menejimenti ya Ufadhili wa Pamoja wa Chaguzi Tanzania mwaka 2015.

Toleo la kwanza 2005
Toleo la pili 2010
Toleo la tatu 2015

# Yaliyomo

DIBAJI ........ iii

MALENGO YA PROGRAMU YA MAFUNZO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, JINSIA NA WAJIBU WA JESHI LA POLISI WAKATI WA CHAGUZI ........ v

SURA YA 1 – Utangulizi Kuhusu Haki za Binadamu ........ 1

SURA YA 2 – Shughuli za Kipolisi Katika Demokrasia ........ 9

SURA YA 3- Jinsia, Hali ya kuwa Tofauti, Umoja wa Kijamii na Chaguzi ........ 18

SURA YA 4 – Polisi Jamii ........ 26

SURA YA 5 – Utatuzi wa Mgogoro ........ 34

SURA YA 6 - Kudumisha Utulivu wa Umma ........ 48

SURA YA 7 – Ukamataji ........ 56

SURA YA 8 – Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto ........ 67

SURA YA 9 – Wajibu wa Jeshi la Polisi katika Chaguzi ........ 74

SURA YA 10 – Ukiukwaji wa Haki za Binadamu ........ 88

SURA YA 11 – Taratibu za Kiusalama kwa Majeshi ya Usalama wanaposhughulika na Vyombo vya Habari ........ 96

# DIBAJI

Kitabu hiki kinachohusu Haki za Binadamu ni cha kipekee kwa namna moja. Kilisanifiwa ili kutoa uelewa wa Kanuni za Haki za Kibinadamu kwa maofisa wa jeshi la polisi Tanzania na kuwajengea uwezo wa kiuweledi kwa ajili ya utendaji muhimu wanaotarajia kutoa katika mchakato wa uchaguzi. Ulinzi na Usalama wa haki za binadamu ni sehemu timilifu ya zoezi la kila siku la kazi za Jeshi la Polisi. Hata hivyo katika mchakato wa uchaguzi, ambao ni utekelezaji wa kiwango cha juu kabisa cha haki za kidemokrasia kwa wananchi, ulinzi na usalama na uangalizi wa haki za binadamu unaonekana kuwa ni jambo linalotiliwa mkazo zaidi.

Kanuni za haki za binadamu kwa kawaida zinajumuisha kanuni zilizokubalika za usawa na za haki. Mchakato wa uchaguzi unahusisha hatua tatu muhimu: uendeshaji wa chaguzi pindi panapokuwepo mikutano ya hadhara, maandamano, n.k. yanayofanywa na vyama vya siasa vinavyopingana, siku ya uchaguzi wakati wananchi wanapopiga kura ilihali jeshi la polisi linaombwa kuhakikisha upigaji kura unafanyika katika mazingira ya amani na utulivu na kipindi cha baada ya uchaguzi pindi wananchi wanapotumia namna tofauti ya kueleza maoni na mawazo yao. Hatua hizi mbili ni hatua zenye changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya jeshi la polisi. Maofisa wa Jeshi la Polisi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuvinjari na kufanya mashauriano katika pande zote zenye maslahi pingamizi kwa usawa na kutoonyesha upendeleo wowote. Juu ya yote wanatakiwa kujiona kama warahisishaji wa mchakato wa kidemokrasia na kujitahidi kuepuka kuchukua hatua zisizokuwa za msingi jambo ambalo linaweza kuzuia zoezi la haki za kidemokrasia kupatikana kwa wananchi.

Shughuli za kipolisi na utekelezaji wa sheria zikifanywa kwa weledi, kwa kweli ni utekelezaji wa ulinzi na usalama wa haki za binadamu. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwahi kuridhia na kuingiza sheria nyingi kabambe za Kimataifa zinazolenga kulinda haki za binadamu. Mifano michache inatosha kudhihirisha jambo hili. Mswada wa Haki ambao ni sehemu ya Katiba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ([1]1) ni kielelezo bayana cha utiifu kwa Tamko la Watu Wote la Haki za Binadamu, Hati Rasmi ya Kimataifa kwa ajili ya ulinzi wa haki za binadamu. Aina ya haki mashuhuri zilizomo katika katiba zote mbili ni Haki ya Uhuru wa Kukusanyika, Uhuru wa Ushirikiano, Kushiriki katika Masuala ya Umma (ya kisiasa), Uhuru binafsi, kwa kutaja hii michache. Mbali zaidi haki ya kuishi kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Kimataifa unaohusu Haki za Kiraia na za Kisiasa zikielezwa bayana na sheria za Tanzania na Zanzibar zikikataza mauaji na vitendo vingine vinavyoshabihiana na hivi vinavyotoa vitisho dhidi ya maisha au makosa kama yanavyoweza kuwa, na haki ya kumiliki mali zinatetewa na sheria zikikataza uingiliaji usiokuwa wa msingi katika mali za wananchi.

Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria hizi, litakuwa linachangia siyo kwa uchache ulinzi na usalama wa haki za binadamu. Kwa hiyo, shughuli za kipolisi ni mpango mkakati dhahiri kwa ajili ya ulinzi wa haki za binadamu. Ama kwa hakika maofisa wa polisi wako mstari wa mbele katika ulinzi na usalama wa haki za binadamu.

1 [1] Tazama Sehemu ya Kwanza I na hasa ya Sehemu ya III ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sura ya I na ya III ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika kuhakikisha ufanisi na ukamilifu wa shughuli za kipolisi, uangalizi wa haki za binadamu kwa maafisa wa Jeshi la Polisi unahamasisha shughuli za kipolisi kwa namna nyingi. Pindi maofisa wa polisi wanapoangalia haki za binadamu watahesh imika na juu ya yote watapata ushirikiano toka kwa wananchi. Ushirikiano na Umma ni jambo muhimu sana katika kugundua vitendo vya kihalifu. Hata hivyo ushirikiano na umma, siyo tu utalindwa pale polisi wanapoheshimika na kuaminiwa na wananchi.

Kitabu hiki kinachohusu Haki za Binadamu ni mchango muhimu kwa ajili ya weledi wa maofisa wa Jeshi la Polisi Tanzania, siyo tu katika usimamizi wa kidemokrasia wa mchakato wa uchaguzi bali pia katika utendaji wa kila siku wa majukumu yao. Ni matumaini yangu ya dhati kwamba sisi sote kitabu hiki ni lulu kwetu na juu ya yote tutakichukulia kama kitabu cha marejeo katika kukuza mienendo ya kipolisi ya kidemokrasia ambayo ni lengo kuu la Jeshi la Polisi Tanzania.

ERNEST JUMBE MANGU
INSPEKTA JENERALI WA POLISI.

# MALENGO YA PROGRAMU YA MAFUNZO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, JINSIA NA WAJIBU WA JESHI LA POLISI WAKATI WA CHAGUZI

Lengo la programu ya mafunzo haya ni kuwapa maofisa wa polisi ujuzi muhimu:

- Ili kuendesha jukumu lao "asilia" kama walinzi wa amani katika muktadha wa ongezeko la juu la wasiwasi wakati wa uchaguzi;
- Ili kuhakikisha maofisa wa polisi wanasaidia kulinda usalama na uadilifu wa mchakato wa uchaguzi, washiriki, taasisi na matokeo;
- Kuwa na mwenendo mzuri wa mahusiano na wadau katika mchakato wa uchaguzi (kwa mfano maadili ya kutopendelea upande wowote, uangalifu shughuli za kipolisi kwa weledi);
- Kuhakikisha kwamba maofisa wa polisi wanahabarishwa kuhusu mahitaji mahsusi na madhaifu yanayoweza kuwa na athari juu ya baadhi ya watu na sehemu za jamii, na kuwa na fursa ya kutoa majawabu kwa mahitaji hayo ipasavyo;
- Kuhakikisha wananchi wote wanapata fursa ya kutekeleza haki zao za kidemokrasia kwa usawa, bila kujali hali yao ya kijamii, utambulisho wao wa kijinsia, umri, ulemavu au jambo lolote lile;
- Na kutekeleza majukumu mahsusi siku ya kupiga kura mathalan kusindikiza masanduku ya kupigia kura.

# SURA YA 1

## Utangulizi kuhusu haki za binadamu

1

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya kwanza.

1.1. Utangulizi

1.2. Haki za binadamu nini?

1.3. Ni nini jukumu la maofisa wa polisi?

1.4. Kwa nini za haki za binadamu ni muhimu kwa maofisa wa polisi?

1.5. Ni jinsi gani Maofisa wa Polisi wanawanyima watuhumiwa /wahalifu haki za Binadamu?

1.6. Hati Rasmi za Kimataifa za haki za binadamu zinazotumika kwa Maofisa wa Polisi

1.7. Umuhimu wa viwango vya kimataifa kwa ajili ya Jeshi la Polisi Tanzania

1.8. Muhtasari/Maswali kwa ajili ya tathmini binafsi

**Malengo ya mafunzo katika Sura ya 1**

**Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-**

- Kujadili jukumu la maofisa wa polisi katika kutii na kulinda haki za binadamu
- Kueleza maana ya haki za binadamu
- Kujadili umuhimu wa sheria za kimataifa kwa ajili ya Jeshi la Polisi Tanzania
- Kujadili jinsi gani maofisa wa polisi wanaweza kuwanyima watuhumiwa kupata Haki za Binadamu

## 1.1. Utangulizi

Haki za Binadamu zinaunda misingi kwa Jeshi la Polisi ambalo litatumika na kulinda jamii za kitanzania kwa namna isiyopendelea na kwa uweledi. Ni jambo la muhimu kwa maofisa wa polisi kuheshimu haki za binadamu za watu wote wanaoshirikiana nao kila siku na watu wote walioko chini ya ulinzi na uangalizi wao, pia ni muhimu kwa jamii kuelewa jukumu la maofisa wa polisi. Vile vile ni muhimu sana hasa katika kipindi cha uchaguzi ambako maofisa wa polisi wanatarajia kusimamia utekelezaji wa sheria, kuheshimu haki za kila mtu bila upendeleo kwa mtu yeyote na kwa uweledi.

Maofisa wa polisi wana jukumu muhimu la kulinda haki za binadamu kwa sababu wanashughulika na watu katika shughuli zao za kila siku, hasa watu ambao wanashukiwa kuwa walitenda makosa ya jinai na watu ambao ni manusura wa vitendo vya makosa ya jinai. Na hali hii inapewa umuhimu wa juu hasa wakati wa uendeshaji wa uchaguzi, pindi na baada ya mchakato wa uchaguzi kipindi ambacho watu wanakuwa na hamasa kubwa ya kujieleza, wanaitisha mikutano, mikusanyiko ya makundi na maandamano. Kwa hiyo ni muhimu sana kwa maofisa wa polisi kuelewa jukumu lao kama maofisa wa utekelezaji wa sheria na pia kama walinzi wa haki za binadamu. Maofisa wa polisi wanatakiwa pia kuelewa kanuni za msingi za utekelezaji wa majukumu yao wakiwa wanazingatia haki za binadamu kama msingi wa matendo yao.

Maofisa wa polisi wanaweza kuwa katika uhalali wa kuzuia kisheria baadhi ya haki za msingi za watu, hasa kwa watu wanaotuhumiwa kutenda kosa la jinai, kwa mfano wanapokamatwa, wanapowekwa kizuizini, pindi upelelezi na upekuzi unapopofanyika, na pindi wanaposimamia mikusanyiko ya makundi ya watu ili kuhakikisha utulivu wa umma unakuwepo. Hata hivyo kuna mambo kadha wa kadha ya kuzingatia unapozuia watu haki kadhaa.

*Sura hii ni utangulizi wa msingi na tutajadili kwa ujumla kuhusu haki za binadamu, ni jinsi gani ziliweza kuasisiwa, tutaangalia baadhi ya nyaraka muhimu za kimataifa zinazohusu haki za binadamu, haki za binadamu katika utungaji wa sheria katika Jumuiya ya nchi za Madola nchini Tanzania na jinsi gani ni muhimu na kwa namna gani maofisa wa polisi wanaweza kuzuia haki za watuhumiwa. Baadhi ya haki za binadamu zitajadiliwa kwa mapana na marefu katika sura zingine.*

## 1.2. Nini maana ya Haki za Binadamu ?

Kuna tafsiri nyingi za haki za binadamu na watu wanatofautiana kuhusu umuhimu wa haki mbalimbali. Haki za Binadamu zimewahi kutafsiriwa kama 'kanani yaliyokubalika kwa ujumla wa usawa na haki ' au 'haki za kimaadili zinazomilikiwa kwa usawa na watu wote kwa sababu ni binadamu'. Ikimaanisha kwamba haki za binadamu ni za watu wote. Kuna kanuni chache zinazoweza kutumika ili kufafanua haki za binadamu.

➢ **KUTOA ULINZI NA USALAMA KADRI IWEZEKANAVYO**

Haki za binadamu ni **ulinzi na usalama kadri iwezekanavyo a**mbao binadamu wote wana haki kuupata kwa sababu ni binadamu. Haki za binadamu zinatoa utambuzi wa kimaadili wa utu na usawa wa watu wote na umuhimu wa kuwapa watu wote fursa ya kujiendeleza kikamilifu.

➢ **HAKI YA ASILI**

Binadamu wanazaliwa wakiwa huru na sawa katika utu na haki – ikimaanisha kwamba haki zao ni za **asili** – siyo za kupewa, kununua, kupata au kurithi. Kwa sababu tu umezaliwa una haki za binadamu.

➢ **HAKI MAHALI POTE NA KWA WOTE**

Haki za binadamu zinatumika kwa binadamu wote. Haki za binadamu ni kanuni kwa ujumla zinazokubalika. Haki za binadamu ni sawa kwa wote bila kujali mbari, rangi, tofauti ya kimaumbile ( kike/ume), jinsia, imani za kidini, asili ya kikabila, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, itikadi zao za kisiasa au itikadi zingine, asili ya kijamii au ya kitaifa – ni za watu wote kwa kuwa ziko sawa kwa kila mtu ulimwenguni. Pia zinalindwa katika nyanja za kimataifa.

➢ **ISIYOONDOLEWA**

Haki za binadamu haziwezi kuondolewa au kutolewa – ni haki zisizoweza kuvuliwa. Haki za binadamu haziwezi kukanwa, kupotezwa. Hata hivyo baadhi ya haki za binadamu zinaweza kuwekewa mipaka – ila tu kwa kukubaliana na sheria za jamii ya kidemokrasia na kwa kiwango cha lazima ili kulinda haki za wengine. Kanuni za usawa, uhalali, uwajibikaji na ulazima zitawaongoza maofisa wa polisi pindi wanapomnyika mtu haki. Maofisa wa polisi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuthibitisha vitendo vyao na pia kubainisha mienendo yao ya kwamba ni ya mantiki katika hatua walizozichukua.

➢ **USAWA**

Watu wote wana haki sawa za binadamu. Madam wewe ni binadamu una haki ya kunufaika na haki za binadamu. Kwa hiyo binadamu wote wana haki ya kupata ulinzi sawa wa haki zao na uangalizi sawa toka kwa maofisa wa utekelezaji wa sheria. Maofisa wa polisi wanaweza kutombagua mtu yeyote kwa misingi ya: kwa mfano kwa kutoa uangalizi tofauti kwa sababu ya mbari yao, jinsia, rangi, jinsi, lugha, dini,

hali ya ulemavu, maoni yao ya kisiasa au mengine, asili yao ya kitaifa au ya kijamii, mali, kuzaliwa kwao au hali nyingine.

➢ **ISIYOGAWANYIKA**

Haki za binadamu zinajikita juu ya kanuni ya heshima kwa utu wa binadamu. Ili kuishi katika hali ya heshima ya utu, binadamu wote wana haki ya uhuru, usalama na viwango stahifu vya maisha wakati wote sawa – haki za binadamu haziwezi kugawanyika, zinaungana na zinategemeana, **hazigawanyiki**.

➢ **HAKI ZA MSINGI**

Maisha, utu, na tunu zingine za kibinadamu zinategemea haki hizi za binadamu. Haki za binadamu zinaunda msingi wa kila mwanadamu.

➢ **HALISI**

Haki za msingi ni halisi na haziwezi kuwa finyu. Chini ya msingi wa Sheria za Kimataifa ni haki ya kuishi, haki ya kuwa huru dhidi ya mateso, haki ya kuwa huru dhidi ya utumwa na haki ya kutendewa kwa misingi ya utu. Hata hivyo kuna haki kadha wa kadha za binadamu zinazoweza kubinywa ikiwa zitakwenda kinyume na maslahi ya kijamii ikionekana kuna umuhimu wa kutosha wa kufanya hivyo, katika hali mahsusi, kwa wakati finyu na kwa madhumuni ya lazima kabisa.

➢ **WAJIBU WA DOLA**

Haki za binadamu ni utambuzi wa kisheria wa **lazima** wa Dola kutoa na kuhakikisha haki hizi kwa binadamu walioko chini ya udhibiti wao.

Maadili haya yanatakiwa kulindwa na kuendelezwa. Haki za binadamu zinaweza kulindwa kwa kupitia Katiba, mswada wa Haki au kwa kupitia sheria za kawaida za nchi. Nchini Tanzania kuna sheria mahsusi inayolinda haki za binadamu. Kila mtu ana haki ya kutekeleza haki, ila kuna wakati haki za binadamu zinaweza kubinywa au kuwekewa mipaka ikiwa zitapingana au zitaingilia haki za watu wengine. Ni muhimu pia kuziheshimu haki za binadamu za watu wengine ili pia wao waweze kuziheshimu za kwako.

## 1.3. Nini wajibu wa maafisa wa polisi?

Ofisa wa polisi ni mtumishi wa kutekeleza sheria na kulingana na Ibara ya 1 ya Kanuni ya Tabia Njema ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Watumishi wa utekelezaji wa sheria:

"Watumishi wa utekelezaji wa Sheria wakati wowote ule watatekeleza jukumu walilopewa kwa mujibu wa sheria, kwa kuitumikia jamii na kuwalinda watu wote dhidi ya vitendo visivyokuwa vya kisheria, kwa kiwango kikubwa cha uwajibikaji kutokana na taaluma zao."

Jambo hili linamaanisha kwamba maofisa wa polisi wanatakiwa wakati wowote ule kuheshimu na kulinda sheria. Siyo tu sheria za ndani ya nchi bali hata viwango na mifano iliyokubalika kimataifa. Maofisa wa polisi wote wanatakiwa kuziheshimu haki za binadamu za watuhumiwa

wote, mbali na hili wanatakiwa pia kuzilinda haki za binadamu za kila mtu, Jambo hili pia litumike katika kipindi cha uchaguzi.

## 1.4. Kwa nini haki za binadamu ni muhimu kwa maofisa wa polisi?

Wanadamu wote wana haki za binadamu za msingi, bila kujali umri wao, jinsia, uwezo au ulemavu wao, asili yao ya kijamii au ya kiuchumi, itikadi yao ya kisiasa au asili yao ya kikabila au imani yao ya kidini. Haki hizi zinatakiwa kuheshimiwa na kulindwa, bila ubaguzi dhidi ya kundi lolote au watu wowote wale. Ubaguzi unamaanisha uangalizi usiokuwa sawa, wa upendeleo au wenye kusababisha madhara kwa watu au makundi ya watu, kwa mfano ubaguzi unaotendeka ukizingatia umri, jinsia, asili ya kikabila au uwezo/ulemavu. Katiba ya Tanzania inapiga marufuku ubaguzi wa aina yoyote ile na sheria nyinginezo, sera za kiserikali, mipango kazi na hati rasmi zingine zinayoshabihiana na hizo mbali zaidi zinaainisha ulazima wa kuweka mkazo juu ya mahitaji ya wanawake, watu wenye ulemavu, vijana na makundi mengine dhaifu.

Wananchi wote wana haki sawa na wanatakiwa kutendewa kwa usawa na kuzingatia sheria. Kuhakikisha usawa na kutowabagua watu wakati mwinginei kunaweza kumaanisha kuwatendea watu kwa utofauti ili kuhakikisha wana uwezo wa kutumia haki zao, kwa mfano, kuwasaidia watu wenye ulemavu katika kufikia maeneo ya huduma, au kuhakikisha kwamba wazee na wanawake wajawazito hawakumbani na hali ya usumbufu (kwa mfano kupanga foleni kwa muda mrefu wakati wa kupigia kura).

Maofisa wa polisi wana nafasi ya kipekee. Wanafanya kazi na watu waliovunja sheria na waliowanyima watu wengine kupata haki zao za binadamu. Na hasa katika kipindi cha uchaguzi ambako vyama mbalimbali vinavyoshindana vinajaribu kubezana na kuzuiana kufanya mikutano, maandamano, mikusanyiko ya hadhara, ambako wanadhihirisha haki zao za kujieleza kwa uhuru au za kujumuika na vyama vyao vya kisiasa. Katika kipindi hiki maafisa wa polisi wanatakiwa kuwa waangalifu zaidi ili wasionekane wanaegemea upande mmoja wa kikundi fulani au chama cha kisiasa. Maofisa wa polisi wanatakiwa siyo tu kutopendelea upande mmoja ila wanatakiwa kuonekana kutoegemea upande wowote ule. Katika muktadha wa chaguzi, wanatakiwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata fursa ya kupiga kura/kushiriki katika michakato ya kisiasa, isiyokuwa na ubaguzi, isiyokuwa na uovu wa maneno au wa kimaumbile, bughudha, na vurugu, zikijumuisha masumbufu ya kingono au ya kijinsia.

Wakati polisi wanapokabiliana na wanajamii hasa ikiwa watu hawa ni watuhumiwa, polisi wana jukumu kubwa na muhimu la kuheshimu, kulinda na kuendeleza haki za binadamu za msingi za kila mtu. Bahati mbaya maofisa wa polisi siyo tu wana jukumu la kuheshimu na kulinda haki za binadamu, ila wanakuwa sehemu ya ukandamizaji wa haki za binadamu za watu. Kwa hiyo ni jambo la muhimu sana maafisa wa polisi kujua na kuelewa jukumu lao katika kuheshimu na kulinda haki za binadamu. Maofisa wa polisi hawatakiwi siyo tu kujua haki za watuhumiwa au watu waliowekwa kizuizini, ila wanatakiwa kujua jinsi ya kuzitumia haki hizi, na wanatakiwa kung'amua jinsi ya kulinda na kuheshimu haki hizi, dhidi ya bughudha inayofanywa na watu wengine, ikijumuisha ukiukwaji wa haki na maafisa wa polisi wengine.

Taswira nyingine ya haki za binadamu ambayo pia ina umuhimu wake kwa mashirika ya kipolisi ni jambo la kutambua kwamba maafisa polisi wao pia ni wanadamu, na kwa hiyo wao pia wana haki za msingi za binadamu zinazotakiwa kuheshimiwa na kulindwa. Kwa mfano haki ya maafisa wa polisi kuwa na mazingira mazuri ya kufanya kazi. Jambo hili linajumuisha pia

haki ya maofisa wa polisi wote kutendewa kwa heshima na bila ubaguzi, na bila kuangalia cheo chake, nafasi yake, umri, jinsi, wasifu wake wa kijamii, wa kidini au wa kikabila na uwezo wake au hali yake ya ulemavu.
Huduma za kipolisi pia zinatakiwa kutolewa kwa namna ya kuheshimu kanuni na kuwawezesha watu wenye mahitaji maalumu kufikia huduma hizi. Kwa mfano, wakati wa kusikiliza shauri za uovu wa kingono au wa kijinsia na uovu dhidi ya mtoto, kesi hizi zinatakiwa kusikilizwa katika mazingira yanayohakikisha usiri, wakati mwingine kwa mfano kuna wazee na watu wenye ulemavu hawawezi kufikia ofisi ya polisi kutokana na uwepo wa ngazi ndefu.

Maofisa wa polisi pia wanatakiwa kuheshimu na kulinda haki za wanusurika na zile za makundi dhaifu katika jamii. Wako pale kuilinda na kuitumikia jamii ambamo wanafanya kazi. Katika muktadha wa chaguzi, makundi mahsusi yanaweza kukabiliana na mahitaji maalumu na madhaifu au vitisho vinavyotakiwa kufahamika na maofisa polisi na, ikiwa kuna ulazima na wakipewa mamlaka ya kufanya hivyo, wanaweza kukidhi mahitaji hayo. Hawa kwa mfano wanaweza kuwa wanawake, wazee au watu wenye ulemavu ambao walinyimwa haki yao ya kidemokrasia, vijana wanaosukumwa kujiunga na makundi ya vijana ya vyama vya kisiasa; wagombea wa kike ambao wanabughudhiwa kwa maneno na kushambuliwa, au vitisho; watu wenye ulemavu wa ngozi au wenye albinism, watoto au wanaume/wanawake wanaolengwa kutokana na imani za kichawi; watu wanaosumbuliwa kingono iwe katika maandamano ya kampeni au pindi wanapopiga kura; mashabiki wa kweli au wakereketwa wanaoshukiwa kuwa wa chama kimoja wanaoshambuliwa au kutishiwa na wakereketwa wa chama kingine au watu wasioshiriki wakijikuta katikati ya masumbufu au vurugu kati ya wakereketwa wa vyama shindani.


Maofisa wa polisi wanaweza kuonekana kuwa mstari wa mbele wa ulinzi wa haki za binadamu. Haki hizi haziwezi kuondolewa kiholela na bila kutoa ufafanuzi wa kisheria. Katika mazingira fulani, kwa mfano ikiwa mtu atavunja sheria na kutenda kosa la jinai baadhi ya haki za binadamu zinaweza kubinywa na maofisa wa polisi, kwa mfano kushikwa, kuwekwa kizuizini, kutumia nguvu, kufanya upekuzi, kwa kutaja tu haya machache. Wakati haki hizi zinapofanywa kuwa finyu kuna mambo kadha wa kadha yanayotakiwa kuzingatiwa. Ikiwa ufinywaji huu unatakiwa kuwa wa lazima, unaokubalika kisheria,unaothibitishwa na unaolingana na kosa, na tabia za maofisa wa polisi zinatakiwa kuwa za kimaadili na pia ni muhimu kutambua kwamba maofisa wa polisi wanaweza kuwajibishwa kutokana na matendo yao. Maofisa wa polisi wanapaswa kujua na kuelewa haki za kila mtu katika jamii. Sababu ya jambo hili ni kwamba maofisa wa polisi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuelewa, kuheshimu na kulinda haki za binadamu za kila mtu wanaoshughulika naye au ambaye yuko chini ya uthibiti wao au uangalizi wao. Wakati wanapofanya kuwa finyu haki za watuhumiwa wa uhalifu wanatakiwa kuelewa jinsi gani wanatakiwa kutumia kanuni za haki za binadamu na katika mazingira gani wanaweza kubinya haki.

## 1.5. Ni jinsi gani maofisa wa polisi wanaweza kubinya haki za binadamu za watuhumiwa wa makosa ya jinai?

Maofisa wa polisi wana nafasi ya kubinya kiasi cha haki za watuhumiwa wanaosadikiwa kutenda makosa ya jinai kupitia kwa mfano kwa kuwashika na kuwaweka kizuizini, kufanya upelelezi, upekuzi na shughuli zingine za kipolisi mathalan kuhakikisha usalama wa umma unakuwepo. Hali hii haitakiwi kamwe kufanyika bila utoaji wa maelezo. Kwa hivyo ni jambo la muhimu pia kwa maofisa wa polisi kujua ni kiasi gani cha haki kinatakiwa kuakisiwa wanaposhughulika na washukiwa wa matukio ya kihalifu. Wanapoakisi haki za watuhumiwa, maofisa wa polisi

wanatakiwa daima kutenda kazi yao katika mipaka ya kisheria ***(uhalali)***. Wanatakiwa pia kutenda katika hali ya ulazima **(ulazima),** kwa mfano wanatakiwa kutumia nguvu kiasi au matendo ya lazima ili kusuluhisha au kushughulikia hali au tatizo fulani ***(uwiano),*** na pia ni muhimu kwa maofisa wa polisi kutenda kwa kuzingatia maadili na kukumbuka kwamba baada ya kila tendo la ofisa wa polisi kutakuwepo na swala la uwajibikaji kuhusu matendo yao ***(uwajibikaji).***

**Herufi pacha nne za U inarahisisha kukumbuka mambo yanayotakiwa kutiliwa maanani pindi haki za binadamu zinapoakisiwa.**




Daima ni jambo jema kupima matendo ya maofisa wa polisi.

## 1.6. Hati Rasmi za Kimataifa za Haki za Binadamu zinazotumika kwa maofisa wa polisi

Kuna nyaraka nyingi zilizo na umuhimu mkubwa katika ulinzi wa haki za binadamu dunia nzima. Kuna nyaraka mbalimbali za Kimataifa zinazoshughulikia moja kwa moja au siyo moja kwa moja kati ya maofisa wa polisi na haki za binadamu.

Baadhi ya nyaraka hizo ni

- Kanuni za tabia njema kwa Watumishi wa Utekelezaji wa Sheria
- Mkataba dhidi ya Utesaji au Ukatili mwingine, Ushughulikaji au Adhabu isiokuwa ya Kibinadamu (Umoja wa Mataifa 1984) na Itifaki yake ya Hiari (Umoja wa Mataifa 2002)
- Kiasi cha Kiwango cha Kanuni za Kuhudumia Wafungwa
- Kanuni ya Kutumia Nguvu na Silaha za Moto
- Kanuni za Ulinzi wa watu wote walioko chini ya aina zote za kizuizi au kifungo
- Mkataba wa Kimataifa unaohusu uondoaji wa aina yoyote ile ya Ubaguzi wa rangi/kimbari
- Mkataba unaohusu Haki ya Mtoto
- Mkataba unaohusu uondoaji wa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW)
- Kanuni za Msingi za Haki kwa Wanusurika wa Kosa la Jinai na Uovu wa Kutumia Nguvu
- Hati ya Afrika ya Haki za Binadamu na za Watu ya mwaka 1981 (ACHPR); na Itifaki ya Kiafrika ya Haki za Binadamu na za Watu inayohusu Haki za Wanawake

Barani Afrika (Itifaki ya Maputo),

Vyombo vyote hivi vina ulazima kisheria kutekelezwa na Dola ambazo zilizosaini mikataba hii. Tanzania ilitia sahihi mikataba yote hii ya kimataifa na kuingiza kanuni hizi katika sheria za ndani. Ikimaanisha kwamba Tanzania kama nchi pamoja na Jeshi lake la Polisi zinalazimika kuheshimu haki zilizowekwa katika maazimio haya. Kwa kuridhia mikataba hii, kanuni zilizomo katika mikataba hii zinageuka kuwa sehemu ya mifumo ya kisheria ya nchi na zinatakiwa kutekelezwa katika sheria za mahali ya pale pale.

## 1.7. Umuhimu wa Sheria za Kimataifa kwa Maofisa wa Polisi nchini Tanzania

Dunia imegeuka kuwa kijiji cha ulimwengu. Pamoja na hati za kimataifa zinazotoa miongozo kwa serikali jinsi ya kuongoza, mikataba hii pia ina jukumu muhimu kwa watumishi wa serikali, na hasa kwa maofisa wa polisi nchini Tanzania. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwahi kuanzisha mchakato wa kusaini na kuridhia mikataba, makubaliano na kanuni za kimataifa zinazohakikisha haki hizi. Kutokana na hatua hiyo sheria na utendaji huo vinaingizwa katika sheria za ndani na zinakuwa sehemu ya sheria na utendaji wa utekelezaji wa sheria. Kwa hiyo ni muhimu sana kwa maofisa wa polisi siyo tu kujua na kuelewa sheria na utendaji wa nchi zao, bali pia kuzingatia sheria na utendaji wa kiwango cha kimataifa.

## 1.8. Muhtasari/Maswali

- Ni nini wajibu wa maofisa wa polisi katika kuheshimu na kulinda haki za binadamu?
- Nini maana ya haki za binadamu?
- Ni kwa nani haki za binadamu zinatumika?
- Jadili maana ya ubaguzi, kutokuwepo kwa ubaguzi, ushughulikiaji kwa usawa na na haki sawa
- Jadili umuhimu wa viwango vya kimataifa kwa jeshi la Polisi nchini Tanzania.
- Elezea maana ya kuzuia haki za binadamu?
- Jadili jinsi gani maafisa wa polisi wanaweza kuzuia haki za binadamu kwa watuhumiwa wa makosa ya jinai
- Ni maswali gani ofisa wa polisi anatakiwa kuuliza anapozuia haki za mtuhumiwa?

# SURA YA 2

## Shughuli za Kipolisi katika Jamii ya Kidemokrasia

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya pili.

**2.1. Utangulizi**

**2.2. Demokrasia ni nini?**

**2.3. Jukumu ya maofisa polisi katika jamii ya kidemokrasia?**

**2.4. Kanuni za shughuli za kipolisi katika jamii huru**

**2.5. Viwango na Utendaji wa Umoja wa Mataifa zinazotumika katika shughuli za kipolisi katika demokrasia**

**2.6. Hatua za kivitendo za Umoja wa Mataifa katika utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa**

**2.7. Muhtasari**

**2.8. Maswali kwa ajili ya kujipima**

**Malengo ya mafunzo katika sura hii**

**Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-**

- Kufafanua wajibu wa maofisa wa polisi katika dola ya kidemokrasia
- Kujadili maana ya demokrasia
- Kujadili maana ya utawala bora
- Kujadili kwa nini ni muhimu kwa maofisa wa polisi wanatakiwa kuheshimu na kulinda haki za binadamu za kila mtu katika jamii bila kujali uanachama wake wa kisiasa
- Kudadavua mwingiliano kati ya haki za binadamu na polisi jamii
- Kuelewa ni nini maana ya kutokuwepo kwa ubaguzi
- Kujadili viwango vya kimataifa vya haki za binadamu utendaji wa maaofisa wanaotekeleza sheria

## 2.1. Utangulizi

Demokrasia na haki za binadamu zinategemeana. Demokrasia ni muhimu kwa nchi yoyote ile kwa sababu inatoa fursa kwa wananchi kushiriki katika maamuzi na utungaji wa sera katika ngazi zote kuhusu maswala yanayowasibu. Wananchi wanashiriki katika uchaguzi wa viongozi na kupitia njia hii wana kauli kuhusu jinsi nchi hiyo itakavyosimamiwa na kutawaliwa.

Katika misingi ya demokrasia kuna uvumilivu wa kisiasa na watu wanaheshimu utawala wa sheria. Na hili ni jambo la msingi sana kwa utawala bora.

Katika jamii ya kidemokrasia, jeshi la polisi na jamii wanafanya kazi pamoja ili kuwa na usalama, maisha yenye heshima na yenye hadhi ya juu kwa wananchi wote, bila kujali umri wao, jinsia, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, asili yao ya kijamii au uwezo wao kiuchumi, mawazo yao ya kisiasa, asili yao ya kikabila au dini zao wala bila kujali utambulisho mwingine wowote ule wa kijamii. Mahusiano mazuri baina ya jeshi la polisi na jamii ni muhimu sana ili kuhakikisha ulinzi wa wananchi wote na pia utii wa haki za binadamu.

## 2.2. Nini maana ya demokrasia?

Neno demokrasia linatokana na maneno ya Kigiriki *demos* ikimaanisha "watu", na *kratos* ikimaanisha "mamlaka". Kuna tafsiri nyingi za neno demokrasia mathalani: serikali inayoendeshwa kutokana na ridhaa huru ya watu; au mfumo wa serikali ambamo mamlaka inajikita katika watu. Tafsiri iliyoenea sana ni ile ya utawala unaoendeshwa na watu. Demokrasia pia inaweza kuchukuliwa kama mfumo ulioratibiwa wa kimamlaka – mamlaka yaliyopewa kwa serikali na wananchi kupitia mchakato wa chaguzi huru na za haki. Demokrasia inaweza tu kuwepo katika nchi ikiwa watu watakuwa na imani nayo na kutenda misingi ya maadili ya kidemokrasia. Hizi ni haki sawa na za heshima za watu kuhusu haki za msingi za binadamu.

### Utawala Bora

Neno Utawala linatumika ili kueleza jinsi gani nchi inavyoongozwa. Ina maana pana zaidi kuliko neno Serikali. 'Serikali' inafafanua michakato ya kisiasa, kiuchumi na kiutawala inayoendeshwa

na chama cha kisiasa kilichopo madarakani. Sekta hii itaitwa sekta ya serikali. Neno 'utawala' linajumuisha sekta ya serikali na sekta zingine mbili, ambazo ni sekta ya wafanyabiashara na ile ya asasi za kiraia.

Utawala ni mchakato ambao taasisi za umma zinaendesha masuala ya umma, zinasimamia rasilimali za umma, na zinahakikisha upatikanaji wa haki za binadamu. Utawala bora unapatikana kupitia taasisi kama Bunge, Mahakama na Serikali-Jeshi la Polisi Tanzania.

Utawala bora unapatikana chini ya mfumo wa kisiasa wa kidemokrasia ambamo vitendo vya sekta zote tatu zinachangia kwa manufaa ya jamii. Jambo hili linaweza kutokea pindi sekta ya serikali na taasisi za sekta ya umma zenye ubora wa juu na pindi taifa na asasi za kiraia zenye nguvu kubwa. Utawala bora unapatikana kwa mtindo ambao kimsingi ni huru dhidi ya uovu na rushwa, na unaozingatia utawala wa sheria na haki za binadamu.

Baadhi ya kanuni za msingi za utawala bora na ufafanuzi na namna kila moja inaingiliana na aina fulani ya haki za binadamu.

| Kanuni ya utawala bora | Mwingiliano na Haki za Binadamu |
|---|---|
| Serikali na michakato ya Kidemokrasia | Serikali ya kweli ya kidemokrasia haiwezi kutokea isipokuwa tu kama watu watahakikishiwa haki za kiraia na za kisiasa, na wanapata haki hizi kwa usawa bila kujali umri wao, jinsia, mali zao, hali zao za ulemavu, viwango vya elimu, asili yao au utambulisho wao mwingine wowote ule. Hii inamaanisha wanaweza kuelezea maoni yao kwa uhuru bila uwoga wa kuwekwa kizuizini, kuteswa au kubaguliwa dhidi ya. |
| Ufanisi wa Taasisi za Sekta ya Umma | Taasisi hizi zinaendelezwa kupitia sera bora za serikali ila haziwezi kusimamiwa kwa ufanisi isipokuwa pale tu wafanyakazi wanapopata fursa ya kunufaika na haki zao za kiuchumi za kibinadamu, mathalani mishahara ya kutosheleza mahitaji yao. Mishahara hiyo inawawezesha watu kujikimu katika mahitaji yao kikamilifu na kwa hiyo kupunguza mianya ya rushwa. Jambo hili linaboresha utawala. Taasisi zinatakiwa kutoa huduma kwa wananchi wote kwa kuzingatia usawa bila kuwabagua, kwa kuheshimu haki za makundi ya watu wachache, na zinatakiwa kuwakilisha wananchi wote ikiwezekana. |
| Ubora wa juu kabisa wa utawala wa sheria na mfumo madhubuti usiokuwa upendeleo | Ubora wa juu kabisa wa utawala wa sheria na mfumo usiokuwa na upendeleo unalinda haki za kiraia za watu wote kuhusiana na mali zao, usalama binafsi na uhuru. Mfumo wa kisheria na wa kimahakama unatakiwa kuwa huru na kutokuwa na mwingiliano wa serikali ili kusimamia maslahi ya wananchi wote kwa usawa kuliko maslahi ya chama mahsusi cha kisiasa. Kwa namna hii utawala bora utalinda haki za kiraia za wananchi wote dhidi ya dola ya unyonyaji. |
| Asasi za Kiraia zenye nguvu | Asasi za kiraia zinamaanisha mchango wa watu katika uongozi wa nchi yao kwa kupitia ushiriki wao katika jamii, iwe kwa mfano kupitia vyama, shirikisho za wafanyakazi, vyama vya kutetea haki za wanawake au kupitia makundi ya kijamii. Ni vigumu kushiriki ikiwa wewe ni maskini, huna kazi, una njaa, huna makazi na huna elimu. Watu wanaoishi katika hali hii wananyimwa haki zao za kiuchumi, za kijamii na zile za kiutamaduni. Utawala bora hauwezi kufikiwa hadi pale Serikali itakapojitolea kuhakikisha haki hizi na kuwajibika katika kutoa hifadhi ya jamii kwa watu wake. |
| Kuweka kipaumbele cha juu kwa watu | Kuwekeza katika watu kunamaanisha kuandaa nguvu kazi iliyokuwa na ujuzi. Jambo hili haliwezi kufikiwa isipokuwa hadi pale haki za msingi za binadamu kiuchumi na kijamii zitakapofikiwa ikiwa ni pamoja na haki ya kupata elimu, huduma za afya, chakula na malazi bila kumbagua mtu yeyote au sehemu fulani ya jamii. |
| Usimamizi makini wa uchumi wa taifa | Serikali ambayo haisimamii vizuri uchumi wake haitakuwa na rasilimali za kutosha kuhakikisha haki za msingi za binadamu. Hata hivyo, ikiwa haki hizi hazitatolewa kwa usawa kwa wananchi wote ni vigumu kuunda taasisi zinazowajibika na zenye uwazi wa mambo ambao ni muhimu sana kwa utawala bora na maendeleo endelevu. |

## 2.3. Jukumu la Jeshi la Polisi katika Jamii ya Kidemokrasia

Shughuli za kipolisi katika jamii ya kidemokrasia zinahitaji maofisa wa polisi kuwa na utashi wa kuwajibika kutokana na matendo yao yanayozingatia kanuni ya ***Uhalali*** (dadavua ikiwa maofisa wa polisi wana mamlaka inayoeleweka na ya kisheria ya umma ya kuchukua hatua), ***Ulazima*** (ubora au hali au jambo la kuwa la lazima au hali inayoibuka nje ya matukio yanayolazimisha mwelekeo fulani wa maofisa wa polisi kuchukua hatua) na ***Uwiano*** (unasaili ikiwa hatua yoyote ile inakwenda nje ya mipaka au ni hafifu katika kushughulikia hali au tatizo fulani).

Tunapozungumzia Jeshi la Polisi katika jamii ya kidemokrasia, tunatakiwa kuzingatia "Vipengele saba" (vilivyowahi kutolewa na *Kundi la Pamoja la Kufanya Kazi kuhusu Jeshi la Polisi na Haki za Binadamu (Joint Informal Working Group on Police and Human Rights'),* linaloendelea kufanya kazi chini ya uhisani wa Baraza la Programu ya Ulaya 'Jeshi la Polisi na Haki za Binadamu miaka ya 1997 hadi 2000, 'Police and Human Rights 1997-2000'), ambavyo vinatenganisha maeneo mbalimbali ya mpangilio wa shughuli za kipolisi. Hakuna kipengele hata kimoja kitakachoangaliwa peke yake. Vinalingana kwa baadhi ya mambo licha ya kuzidiana, vipengele hivi ni:

- Tunu za msingi
- Wafanyakazi
- Mafunzo
- Utendaji wa kiutawala
- Shughuli za kiutendaji za kipolisi
- Muundo na
- Uwajibikaji

Kipengele cha *Tunu za msingi* kinatakiwa kuonekana kama 'mwavuli' unaofunika waraka wote kwa ujumla, siyo tu kuhimiza utendaji mzuri wa oparesheni za kipolisi, bali kuhimiza zaidi namna ya kusajili askari wapya, kuwapa ajira na kutoa uangalizi kwa wafanyakazi. Jinsi gani tunachanganua mahitaji ya mafunzo, jinsi gani tunashirikiana na kuwajibika kwa umma, na kwa wadau wengine, jinsi gani tuna hamasa ya kutoa haki na amani.
Kipengele cha *Tunu za msingi* kinaibua maswali, yanayohusiana na falsafa ya shughuli za kipolisi katika jamii ya kidemokrasia.

Zifuatazo ni njia ambazo Jeshi la Polisi linaweza kutumia ili kuhakikisha demokrasia inatumika katika jamii pindi uchaguzi unapofanyika:

- Kurahisisha uchaguzi huru na wa haki
- Kutoa kwa wananchi wote haki sawa bila kujali umri wao, jinsi, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, asili ya kijamii au hali ya kiuchumi, itikadi zao za kisiasa au asili ya kikabila wala imani zao za kidini au utambulisho wowote walionao kijamii, na fursa ya kupiga kura na/au kupigiwa kura
- Kuwasaidia watu wenye hamasa ya uchaguzi ambako utawala wa sheria unatumika, mchakato ambao unatoa majawabu kwa maslahi ya wananchi wake.
- Maofisa wa Polisi hawatakiwi kuwa wafuasi wa chama na kutoshawishika na chama kimoja cha kisiasa
- Tambua kwamba kuna uhuru wa kutoa mawazo na wa kujieleza

- ➢ Heshimu haki ya kupata habari toka kwa vyombo vya habari vya umma
- ➢ Heshimu katiba ambayo sheria zake zinazingatiwa katika ngazi zote
- ➢ Uwezo wa kuvumilia mawazo ya watu wengine hata kama yanatofautiana na ya kwako
- ➢ Toa ulinzi bila kujali kabila, dini wala chama cha kisiasa, umri, jinsi, uwezo au hali ya ulemavu, asili ya kijamii au uwezo wa kiuchumi, bila kuzingatia itikadi ya kisiasa au asili ya kikabila wala dini, au vielelezo vingine vya utambulisho wa kijamii. Wagombea na wapiga kura wanatakiwa kutumia haki zao za kidemokrasia bila ubaguzi, bugudha ya maneno au kimaumbile, usumbufu na ukatili ukiwemo wa kingono au wa kijinsia, dhidi yao au familia zao au watu wao wa karibu.

**Chaguzi huru na za haki**

Uchaguzi unatamkwa kuwa huru na wa haki pindi;

- ➢ Uchaguzi haupo chini ya udhibiti au mamlaka ya chama kimoja, mgombea mmoja au kikundi kimoja cha watu.
- ➢ Wagombea na wapiga kura wakiwa na fursa ya kufanya kile wanachotaka kufanya sambamba na hayo wakizingatia sheria ya uchaguzi
- ➢ Kila mtu anashughulikiwa kwa usawa na kulingana na utawala wa sheria bila ubaguzi
- ➢ Matokeo ya uchaguzi yanakubalika na yanafaa katika hali mahsusi

## 2.4. Kanuni ya shughuli za kipolisi katika jamii ya kidemokrasia

Taasisi inayofanya kazi ya kutekeleza sheria katika jamii huru ni ile ambayo:

1. Inayozingatia kwamba ***Jeshi la polisi linatumikia watu:*** na siyo dola

2. Jeshi la polisi linatakiwa kutii kanuni na sera za idara. Jeshi la Polisi linatakiwa kufanya shughuli zake kwa kuzingatia usawa kwa watu wote **bila kujali** umri wao, jinsi, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, chimbuko lao la kijamii au la kiuchumi, itikadi yao ya kisiasa au ya kidini au kikabila au viashiria vingine vyovyote vile vya utambulisho wa kijamii ***au sifa za kibinadamu zisizokuwa za kitabia*:**

*Kutoa heshima* kwa haki za binadamu na kwa utu wa kibinadamu wa polisi na watu kwa ujumla;
*Kuunga mkono* zoezi huru la upatikanaji wa haki za kisheria kwa watu wote; na
*Kuhamasisha utekelezaji wa usawa na usiopendelea* wa sheria hizo katika mamlaka yake ya kisheria;

3. Majukumu yote ya kipolisi yanatakiwa ***kufuata kwa msisitizo masharti ya kisheria*** yaliyomo katika Katiba ya Taifa, sheria za Jeshi la Polisi, Kanuni na taratibu za makosa ya jinai na sheria zingine zinazotumika;

4. Jeshi la Polisi linatakiwa kuutumikia umma badala ya kuzuia umma kudhihirisha utamaduni na uhuru wake.

5. Jeshi la Polisi linatakiwa kufikiria jinsi ya kuzuia uhalifu kabla haujatokea ili *liaminike na umma, kusimamia utaratibu wa umma*, *utulivu wa ndani* na ***ubora wa maisha unaokubalika*** *kwa watu wote ndani ya nchi*;

6. Ikiwezekana Jeshi la Polisi linatakiwa kushirikiana na jamii ili ***kubaini na kutatua matatizo ya jamii*** **ambayo yanatoa** ***fursa za kubaini tabia za kiuhalifu*;**

7. ***Jeshi la Polisi litafanya upepelezi yakinifu*** na ripoti za mwenendo wa kiuhalifu kwa malengo ya ***kubaini na kuwashika*** wahalifu ***ili mahakama iweze kubaini kikamilifu kwamba wana makosa au hawana hatia.***

8. Jeshi la Polisi linatakiwa kufanya kazi na maofisa wa Mahakama, Majaji na Waendesha Mashtaka kwa upatanifu ili kuhakikisha kwamba watu waliopelekwa katika mfumo huo wanashughulikiwa kulingana na ***sheria, kikamilifu na kwa misingi ya haki*;**

9. Kupitisha na kuhimiza matumizi ya ***nguvu ya yasiyosababisha kifo*** yanayofanywa na askari isipokuwa tu kwa uangalifu mkubwa katika mazingira yaliyotafsiriwa ili kukamilisha lengo halali na la kisheria, na la kijamii na matumizi ya *nguvu ya kusababisha kifo* na askari wake ***ikiwa yanalenga kuokoa maisha ya mtu yeyote, hali hii ikijumuisha askari wa Jeshi la Polisi, dhidi ya tishio inayodhaniwa kusababisha kifo kinachokaribia kutokea au jeraha kubwa,*** au chini ya mazingira mengine yaliyoandikwa katika sheria za nchi, au sheria ya umma;

10. Kuendeleza, kufanya shughuli zao chini ya mwongozo wa ***kanuni za tabia njema, desturi, sera na taratibu*** **zinazotoa mwongozo makini** kwa wafanyakazi wa Jeshi la Polisi katika tabia zao na katika utendaji wa majukumu waliyopewa sanjari na hayo yakiwadhibiti ili ***wawajibike*** kutokana na jinsi gani walitekeleza majukumu yao;

11. Kuhusu shauri za ukatili wa kingono na wa kijinsia (SGBV) na /au ukatili dhidi ya mtoto (CA), maofisa wa polisi wanatakiwa kuitikia kwa kuzingatia Utendaji wa ubora wenye viwango (SOPs) uliowekwa ili kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia (2012)" haraka iwezekanavyo na kuwasilisha shauri hilo kwenye Dawati lawa Jinsia na Watoto (GCDs) ambako Maofisa wa Polisi waliopata mafunzo wapo.

12. Wafanyakazi wote wa Jeshi la Polisi ambao watakao heshimu kanuni hizi na kufanya shughuli zao kwa kutii sera za idara watazawadiwa kwa kupandishwa vyeo na kupewa heshima ya juu na idara, na hali hii inatakiwa kutangazwa hadharani kwa umma. Wafanyakazi wa Polisi wanatakiwa *kuhimizwa* kuheshimu kanuni hizo au kuachana na tabia mbaya

13. *Jeshi la Polisi linatakiwa kuwa tayari kukubali na kufanya upelelezi yakinifu wa malalamiko ya tabia mbaya dhidi ya maofisa wa polisi;* na:

14. *Jeshi la Polisi linatakiwa kuwaadhibu kikamilifu* wafanyakazi wake ambao kwa makusudi walikiuka kanuni za tabia njema zilizowekwa, sera na/au utaratibu. Adhabu inayofaa inaweza kujumuisha yote au mojawapo ya yafuatayo: barua ya onyo, likizo bila malipo, kushushwa cheo, uhamisho, kufukuzwa kazi au kufunguliwa mashtaka ya kijeshi/ jinai.

## 2.5. Viwango na mifano ya Umoja wa Mataifa inayotumika katika Amri na Usimamizi

Kuna viwango vya msingi vya binadamu na matendo ambayo yanatumika katika shughuli za kipolisi katika mfumo wa kidemokrasia.

- Katika kunufaika na haki na uhuru wake, kila mtu anaweza kuathirika na ufinyu wa haki hizo ikiwa tu hali hiyo itaamuliwa na sheria.[2]

- Ufinyu wa kunufaika na haki za uhuru utafanyika tu pale kwenye ulazima ili kuhakikisha utambuzi na heshima kwa haki za watu wengine, na kwa ajili ya kukidhi masharti ya maadili, utulivu wa umma na ustawi wa jumla katika jamii ya kidemokrasia.[3]

- Kila mtu ana haki ya kushiriki katika serikali ya nchi yake, bila kujali umri wake, jinsi, uwezo wake au hali yake ya ulemavu, asili yake ya kijamii au uwezo wake wa kiuchumi, maoni yake ya kisiasa au imani yake ya kidini au bila kujali kiashirio kingine cha utambulisho cha kijamii, moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa misingi ya uhuru.[4]

- Matakwa ya watu ndiyo msingi wa mamlaka ya serikali.[5]

- Matakwa ya watu yatajieleza kupitia vipindi vya awamu vya kweli vya uchaguzi, utakaokuwa wa haki sawa ya kupiga kura kwa wote.[6]

- Kila taasisi ya utekelezaji wa sheria itakuwa mwakilishi na muitikiaji na muwajibikaji kwa jamii nzima.[7]

- Kila mtu ana haki za uhuru wa kutoa maoni, kujieleza, kukusanyika au wa kujumuika.

- Maofisa[8]wote wa polisi ni sehemu ya jamii na wana kazi ya kuitumikia jamii.[9]

## 2.6. Hatua za kivitendo za Umoja wa Mataifa kwa ajili ya utekelezaji wa viwango vya kimataifa.

Umoja wa Mataifa uliwai kuandaa hatua chache za kivitendo zinazoweza kusaidia katika utekelezaji wa viwango hivi vya kimataifa kama ifuatavyo:

---

2 UDHR, ibara ya 29(2).
3 UDHR, ibara ya 29(2).
4 UDHR, ibara ya 21(1); ICCPR, ibara ya 25 (a) - (b)
5 UDHR, ibara ya 21(3); ICCPR, ibara ya 25(b).
6 UDHR, ibara ya 21(3); ICCPR, ibara ya 25(b).
7 General Assembly resolution 34/169 of 17 December 1979 (adopting the Code of Conduct) [hereinafter Aresolution 34/169"], eighth preambular paragraph, subparagraph (a).
8 UDHR, articles 19 and 20; ICCPR, articles 19, 21 and 22; Principles on Force and Firearms, principle 12.
9 Code of Conduct, article 1.

## A. Maofisa wote wa Jeshi la Polisi:

- Wakati wowote ule wanatakiwa kudhihirisha uhuru wa kisiasa na kutoegemea upande wowote ule:
- Kuwa karibu na watu katika jamii ambamo wanatumwa kufanya kazi.
- Kuwa karibu na jamii. Kwa kawaida, wasikae kituoni ilihali wangaliweza kufanya doria wakiwa na gari; wasifanye doria na gari ilihali wangaliweza kwenda kwa miguu.
- Kufanya kazi za kujitolea kwa ajili ya kutoa huduma katika jamii.
- Katika vituo vya kupigia kura, wanapotoa ulinzi katika uchaguzi, wakutane kwanza na watumishi wa uchaguzi na kuhakikisha mwenendo wa tahadhari kubwa, wa nidhamu na weledi wakiwa mbele ya umma unaopiga kura.
- Wanapofanya shughuli zao za kipolisi katika mikusanyiko na maandamano ya kisiasa, wawe wavumilivu, na wakumbuke kwamba usalama wa umma na hali kutokuwa mbaya zaidi ndiyo jambo lenye umuhimu wa juu.

## B. Maofisa wanaotoa Amri na Usimamizi:

- Weka na tekeleza sera na mikakati ya taasisi za kipolisi kwa kuheshimu maadili ya serikali ya kidemokrasia.
- Anzisha mikakati ya ushirikiano kati ya jamii na polisi, ambamo Jeshi la Polisi litaunda ubia na jamii na linaonekana kuwa sehemu ya jamii.
- Fanya mashauriano na umma ili kugundua mahitaji maalumu ya jamii ya mahali ya pale pale, yakijumuisha mahitaji ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu na pitisha mikakati ya kuitikia mahitaji hayo. Weka mkazo juu ya mahitaji na madhaifu ya makundi ya watu wachache au ya watu waliotengwa kwa mfano watoto wa mitaani kwa sababu wanaweza kuwa wanakabiliana na madhaifu mahsusi.
- Kuandaa programu za mahusiano na umma ili kuhimiza ushirikiano wa jamii na Jeshi la Polisi.
- Hakikisha kwa muundo wa Jeshi la Polisi linawakilisha makundi yote ya jamii kwa kupitia uandikishaji unaozingatia usawa bila ubaguzi na kwa kusimamia sera na mifano bora.
- Weka taratibu za uandikishaji na programu za mafunzo zilizoandaliwa kuandikisha na kuvutia utashi wa Maofisa wa Polisi na kuwa na uwezo wa kukidhi maombi ya shughuli za kipolisi chini ya serikali ya kidemokrasia.
- Fanya ushirikiano wa karibu na viongozi wa uchaguzi, viongozi wa vyama vya wafanyakazi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, yakijumuisha makundi ya wanawake, makundi ya vijana na mashirika na vyama/mashirika ya watu wenye ulemavu.
- Ikiwezekana, panga maofisa wa polisi kwa ajili ya usalama wa uchaguzi kulingana na mahitaji yaliyobainishwa na Mamlaka ya Tume ya uchaguzi.
- Panga idadi kiasi ya maofisa wa polisi wanaotosha kwa ajili ya ulinzi wa uchaguzi.

Weka mfumo unaofikiwa na umma kwa urahisi kwa ajili ya kupokea malalamiko na mazingatio ya wananchi. Mfano wa jambo hili ni mfumo wa utafiti wa wateja kwa njia ya mtandao ulioandaliwa kwa ajili ya Madawati ya Jinsia na Watoto na ulioandaliwa kwa pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania na UNFPA.

## 2.7. Muhtasari

Maofisa wa polisi wana jukumu kubwa la kutekeleza sheria katika kila jamii ya kidemokrasia. Hasa katika kipindi cha chaguzi za kidemokrasia maofisa wa polisi hawatakiwi kuegemea upande wowote ule na wanakiwa kuonyesha uweledi, wakiheshimu, na kulinda haki za msingi za binadamu za kila mtu katika nchi.

## 2.8. Maswali kwa ajili ya kujipima

- Ni kitu gani kinachounganisha haki za binadamu na shughuli za kipolisi katika jamii ya kidemokrasia?
- Nini maana ya demokrasia?
- Utawala bora unamaanisha nini?
- Kwa nini ni muhimu maofisa wa polisi kuheshimu na kulinda haki za binadamu za wanajamii wote?
- Tafadhali toa mifano ya uangalizi wa usawa?
- Eleza hali ya kutokuwepo ubaguzi unaotakiwa kufanywa na maofisa wa polisi.
- Jeshi la polisi linawajibika kwa nani?

3

# SURA YA 3

## Jinsia, Hali ya kuwa tofauti, Umoja wa Kijamii na Chaguzi

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya tatu.


**3.1.** **Tafsiri za msingi.**

**3.2.** **Hali ya kuwa tofauti.**

**3.3.** **Jinsia, vurugu na udhaifu katika chaguzi.**

**3.4.** **Mwitikio.**

**3.5.** **Maswali ya kujipima.**

**Malengo ya Mafunzo ya Sura ya 3**

**Baada ya kumaliza washiriki wataweza:-**

- Kujua maana ya jinsia na kwa nini jinsia, pamoja na mambo mengine, mahitaji ya kuzingatia katika shughuli za kipolisi.
- Kuelewa aina mbalimbali ya maovu ya kutumia nguvu dhidi ya maumbile, uovu wa kutumia maneno, uovu wa kingono au wa kiuchumi unaoweza kutukea katika kampeni za uchaguzi na jinsi gani maovu haya yanaweza kuwaathiri watu mbalimbali au makundi ya kijamii kwa namna tofauti.
- Kuelewa wajibu wa kisheria kwa kuzingati aina ya ukatili kwa umakini, na namna ya kuitikia katika ukatili ipasavyo
- Kuelewa namna maofisa wa polisi wanavyotakiwa kuelewa, kujipanga na kushughulikia aina ya vurugu katika michakato ya uchaguzi.

## 3.1. Tafsiri za Msingi

Kulingana na 'Miongozo ya uanzishaji wa madawati ya polisi ya Jinsia na Watoto' ya Wizara ya Mambo ya Ndani/Jeshi la Polisi Tanzania (Mwaka 2012), dhana za msingi zinatafsriwa kama ifuatavyo:

**Mtoto** mtu mwenye umri chini ya miaka 18.

**Uovu dhidi ya mtoto** unajumuisha: uovu dhidi ya maumbile, mathalan kumzaba kibao, kumsukuma, kumpiga ngumi, kumpiga teke, au kumchapa, au kumtishia na silaha mathalan bastola au kisu; uovu wa kihisia kumfanya mtoto kutokuwa wa thamani au kutopendwa, asiyefaa au kuthaminiwa ikiwa tu anahijika na mtu mwingine, au kumfanya mtoto kuhisi kwamba anatishika au kuwa hatarini; na uovu wa kingono mathalan kumshirikisha mtoto katika shughuli yoyote ile ili mtu mwingine aweze kufurahishwa kingono – hata kama mtoto "aliridhia". Jambo hili linajumuisha kufanya tendo la ngono, jaribio la tendo la ngono, na kumpapasa mtoto kingono. Pia inaweza kujumuisha shughuli zisizokuwa za kugusana kimwili mathalani kumfanya mtoto aweze kuangalia picha za ngono au shughuli za kingono. Pia inaweza kuhusiana na lugha ya kingono pindi unapoongea na mtoto au kumhimiza mtoto na kuonyesha tabia ya hamasa ya kingono kwa namna isiyofaa.

**Dhulma za Majumbani** inamaanisha madhara yoyote ya kimaumbile, kingono au ya kisaikolojia yaliyofanywa na upande mmoja dhidi ya upande mwingine katika tafsiri ya mahusiano ya majumbani (undugu wa kuzaliwa, wa damu, wa kuishi kinyumba, ndoa, kimapenzi au undugu wa ukoo).

**Mzee** inamaanisha mtu yeyote ambaye ana umri zaidi ya miaka sitini kama ilivyoainishwa na Sera ya Taifa ya Wazee, ya mwaka 2003

**Jinsia** inamaanisha uhusiano uliotungwa kijamii na kiutamaduni baina ya mume na mke. Uhusiano huu unabadilika kulingana na utamaduni na mahali na kadiri muda unavyopita.

**Dhulma ya kijinsia** inamaanisha uovu wowote ule wa kimaumbile, kisaikolojia, kingono au kiuchumi uliotendwa na mtu mmoja dhidi ya mtu mwingine kwa mantiki ya uhusiano wa kijinsia.

**Bughudha** inamaanisha matendo ya kurudia rudia, ya kuyumbisha dhidi ya mtu yakidhamiria kumtesa, kumdharau, au kumtusi, kumlaumu, n.k.

**Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi** linamaanisha dawati maalumu katika Kituo cha Polisi au katika eneo lolote lingine kama itakavyoainishwa na Jeshi la Polisi Tanzania lenye maofisa wa polisi waliopata mafunzo maalumu ili kushughulikia shauri za dhulma za kijinsia na zile za watoto.

**Dhulma za kingono** inamaanisha kitendo chochote cha kingono, jaribio la kupata tendo la ngono, au matendo yote yanayopelekea kufanikisha malengo ya kingono, yanayoelekezwa dhidi ya mtu kwa kutumia nguvu, na maoni yasiyokaribishwa ya kingono, bughudha au tendo la kumrubuni mtu bila kujali mahusiano ya mnusurika/Mhanga, katika mahali popote pale, yakijumuisha siyo tu nyumbani na kazini.

**Mnusurika/Mhanga** inamaanisha mtu yeyote yule aliyefanyiwa dhulma za kijinsia au uovu wowote ule uliofanywa dhidi ya mtoto.

**Dhulma** inajumuisha na haiishi tu kwa uovu wa kimaumbile, wa kihisia na kingono.

Ni muhimu sana kubaini tofauti baina ya **hali ya ke/me kibaolojia (Jinsi)** na **Jinsia**: ilihali **Jinsi** ya me/ke inamaanisha wanaume na wanawake kwa maana ya tofauti ya maumbile kibaolojia, wakati, **Jinsia** inamaanisha majukumu na nafasi katika jamii kama walivyopewa mume na mke. Kwa hiyo wanaume tofauti na wanawake tofauti watakuwa katika nafasi tofauti ya nguvu au ya udhaifu katika miktadha tofauti na kwa nyakati tofauti. Ilihali wanaume wanakuwa katika nafasi ya upendeleo dhidi ya wanawake, vipengele vingine vinaweza kuwa na umuhimu mkubwa: mwanaume mwenye ulemavu, anayeishi mitaani kama ombaomba atakuwa mbali sana katika hali hatarishi kuliko mwanasheria aliyefanikiwa kiuchumi.

Jinsia pia inaainisha kwa upande mmoja udhaifu wa watu kuhusu aina fulani ya dhulma: wanawake na wasichana wanaelekea kuathirika na vitendo vya dhulma ya kingono na bughudha, na utumiaji wa nguvu, ukijumuisha vitisho vinavyoambatana na dhulma hizo. Ila tunatakiwa kuelewa kwamba wanaume na wavulana pia wanaweza kuwa wanusura/wahanga wa aina hii ya dhulma. Matarajio kuhusu ni aina gani ya tabia inayoonekana inafaa kijamii kwa wanaume na wanawake yanaweza pia kutoa shawishi juu ya ripoti za dhulma dhidi ya jinsia na ya kingono, tukizingatia aina tofauti ya aibu na unyanyapaa unaowaathiri wahanga/wanusura wa aina hii ya dhulma ikiwa wataripoti uhalifu huu.

### 1.1. Hali tofauti

Maofisa wa Polisi kulingana na sheria wanalazimika kuwasaidia watu wote kwa usawa, na kwa hiyo wanatakiwa kuelewa mahitaji na madhaifu maalumu yanayoweza kuwaathiri watu tofauti au makundi ya kijamii kwa namna tofauti kwa kuzingatia umri wao, jinsi, jinsia, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, asili yao ya kijamii au ya kiuchumi, maoni yao ya kisiasa au imani yao ya

kidini au asili yao ya kikabila au kiashiria kingine chochote cha utambulisho wa kijamii.

Kutokana na mabadiliko ya kasi ya jamii yanayosababishwa na maendeleo ya miji, maendeleo ya kisasa na utandawazi, jamii ya Kitanzania imekuwa na watu tofauti, na maofisa wa polisi wanatakiwa kutoa majawabu chanya kwa **hali hii ya utofauti** ili kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma ya ulinzi na usalama na huduma zingine kwa watu wote kwa usawa na bila ubaguzi.

Kwa upande mmoja, inamaanisha kwamba maofisa wa polisi wanatakiwa kufunguka kwa mabadiliko haya ya kijamii na kushirikiana na kundi kubwa la watu ikiwezekana (kwa mfano kuwa sehemu ya polisi jamii), ila kwa kutoa majibu chanya kwa hali hii ya utofauti inamaanisha utoaji wa huduma madhubuti zaidi, ya kuwajibika na ipasayo. Kama Jumuiya ya Washauri mabingwa wa sekta ya Usalama ya DCAF wanavyotamka,

"Utawala wa sekta bora ya usalama unahusisha kufanikisha malengo pacha ya ufanisi na uwajibikaji:

- Ufanisi bila uwajibikaji unazaa mfumo wa kiimla ambako hali ya utulivu inadhitiwa kwa kutoa haki kafara.
- Uwajibikaji bila ufanisi unazaa taasisi hafifu zinazotoa ulinzi na usalama kwa watu wasiokuwepo.

Malengo pacha haya yanaweza tu kufikiwa ikiwa una watu wa eneo husika watahisi kwamba ni wamiliki wakuu wa ulinzi na usalama katika eneo lao. Umiliki huu unahusisha jeshi la polisi katika kuitikia kujibu mahitaji tofauti ya kiusalama ya wananchi. Pia inahitaji jeshi la polisi kuwa na taswira ya kuwakilisha watu wote wa dola husika.

Mitazamo ya jumla kwa usalama ni rahisi zaidi kufanikisha pamoja na nguvu kazi tofauti ambayo ina uzoefu mpana wa tofauti ya hali za kiusalama lakini pia ina uwezo wa kufika sehemu mbali za makundi ya watu. Watu watamheshimu ofisa wa polisi ambaye wanaweza kumbaini.

## 3.2. Jinsia , Vurugu na Udhaifu katika Chaguzi

Licha ya kuwa michakato ya uchaguzi inapaswa kuwa ya amani na ya watu wote, kivitendo unaweza kuibua nguvu ambazo zinaweza kusababisha vurugu ambazo zitawalenga au zikasababisha madhara kwa baadhi ya makundi au sehemu fulani katika jamii kutokana na umri wao, jinsi-me/kike, Jinsia, uwezo au hali ya ulemavu, asili yao ya kijamii au ya kiuchumi, maoni ya kisiasa au asili ya kikabila na kutokana na imani yao ya kidini au kiashirio kingine chochote kile cha kijamii. Kama ilivyo jukumu la maofisa wa polisi kuhakikisha chaguzi tulivu na za haki na uwezekano wa wananchi stahiki kushiriki bila ubaguzi, kuna umuhimu kwa maofisa wa jeshi la polisi kuelewa aina tofauti za vurugu zinazoweza kutukea katika michakato ya uchaguzi na kutambua makundi/watu gani wako katika hatari ya hali ya juu kuathirika na vuguvugu hizi.

Vurugu za uchaguzi zinaweza kuchukua taswira tofauti. Kulingana na maoni ya majibu ya jeshi la polisi, vurugu zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa pindi zinapotukea:

1. **<u>Wananchi wamezuiawa kushiriki kupiga kura</u>**: Hali hii inaweza kutukea kwa *mtu mmoja mmoja*, kwa mfano mume au mzazi wa kiume anamkataza mwanakaya wa kike kupiga kura, au inaweza kutukea kwa misingi fulani ya *kimpangilio* ikiwa makundi kadha

wa kadha yatazuiwa kufika katika vituo vya kupigia kura kutokana na utambulisho wao (kwa mfano kutokana na asili yao ya kikabila/kimbari, utambulisho wao wa kijinsia au uanachama wao wa kisiasa) au kutokana na maswala ya kimiundo mathalani watu wenye ulemavu au wazee hawawezi kufika katika maeneo ya vituo vya kupigia kura.

2. **Matumizi ya makusudi yanayolenga ubaguzi wa kijinsia, dhulma ya kingono, bughudha, kashfa, utumiaji nguvu au vitisho vinavyoambatana na ukatili**: Hasa wagombea wa kike, wafuasi wa kike wa chama cha kisiasa au wapiga kura wa kike wanaweza kukabiliana na kauli za ubaguzi, au katika hali ya hatari, vitisho au hata matumizi halisi ya dhulma za kingono, bughudha, kashfa au utumiaji nguvu katika michakato ya uchaguzi. Baadhi ya maovu haya yawezekana yakashinikizwa na sababu za kisiasa (kwa mfano jaribio la kumuaibisha mgombea wa kike au kutoa vitisho kwa wapiga kura), ilihali nyingine ni ya kufuata tu upepo (kwa mfano kupapasa kimahaba au aina nyingine ya bughudha ya kingono pindi watu wanapopaga foleni ya kupiga kura).

   Aina hizi za dhulma pia zinaweza kuwalenga wanaume na wavulana, kama ilivyotukea katika vurugu za uchaguzi za mwaka 2007 nchini Kenya.
   Aina hizi za vurugu zinaweza kutukea katika muktadha wa kuongezeka kwa vurugu, iwe kabla, pindi na baada ya uchaguzi, na vurugu hizi zinaweza kuwalenga watu wasiohusika na kampeni za uchaguzi. Pamoja na aina zingine za dhulma za kijinsia au za kingono, baadhi ya watu au makundi yanaweza kuwa katika ugumu wa kuamua pindi inapofika wasaa wa kuripoti dhulma dhidi yao kwa hofu ya kufunguliwa wenyewe mashtaka ya jinai. Hali hii inajumuisha wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wahamiaji wasiokuwa na vitambulisho, wanawake wanaofanya biashara ya kuuza miili yao au watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, watoto washio katika mazingira hatarishi.

3. **Unyonyaji na ukatili wa kingono** dhidi ya wagombea, wafuasi wao na dhidi ya wapiga kura wao, hasa wanawake wanaweza kukabiliana na tatizo la kutongozwa bila wao kuridhia, au kuombwa tendo la ngono au fadhila zingine zozote zile na mtu aliye na mamlaka dhidi ya mtu huyo, pindi anapoombwa na mtu yeyote apate huduma, au pindi anapotaka kupata haki yake anaombwa na mtu huyo mwenye mamlaka juu yake ampe fadhila hiyo ya kingono naye atamfanyia upendeleo.

   **Kuwalazimisha watu wajiunge katika kampeni za vurugu kwa kutumia nguvu**: Kutokana na umri wao, jinsia na hali ya kijamii, makundi kadha wa kadha au watu wanaweza kushinikizwa au kuwa katika hali hatarishi kutokana na jaribio la kuwaandikisha katika makundi yanayoelekea kusababisha vurugu kubwa. Watu wanaojikuta katika hatari ya mwelekeo huu ni vijana wanaume, na kwa kiwango fulani wanawake, na wale wote walioko katika mazingira ya kijamii na ya kiuchumi duni. Mifano ya vurugu za uchaguzi wa Kenya zilizotukea kati ya mwaka 2007-2008 na vurugu za kabla ya uchaguzi nchini Burundi mwaka 2014-2015.

4. **Hali hatarishi kutokana na vitendo imani za kishirikina**: imani za kishirikina mathalani katika uchawi, utoaji kafara wa watoto au watu wenye ulemavu wa ngozi au wenye albinism, hali hii inaweza kuwaweka baadhi ya watu katika hali hatarishi katika kipindi cha michakato ya uchaguzi pia. Watu hawa wanajumuisha wasichana au wavulana wadogo, hasa wakiwa wenyewe, watu wenye albinism, wanaume na wanawake walioko katika mazingira hatarishi (kwa mfano wanaume wagane na wajane wa kike.).

Utafiti uliofanywa na Gabrielle Bardal kwa ajili ya IFES (tazama marejeo) kuhusu vurugu za uchaguzi za kijinsia katika nchi sita (Bangladesh, Burundi, Guyana, Guinea, Nepal na Timor-Leste) unaonyesha kwamba wanawake:

- "ndiyo wanaoathirika sana na vitisho (aslimia 32 ya aina zote za vurugu dhidi ya wanawake), bughudha ya maneno (asilimia 11) na madhara ya kimaumbile na vurugu za makundi (vyote asilimia 10).
- Kulingana na aina ya manusura, wanawake ndiyo waliweza kubainika kuwa wahanga wanapojihusisha na jukumu fulani la umma (wakiwa viongozi wa chama cha kisiasa, wagombea au wafuasi ni (asilimia 48) ya aina ya wanusura wanawake walioripotiwa). Wapiga kura walikuwa kundi la pili lililoripotiwa zaidi kuwa na aina hii ya wanusura wa vurugu (asilimia 22).
- Wanawake kama wakosaji wasiokuwa wa kawaida na kusababisha vurugu katika kipindi cha uchaguzi ni kundi ndogo sana (asilimia 4 ya jumla ya matukio); hata hivyo, wanawake wanaposhirikiana na wanaume wanaunda kundi kubwa. Wakijumuishwa pamoja, hali hii inamaanisha kwamba wanawake walionekana kuwa wakosaji karibu katika robo ya matukio ya vurugu.
- Mchanganuo wa wanawake wakosaji unaonyesha kwamba wanawake walishiriki sana katika migongano ya makundi, bughudha ya maneno na maovu mengine ya vitisho/kisaikolojia. Vitendo vya wanawake katika vurugu vinahusisha matumizi hafifu sana ya silaha: asilimia 70 ya vitendo vya wanawake havikutumia silaha, vikilinganishwa na asilimia 24 tu ya vitendo vya wanaume. Na matumizi ya silaha na wanawake ni ya chini mno kuliko viwango katika takwimu zilizokusanywa."

Kulingana na utafiti huu, kuna sababu nyingi zinazoonyesha ni kwa nini aina kadha wa kadha za vurugu za uchaguzi zinawalenga wanawake:

- "kwanza, kutokana na mabadiliko ya kasi katika majukumu ya wanawake katika nchi nyingi, hali hii inamaanisha kwamba hatari za kawaida za shughuli za kisiasa zinaongezeka zikiambatana na hatari ya kupuuza wajibu na tunu za asili.
- Pili, vitisho na shinikizo za kifamilia na kijamii zinazotokea katika maeneo ya faragha hazijumuishwi katika tafiti nyingi wala haziingizwi katika mkakati wa kudhibiti vurugu za uchaguzi.
- Tatu, mifumo ya sasa inaelekea kuweka kando dhana ya jinsia na bughudha iliyosanifiwa kuzuia na kutishia wagombea, wapiga kura na wanaharakati wanawake.
- Nne, takwimu kama hizo zimeanza kurekodi vurugu za kiuchumi mathalan shinikizo inayofanywa na mwajiri au inayolenga wamiliki wa makampuni fulani kutokana na imani yao au matendo yao ya kisiasa, na mbali zaidi ya kutatua mgao wa rasilimali za kifamilia au udhibiti wa uangalizi wa mtoto.
- Na mwisho, namba na mbinu za ukusanyaji taarifa hazikukusanya vurugu za moja kwa moja, au za wenye watu wenye mahusiano ya karibu, ambazo ni ukatili wa kimaumbile au za kingono majumbani."

## 3.4. Majibu

Kama ilivyo kwa kosa la jinai au kwa kosa ndogo, jawabu bora zaidi ni kinga. Misingi ya kinga ni:

- Kuelewa chanzo na ukubwa wa tatizo,
- Kulichukulia tatizo kwa umakini zaidi,
- Utoaji wa mafunzo kwa maofisa wa polisi kuhusu chanzo na majibu ya tatizo,
- Kuwasiliana na wale walioathirika zaidi (kwa mfano vyama vya watu wenye ulemavu, mgombea mmoja mmoja, vyama vinavyotetea haki za wanawake) na pia wale wote wanaoshiriki moja kwa moja au siyo moja kwa moja katika michakato ya uchaguzi na watu wanaoweza kutoa ushawishi katika maoni ya umma ili kuwahamasisha kuhusu matatizo haya (kwa mfano viongozi wa kisiasa na wanaharakati, viongozi na watawala wa eneo husika, watumishi wa uchaguzi, viongozi wa jadi na wa madhebu ya dini), na Kuandaa mipango ya kuitikia katika matatizo hayo.

Ikiwa kutabainika ishara za mapema za tahadhari kuhusu vurugu inayoweza kutumika, mathalani dhulma za maneno ya kingono, vitisho vya dhulma ya kingono au ripoti za kuwaandikisha vijana wavulana katika makundi ya vurugu, jeshi la polisi pamoja na watu wengine mashuhuri wenye mamlaka wanatakiwa kutoa mara moja majawabu, kwa mfano kusisitiza kwamba ubaguzi, dhulma za kingono na vurugu havitavumiliwa.

Ikiwa kutafanyika tendo la vurugu, maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kujibu haraka iwezekanavyo, na ikiwa kutatendeka kosa lolote la kingono au la kijinsia au ukatili dhidi ya mtoto, shauri hili lipelekwe mara moja kwa maofisa maalum wa Dawati la Jinsia na Watoto.

Mitazamo hii inarudiwa pia katika mifano bora iliyobainishwa na USAID (mwaka 2013) ili kuzuia vurugu za uchaguzi. USAID inapendekeza:

- "Kwanza, kubaini mianya dhaifu ya usalama, ya kisiasa, kijamii, na ya kiuchumi inayochangia kutokea kwa mgogoro wa uchaguzi, ishara za mapema za tahadhari zinaweza kubainika ili kuweka mkazo juu ya mipango ya programu za uingiliaji kati.

- Pili, kuandaa viashiria vya vitisho, programu ya majawabu inaweza kuandikwa ili kutatua mgogoro unaoibuka kutokana na vitisho hivyo.

- Tatu, historia ya mgogoro wa uchaguzi uliopita inaweza kutabiri mgogoro wa uchaguzi wa siku za usoni. Kwa hiyo, sifa bainifu za vitisho vya siku za nyuma zinaweza kuwa na umuhimu mkubwa sana katika chaguzi za siku za usoni.

- Nne, majibu ya programu pana inatakiwa kujumuisha sekta zote", kwa maneno mengine inatakiwa kushirikisha watumishi wa uchaguzi, asazi za kiraia, watekelezaji wa sheria na vyombo vya habari.

Pia USAID inasisitiza kuhusu umuhimu wa utekelezaji wa sheria, ikimaanisha **kusimamia sheria kwa usawa, kwa misingi ya kijinsia**, sheria na sera zingine zinazokataza ubaguzi katika mamlaka zao za kisheria na **kushirikiana na mashirika ya asasi za kiraia**, zikijumuisha mashirika ya kutetea haki za wanawake, mashirika ya usimamizi wa migogoro na vyama ya watu wenye ulemavu vinayoshughulika na maswala haya na kupata uzoefu wao.

Uzoefu wa Afrika Kusini na Kenya uliokusanywa na EISA na USAID pia unaweka mkazo juu

ya faida ya uratibu baina ya wadau mbalimbali na kubadilishana taarifa kuhusu viashirio vya taadhari za mapema na kufanya zoezi la ufahamu wa orodha ya matukio ya vurugu.

## 3.5. Maswali ya kujipima

- Eleza kwa maneno yako, dhana ya jinsia na jinsi gani inahusiana na mahitaji au madhaifu ya watu mbalimbali.
- Jadili jinsi gani jamii unamofanyia kazi imebadilika/haijabadilika na kuwa ya watu tofauti na jinsi gani unaweza kutoa jawabu kwa hali hii katika kazi yako
- Jadili aina mbalimbali ya vurugu au ya ubaguzi unaoweza kutokea katika kampeni za uchaguzi, na jinsi gani jinsia na vipengele vingine vya kijamii vinahusishwa katika hali ya udhaifu.
- Andaa mpango kazi uliokuwa na maelezo mengi unaoonyesha jinsi gani unaweza kuzuia aina za vurugu na ubaguzi wa kijinsia katika medani ya kazi yako. Katika mpango kazi tafadhali bainisha wadau unaotakiwa kushirikiana nao katika kila hatua (wanaweza kuwa makundi ya wanawake, Maaafisa Wakuu wa Vijiji, Mabalozi wa Vijiji, n.k.).

Marejeo:

EISA (mwaka 2009). "Preventing and Managing violent election-related conflicts in Africa - Exploring good practices," http://www.content.eisa.org.za/pdf/symp09cp.pdf

Gabrielle Bardall (mwaka 2011) "Breaking the Mold: Understanding Gender and Electoral Violence," Washington DC: IFES.

USAID (mwaka 2013). "Best Practices In Electoral Security - A Guide For Democracy, Human Rights And Governance Programming." Washington DC:USAID

4

# SURA YA 4

## Polisi Jamii

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya nne.


**4.1. Utangulizi**

**4.2. Tafsiri ya Polisi jamii**

**4.3. Kwa nini Polisi jamii ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia?**

**4.4. Manufaa ya Polisi jamii**

**4.5. Misingi ya Polisi jamii**

**4.6. Viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu zinazotumika katika Polisi jamii**

**4.7. Muhtasari**

**4.8. Maswali kwa ajili ya kujipima**

**Malengo ya mafunzo ya sura ya 4**

**Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-**

- Kutafsiri Polisi jamii, kutaja vipengele vyake muhimu.
- Kuelezea jinsi gani Polisi jamii ni tofauti na shughuli "asilia" za kipolisi
- Toa vipengele vya manufaa vinne pindi Polisi jamii inapotekelezwa.
- Eleza jinsi gani Polisi jamii inaweza kusaidia katika utekelezaji wa sheria na kutatua matatizo.

## 4.1. Utangulizi

Polisi jamii ni mkakati wa kiutendaji unaounga mkono Haki za Binadamu, Utawala Bora na shughuli za kipolisi za kidemokrasia.

Karne ya 21 iliibua changamoto mpya kwa majeshi la polisi duniani kote. Uhalifu na wahalifu wamekuwa na mbinu mpya tofauti na mbinu asilia za "kupambana na uhalifu", ambazo zimendelea kuonekana dhaifu siku hadi siku. Muundo "asilia" wa kipolisi wa kinga ya uhalifu kwa kufanya doria, kutoa majibu ya haraka kwa matukio ya kihalifu na kufanya upelelezi wa kihalifu vyote hivi viliwahi kufanyiwa utafiti na shughuli za kipolisi asilia zilizotajwa hapo juu zilionekana kuwa za muhimu, ila kwa upekee wao hazitoshi kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya uhalifu. Mbali zaidi matumizi ya teknolojia ya kisasa yalionekana kuwa na msaada mkubwa na muhimu, ila hayatoshi pia. Bajeti za jeshi la polisi na rasilimali zake aghalabu ni finyu ili kumudu gharama za mtazamo wa teknolojia ya kisasa ili kupambana dhidi ya uhalifu. Ukweli huu ndiyo hali halisi kwa majeshi ya polisi katika nchi zinazoendelea. Katika nchi nyingi ulimwenguni majeshi ya polisi yaliwahi kugundua kwamba yanahitaji kufanya ubia na jamii ili kupambana kikamilifu dhidi ya uhalifu.

Polisi jamii ni sehemu kamili ya haki za binadamu na inaheshimu haki za binadamu kwa wote bila ubaguzi. Kwa kufanya kazi karibu na jamii ili kuzuia na kutatua matatizo ya kihalifu, jeshi la polisi lina nafasi ya kulinda kwa ufanisi haki za jamii. Kwa upande mwingine jamii ina wasaa mzuri wa kuhakikisha jeshi la polisi linafanya kazi kwa mtindo wa uweledi na wa wazi na kwa namna hiyo wanaheshimu haki za msingi za binadamu pindi wanapotekeleza majukumu yao.

Utekelezaji wa sheria unahusu watu – unahusu kuwatumikia na kuwalinda watu pamoja na haki zao za msingi – unahusu ulinzi wa mtu dhaifu, mtu asiyekuwa na hatia na yule asiyekuwa na msaada dhidi unyama wa wahalifu, kulinda maisha na mali. Kwa sababu hiyo basi utekelezaji wa sheria hauwezi kufanyika katika upekee wake.

Polisi jamii iliaasisiwa kwa ajili ya kutoa majawabu kwa hali halisi ya mabadiliko yanayoyakabili majeshi ya polisi duniani kote. Katika sura hii tutajadili kuhusu polisi jamii kama sehemu ya mtazamo unaozingatia haki za binadamu katika shughuli za kipolisi.

## 4.2. Tafsiri ya Polisi Jamii

Kuna mlolongo wa tafsiri tofauti kuhusu polisi jamii. Maoni kuhusu polisi jamii yanaweza hata kutofautiana nchi baina ya nchi hali hii ikitegemea utamaduni, maoni kuhusu jamii na vipengele tofauti. Kuna vipengele vichache ambavyo vinakubalika na watu wote.

- **Ubia** ni moja ya vipengele muhimu baina ya jeshi la polisi na jamii.
- Lengo kuu la polisi jamii ni **kupambana, kupunguza au kutatua matatizo ya kiuhalifu**.
- Polisi jamii inakuza **mahusiano mazuri** baina ya jeshi la polisi na wanajamii wote na inaimarisha heshima kwa haki za binadamu.

Polisi jamii ni falsafa, mtindo wa usimamizi, na mkakati wa kiuendeshaji unaokuza ubia madhubuti wa jeshi la polisi na jamii ili kushughulikia sababu za uhalifu, na uwoga dhidi ya uhalifu na maswala mengine ya kijamii.

Kwa hiyo Polisi jamii ni falsafa mpya inayokubali kwamba jeshi la polisi linaweza kutatua matatizo yanayohusiana na uhalifu kwa ufanisi na ukamilifu, tatizo la uwoga utokanao na kufanyiwa uhalifu, vurugu za kijamii na za nje, na kudhoofika kwa dhana ya ujirani, ikiwa tu wananchi na jeshi la polisi wataaminiana, kuheshimiana na kushirikiana. Lengo la mwisho ni kusimika mizizi ya ubia madhubuti na ya usawa baina ya jeshi la polisi na umma na kwa kupitia daraja hili la ubia uhalifu na maswala mengine ya kiusalama kwa pamoja yanaweza kuamuliwa na suluhu kutekelezeka.

## 4.3. Kwa nini tunahitaji Polisi Jamii?

Wahalifu ni binadamu wenye akili. Katika enzi hizi za teknolojia ya habari na sayansi iliyoendelea, wahalifu wanajihusisha na shughuli tete zaidi. Waliwahi kuasisi mashirika ambayo ni vigumu kuyaelewa. Hali hii imewahi kutokea kutokana na sababu zifuatazo:

- Wanatumia sheria

  Wahalifu wana mawakili wanaowashauri kuhusu sheria. Wanaelewa kanuni za ushahidi na mzigo wa uthibisho unahitajika kuwashtaki au kuwatia hatiani. Sanjari na hayo wanaunda mashirika ya kisheria na makampuni wanayoyatumia kwa shughuli zao za kiuhalifu.

- Wanaielewa serikali

  Wahalifu wanajua jinsi sheria zinavyotungwa na kutekelezwa. Wanajua jinsi ya kutoa shinikizo katika kura na wanawania madaraka.

- Wanazingatia athari za kijamii

  Wahalifu wanatoa ajira na usalama kwa wafanyakazi wao. Wanashiriki pia katika shughuli za kihisani. Wanawalinda baadhi ya watu na makundi kadha wa kadha. Uaminifu unajengeka kutokana na msaada wanaotoa.

  Kuna sababu nyingi za kutekeleza polisi jamii kama mkakati wa kiutendaji. Hali halisi muhimu inayoiathiri jeshi la polisi na hitaji la utekelezaji wa polisi jamii ni kama ifuatayo:

- ➢ Kuna ongezeko la hitaji la wataalamu zaidi nadani ya jeshi, ambao wako tayari kuleta majawabu na jeshi liko tayari kuwasikiliza wateja
- ➢ Polisi jamii madhubuti inaweza kutoa kwa ufanisi mkubwa ulinzi na usalama kwa wanajamii wote, bila kujali umri wao, jinsia, uwezo au hali yao ya ulemavu, asili yao ya kijamii au uwezo wao wa kiuchumi, bila kujali maoni yao ya kisiasa au asili yao ya kikabila au imani yao ya kidini au bila kujali viashirio vingine vyovyote vile vya kijamii.
- ➢ Polisi jamii inahitaji kwamba, uelewa thabiti wa majibu madhubuti kwa mahitaji maalumu ya watu wanaodharauliwa na dhaifu katika jamii
- ➢ Kuna ongezeko la kichocheo cha kijamii na kiuchumi cha uhalifu
- ➢ Maofisa wa polisi wanatarajia kuwajibika kwa jamii na kuwa wawazi zaidi
- ➢ Kuna matarajio yasiyoweza kuwa kweli upande wa jamii kuhusu ufanisi wa majawabu ya jeshi la polisi asilia
- ➢ Ongezeko la ushahidi la kushindwa kwa mtazamo wa polisi asilia kutoa jawabu la muda mrefu kwa uhalifu na matatizo ya vurugu
- ➢ Uelewa umeoongezeka kwamba bila msaada wa jamii, iwe pesa, watumishi zaidi, teknolojia yenye ubora kiasi gani, mamlaka yenye nguvu zaidi haitaiwezesha jeshi la polisi kushughulikia mzigo mkubwa wa tatizo la uhalifu
- ➢ Maofisa wa jeshi la wanatamani kushiriki katika kuamua na kusimamia mustakabali wao (usimamizi shirikishi)
- ➢ Kuna uthibitisho mkubwa kwamba rasilimali za jeshi la polisi zitakuwa haba siku za baadaye na maofisa wa polisi watalazimika kufanya mambo mengi wakiwa na uwezo mdogo

## 4.4. Manufaa ya Polisi Jamii

Uzoefu unathibitisha ulimwenguni kote katika nchi ambako polisi jamii inatekelezwa, inaonyesha kwamba kuna faida nyingi kama ifuatavyo:

- ➢ Matukio ya uhalifu yalipungua na uwoga wa kufanywa wahanga nao ulipungua
- ➢ Ongezeko la kuridhika la wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na polisi
- ➢ Utaratibu mzuri na mgawanyo wa majukumu baina ya jeshi la polisi na taasisi nyingine za kimahakama na huduma za kijamii dhidi ya uhalifu
- ➢ Fursa zaidi kwa hatua zinazoungwa mkono na jamii
- ➢ Kuungwa mkono kikamilifu na jamii kwa bidii zinazofanywa na jeshi la polisi
- ➢ Jamii kuunga mkono jitihada zinazolenga kuongeza idadi ya maofisa wa jeshi la polisi au kupata rasilimali zaidi za kipolisi
- ➢ Ushirikishwaji madhubuti wa jamii katika kuzuia uhalifu na katika shughuli za utatuzi wa matatizo
- ➢ Utashi wa hali ya juu kwa upande wa wanajamii kuripoti vitendo vya uhalifu,

kutoa taarifa, na kutoa ushirikiano katika upelelezi

- Ubia ulioboreshwa baina ya jeshi la polisi na umma kwa ujumla umesababisha kuwepo na ufahamu wa changamoto na matatizo ya jeshi la polisi inayokabiliana nayo
- Ongezeko la kuridhika kwa maofisa wa jeshi la polisi – hasa maofisa wanaofanya doria

## 4.5. Kanuni za Polisi Jamii

Baadhi ya kanuni za polisi jamii ni kama yafuatayo.

Polisi jamii:

- Inatakiwa kukuza tathmini mpya ya swali linalouliza ni nani anawajibika kuhusu usalama wa umma na inatoa tafsiri mpya ya majukumu na mahusiano baina ya polisi na jamii
- Inatakiwa kukuza uwazi na heshima kwa haki za binadamu, pia usawa kwa wote mbele ya sheria na bila ubaguzi
- Inahitaji umiliki wa pamoja, kuchukua maamuzi na uwajibikaji, pia ahadi ya kudumu toka pande zote mbili yaani jamii na jeshi la polisi
- Inafafanua jukumu la maofisa wa jeshi la polisi wakiwa kama watumishi wanaohakikisha sheria inatekelezwa kwa kuitumikia jamii kuliko kushurutisha
- Inatoa matarajio mapya ya umma kwa jeshi la polisi na (matarajio hayo yanajumuisha ubora wa huduma, kuridhika kwa mteja (jamii), kutoa majawabu kwa matatizo yaliyobainishwa katika jamii, hali nyeti ya kiutamaduni) viwango vya ufanisi wa kazi iliofanyika na jeshi la polisi vinapimwa (kwa mfano, muda wa kujibu na takwimu za watu waliokamatwa/takwimu za uhalifu)
- Ongezeko la uelewa na uaminifu baina ya maofisa wa jeshi la polisi na jamii
- Inawezesha na kuimarisha bidii zinazofanyika katika ngazi ya jamii
- Inahitaji wepesi na uimara ili kutoa majawabu kwa maswala yanayoibuka katika jamii
- Inahitaji kujitoa kwa ajili ya kuendeleza programu na mikakati ya kudumu ya kuzuia uhalifu kabla haujatokea unaosababisha matatizo katika jamii.
- Inahitaji maarifa kuhusu rasilimali zilizopo katika jamii na namna zinavyoweza kupatikana na kuptumika, pia uwezo wa kukuza rasilimali mpya katika jamii.
- Inahitaji ahadi toka ngazi ya juu ya utawala wa jeshi la polisi na mashirika mengine ya serikali za mitaa, pia ahadi ya kudumu ofisa wa polisi binafsi katika ngazi zote za utawala na ya watumishi wengine muhimu.
- Inasogeza huduma za kipolisi karibu na jamii, utendaji na usimamizi, inalegeza "mlolongo wa kutoa amri" asilia na inahimiza utatuaji wa matatizo kwa namna mpya na yenye ubunifu, sanjari na hayo ikitumia maarifa yote ya wajumbe wa mashirika bila kuzingatia safu.
- Inabadili mwelekeo wa kazi za kipolisi za kujibu matukio moja moja na kushughulikia

matatizo yaliyobainishwa na jamii na jeshi la polisi, mkazo ukiwekwa katika mitazamo ya kuleta suluhu kwa matatizo ili kutekeleza sheria asilia – mbinu za utekelezaji wa sheria

- Inahitaji kujitoa kwa ajili ya kuendeleza ujuzi mpya kupitia mafunzo (kwa mfano, utatuzi wa matatizo, mawasiliano katika jamii, usuluhishi, uwezeshaji, usuluhishi wa migogoro, shughuli za kipolisi zinazozingatia masuala nyeti ya kijinsia, kubobea katika masuala ya kiutamaduni)

Polisi jamii inatoa changamoto kwa jeshi la polisi na watumishi wa kiraia kutoa uongozi unaofaa ili kutatua matatizo inayoisibu jamii. Jambo la muhimu sana kwa falsafa ya polisi jamii ni tumaini la mustakabali bora, kwa sababu linatoa mfumo wa kuchunguza na kujibu kwa kuunga mkono mabadiliko ya ongezeko la watu, vurugu za kijamii na kudhoofika kwa maumbile ya nje. Polisi jamii inaweka mkazo juu ya kuimarisha ujirani mwema au kuupa nguvu mpya, ikiwezekana na inaendeleza shughuli za uingiliaji kati zenye ubunifu na pana zaidi dhidi ya milipuko ya kijamii inayodhuru kwa siri mathalani 'ujambazi', biashara ya madawa ya kulevya na vurugu za kijamii mfamo utumiaji uliokithiri wa pombe, dhulma za majumbani na kero za makusudi dhidi ya mtoto.

## 4.6. Sheria za Kimataifa zinazoweza kutumika katika Polisi Jamii

Kuna viwango na miongozo kadha wa kadha vya kimataifa kwa maofisa wa polisi vinavyoweza kutumika katika utekelezaji wa polisi jamii kama ifuatavyo:

- **Kutunga ubia baina ya jeshi la polisi na wanajamii wanaofuata sheria**
  Ni muhimu sana kwa jeshi la polisi kuanzisha ubia na jamii. Jambo hili linaweza kufanyika kwa namna mbalimbali. Kwa mfano nchini Japan jeshi la polisi linafanya kazi katika jamii kwa kutumia mfumo wa "Koban". Katika nchi zingine jamii na jeshi la polisi wanafanya kazi katika majukwa ya polisi jamii ya kinga ya uhalifu. Kipengele muhimu cha mwongozo huu ni kwamba jeshi la polisi na jamii wanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja wakiwa wanaunga mkono harakati za kuzuia kabla na kutatua matatizo ya uhalifu.

- **Kupitisha Sera ya mahuiano ya kijamii na mpango kazi**
  Jeshi la polisi linatakiwa kuandaa na kupitisha sera na mipango kazi inayohusu jinsi ya kutekeleza polisi jamii na jinsi ya kuboresha mahusiano ya polisi jamii.

- **Kuandikisha watumishi toka sekta zote za jamii**
  Jeshi la polisi linatakiwa kuwakilisha sekta zote za jamii. Jambo hili litabuni mawasiliano na mahusiano mazuri na sekta zote za kijamii. Hali hii pia itaimarisha misingi ya usawa na kutokuwa na ubaguzi.

- **Kutoa mafunzo kwa maofisa wa polisi ili kushughulikia hali tofauti**
  Dunia imegeuka kuwa kijiji kidogo. Kutokana na usafiri na mawasiliano ya kisasa watu zaidi na zaidi wanasafiri na kuhamia katika nchi mbalimbali duniani kote. Jamii zinageuka kuwa na watu tofauti. Maofisa wa polisi wanatakiwa kushughulika katika jamii ya watu tofauti na wanatakiwa kupata mafunzo ya kushughulika hali tofauti za kiutamaduni. Yote haya yanajumuisha kushirikiana na watu wa uraia

tofauti, asili tofauti ya kikabila na imani tofauti za kidini bali pia na tambulisho tofauti za kijinsia, na misimamo tofauti ya kisiasa.

➢ **Kuanzisha programu za kuwafikia jamii na usambazaji wa taarifa kwa umma**

Jeshi la polisi linatakiwa kukuza kanuni za polisi jamii kwa kuelimisha umma na kuwahabarisha kuhusu jeshi la polisi na jukumu lake katika jamii. Jambo hili linaweza kufanikishwa kwa kupitia programu za kuafikia jamii na usambazaji taarifa kwa umma.

➢ **Kuwasiliana mara kwa mara na makundi yote katika jamii**
Kunatakiwa kuwa mawasiliano mazuri na madhubuti baina ya jeshi la polisi na jamii. Kwa upande mmoja ni kukuza njia zinazofaa za mawasiliano na makundi katika jamii na kisha kuhakikisha mawasiliano ya kudumu na ya kawaida na jamii. Jambo hili linaweza kufanikiwa kwa mfano kwa kupitia majukwaa ya kuzuia uhalifu. Majina na kazi za majukwaa haya yanaweza kutofautiana baina ya nchi na nchi.

➢ **Kujenga mawasiliano na jamii kupitia shughuli zisizokuwa za utekelezaji sheria**
Jeshi la polisi linatakiwa kushiriki katika shughuli zingine katika jamii, kwa mfano katika matukio ya kijamii au ya burudani. Hali hii itakuza uaminifu baina ya jeshi la polisi na jamii.

➢ **Kuwapanga maofisa wa jeshi la polisi katika doria ya ujirani ya kudumu**

Polisi jamii ni falsafa inayotakiwa kutumika kwa kila ofisa wa jeshi la polisi. Kila ofisa wa jeshi la polisi anatakiwa kukuza na kutumia kanuni za polisi jamii na kuheshimu haki za binadamu. Hata hivyo ni muhimu kwamba baadhi ya maofisa wa jeshi la polisi watashiriki katika doria za ujirani za kudumu.

➢ **Kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika shughuli za kipolisi na katika programu za usalama wa umma za kijamii**
Jukumu la jeshi la polisi ni kulinda na kuitumikia jamii. Ni muhimu kwa sehemu zote za jamii kuwa na kauli kuhusu ulinzi na usalama wao. Kwa hiyo ni muhimu kwa wanajamii kushiriki katika shughuli za kipolisi na kulisaidia jeshi la polisi katika kuendeleza programu za usalama wa umma za kijamii.

➢ **Shirikisha jamii katika kubaini matatizo na mambo yanayowahusu**
Wanajamii wanatakiwa kupewa fursa ya kutoa michango ya mawazo kwa jeshi la polisi kuhusu matatizo na mambo ya kiusalama yanayowasibu katika maeneo wanamoishi. Mambo haya yanajumuisha maswala ya ubaguzi na utengano, ambayo baadhi ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi au sehemu kadha wa kadha katika jamii wanayoweza kukabiliana nayo.

➢ **Tumia mtazamo wa ubunifu wa kutatua matatizo ili kuandaa majibu kwa matatizo mahsusi ya kijamii, yakijumuisha mbinu na mikakati isiyokuwa ya asilia.**
Jeshi la polisi likiwa linakabiliana na hali ya uhalifu inayosadikiwa kuleta utata, linatakiwa kubuni fikra mpya ili kutatua matatizo katika jamii. Daima jeshi

la polisi linatakiwa kujitahidi kukuza mitazamo na mbinu mpya ili kwenda sambamba na mienendo mipya, na maendeleo ya uhalifu.

- **Kuratibu sera, mikakati na shughuli pamoja na mashirika mengine ya kiserikali, na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali**

Kuna mashirika mengi na taasisi zinazoshiriki katika miradi ya kijamii, kuzuia uhalifu na kufanya utafiti wa uhalifu na mada zingine zinazoshabihiana na yaliyotajwa. Jeshi la polisi linatakiwa kushirikiana na mashirika hayo ili kuendeleza sera, mikakati na kazi za kushughulikia uhalifu.

Kuna mikakati mingine, nadharia na miongozo inayoweza kutumika katika polisi jamii. Kila nchi inatakiwa kukuza mikakati yake na shughuli zinazoendana na hali na tamaduni zake.

## 4.7. Muhtasari

Polisi jamii inaweka mkazo juu ya uanzishaji wa ubia baina ya umma na jeshi la polisi. Inaunga mkono haki za binadamu na inasaidia kubuni jeshi la polisi lisiloficha mambo. Ni falsafa, inatambua na kukubali jukumu la jamii katika usimamizi na utoaji huduma za kipolisi. Jamii ni mbia hai katika mchakato wa kuchukua maamuzi. Ubia huu unatoa njia kwa kuzingatia vipaumbele, kutenga rasilimali, na matatizo ya uhalifu yanashughulikiwa.

Kanuni za polisi jamii zinatumika kama mfumo wa kuongoza shughuli na majukumu ya jeshi la polisi na jamii. Kanuni hizi ni sharti la utekelezaji madhubuti wa polisi jamii.

## 4.8. Maswali ya kujipima

- Andika kwa maneno yako kile ulichoelewa kuhusu dhana ya polisi jamii.
- Elezea baadhi ya Kanuni za polisi jamii.
- Taja faida tano za polisi jamii kwa maofisa wa jeshi la polisi.
- Taja faida tano za polisi jamii kwa jamii.
- Fafanua jukumu lako kama ofisa wa polisi kuhusiana na polisi jamii.

- Andika mpango kazi jinsi unaweza, kivitendo, kutekeleza kanuni za polisi jamii katika kazi yako ya kila siku (kwa mfano, jambo hili linaweza kujumuisha matembezi ya kila siku mjini ukiwasalimia watu, kuwa na mazungumzo ya kila mwezi kijijini kuhusu uchaguzi/makundi dhaifu; mikutano miwili kila juma na Wakuu wa Kijiji/ Wakuu wa kata ili kuwashirikisha waweze kuunga mkono chaguzi za amani, kuwa na mahusiano na mashirika yanayotetea haki za wanawake na vyama vya watu wenye ulemavu)

- Jadili jinsi gani ongezeko la hali tofauti katika jamii linasaili jeshi la polisi na maofisa wake kubadili njia ya shughuli za kipolisi.

Marejeo
Police Stranding Order No.25/2011.
Crime Prevention (Police Handbook)
Voter’s Rights and Responsibilities (Police Handbook)

5

# SURA YA 5

## Usuluhishi wa Mgogoro

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya tano.


**5.1.** **Utangulizi**

**5.2.** **Tafsiri ya Mgogoro**

**5.2.1.** **Chimbuko la Mgogoro**

**5.2.2.** **Vipengele vinavyochochea Mgogoro**

**5.3.** **Mgogoro na Vurugu**

**5.4.** **Kushughulikia Mgogoro**

**5.5.** **Mitindo ya Mgogoro**

**5.6.** **Hatua za kudhibiti Mgogoro katika nafsi yako**

**5.7.** **Hatua za kudhibiti Mgogoro na Mtu mwingine**

**5.8.** **Sifa za kitabia za kudhibiti Mgogoro**

**5.9.** **Majadiliano na Upatanishi wa Mgogoro**

**5.10.** **Majukumu ya Watu katika hali za Mgogoro**

**5.11.** **Jukumu la uaminifu na ushirikiano**

**5.12.** **Muhtasari**

**5.13.** **Maswali ya kujipima**

**Malengo ya mafunzo ya sura ya 5**

**Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-**

- ➢ Kueleza maana ya Mgogoro, kutaja vipengele vyake kuu.
- ➢ Kutofautisha Mgogoro na Vurugu
- ➢ Kutaja na kuweka mbinu na mikakati ya kushughulikia Mgogoro.

## 5.1. Utangulizi

Wakati wa uchaguzi jeshi la polisi linatarajiwa kutatua na kudhiti mgogoro. Ikiwa unashughulika na watu, hasa nyakati za kusisimua mathalani katika maandamano ya uchaguzi, mikusanyiko ya watu na mikutano na katika hadhira zingine ambako watu wanaelezea maswala ya hisia kubwa, punde au baadaye unatakiwa kushughulikia mgogoro. Kimsingi mgogoro siyo mbaya. Kwa hakika, chanzo cha mgogoro ni kutofautiana kimawazo. Kwa sababu watu wawili hawawezi kuona dunia kwa mtazamo unaofafana kabisa, kutofautiana kimawazo ni jambo la kawaida kabisa. Kwa kweli, mtu yeyote anayekubaliana nawe wakati wowote ule hakika anakwambia kile ambacho unachotaka kukisikia, na siyo kile anachokiamini.

Sababu ya kwamba mgogoro unapata chapa mbaya ni kutokana na vipengele vya hisia vinavyoambatana nao. Pindi kunapotokea mgogoro, ina maana kwamba kuna kutofautiana baina ya watu wawili au zaidi. Aghalabu mgogoro unafungamana na uhusiano wa maslahi au fikra zilizokuwa na maana kubwa kwa upande mmoja au pande zote mbili zinazoshiriki katika mgogoro.

Mgogoro usiodhibitiwa unaweza kusababisha vurugu na ukaidi. Jambo la muhimu la kudhibiti mgogoro kwa ufasaha ni kujifunza stadi muhimu ili kuwa msimamizi mzuri wa mgogoro.

## 5.2. Maana ya Mgogoro

Kuna maoni na fikra mbalimbali kuhusu mgogoro na zifuatazo ni dhana chache kama mfano: Mgogoro unachukuliwa kama:

- ➢ Ushindani
- ➢ Upinzani
- ➢ Wa kubomoa
- ➢ Hasi
- ➢ Uwezekano wa uhalifu

ilihali uchunguzi wa kina unatoa picha tofauti.

Mgogoro unaweza kutafsiriwa kama uhusiano baina ya pande mbili au zaidi zilizokuwa na mahitaji yasiyooana au yanayokinzana. Mbali zaidi mgogoro pia ni kuwania kiasi cha mamlaka, hadhi na rasilimali ambako mkinzani atafanya kila njia katika uwezo wake ili kuharibu kabisa, kuumiza au kuzima pande nyingine.

Tafsiri yoyote inatakiwa kuwa na vipengele vifuatavyo dhidi taarifa za jumla za yale yaliyotajwa. Kunatakiwa kuwa na pande mbili au zaidi zinazoshiriki. Pande husika zinatakiwa kudhani kuwa zina maoni ya moja kwa moja tofauti. Kunatakiwa kuwa na mchakato fulani ambao ushindani unatokea ili kufanikisha matokeo fulani.

Mgogoro una sura mbili, yaani mgogoro usiojitokeza (wa kulala) na mgogoro hai. Mgogoro usiojitokeza unakuwepo katika uhusiano ambako pande mbili zina maoni kwamba mahitaji yao hayawezi kukamilishwa kwa sababu ya uwepo wa upande mwingine. Mgogoro hai unaanza pindi nguvu inapotumika katika jaribio la kuzima upande mwingine ili kukidhi mahitaji yao. Maofisa wote wa polisi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuelewa tofauti kati ya mgogoro usiojitokeza na ule uliohai na kuhakikisha uzuiaji thabiti wa uhalifu kwa kushughulikia mgogoro usiojitokeza. Na hapa ndipo mtumishi aliye na maarifa anafahamu na kuelewa mawazo ya jamii yake yalivyo na kwa maana hiyo anatakiwa kuwa na uwezo wa kuzuia mgogoro hai kwa kupitia majadiliano na usuluhishi wa mapema.

## 5.2. Kuelewa Mgogoro

Ili maofisa wa polisi waweze kuelewa mgogoro wanatakiwa kufahamu vyanzo vya mgogoro na vipengele vinavyoweza kuchochea mgogoro.

### 5.2.1 Chimbuko (Vyanzo) la Mgogoro:

Chanzo cha mgogoro kinaonekana bayana katika ngazi mbalimbali.

➢ **Kweli**
Watu huwa wanatofautiana kuhusu kweli mbali mbali katika hali fulani. Kwa mfano kuna kweli tofauti kuhusu tabia ya uvutaji au kutovuta sigara.

➢ **Michakato**
Watu huwa wanatofautiana katika mawazo yao kuhusu mchakato unaotakiwa kufuatwa katika kukamilisha zoezi fulani. Kwa mfano marafiki wawili wanatofautiana kuhusu ratiba yao ya siku. Wote wawili wanafahamu kwamba wanatakiwa kufanya manunuzi ya vitu na kazi ya bustani ila wanatofautiana kuhusu shughuli ipi itangulie. Je, wanatakiwa kwanza kwenda kununua vitu au kufanya kazi ya bustani.

➢ **Malengo/Azma**
Watu huwa wanatofautiana kuhusu malengo katika maisha. Mfano wa kutofautiana katika malengo ni ule wa mwajiri na mwajiriwa kabla ya ajira kuhusu mishahara itakayolipwa katika kukamilisha kazi.

➢ **Tunu**
Watu huwa wanatofautiana kuhusu tunu katika maisha. Mfano wa tunu tofauti ni hali tofauti baina ya makundi ya kisiasa na makundi ya kidini.

### 5.2.2. Vipengele vinavyochochea Mgogoro

Maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kufahamu kwamba kuna vyanzo vya mgogoro. Pia kuna vipengele kadha wa kadha, vinavyochochea mgogoro. Vipengele hivyo vinajumuisha yafuatayo:

➢ **Kuvunjika kwa mawasiliano**

Kwa sababu mawasiliano ni mchakato tete unazongwa na vizuizi vingi, mara nyingi vizuizi hivi vinasababisha mgogoro. Ni rahisi kumwelewa vibaya mtu mwingine au kundi la watu ikiwa mawasiliano yatazuiliwa kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo mawasiliano yanayoeleweka yanaweza kuzuia mgogoro katika mazingira kadha wa kadha.

➢ **Wajumbe tofauti kuwa na hamu ya kupata kitu bora**

Kukiwa na matarajio makubwa kwa mjumbe mmoja katika mawasiliano ndivyo kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kutokea mgogoro. Ikiwa pia matarajio ya jamii ni makubwa kuna uwezekano wa kutokea hitilafu katika matarajio ya kisiasa ya jamii.

➢ **Uelewa**

Jinsi hali ya kutoelewana vizuri itakapoongezeka kati ya makundi ndivyo hali hii itakuza uchochezi mkubwa wa mgogoro. Uelewa wa kundi moja unaweza kuharibu sifa ya kundi lingine. Mathalani uelewa unopokuwa mdogo juu ya jambo fulani, mifano ya kawaida na mingi inawezakutokea baina ya jinsi mbili yaani ke na me. Hivyo hivyo, wakati wa kampeni za uchaguzi, uelewa na mitindo hasi isiyobadilika inayofuatwa na takriban kila mtu na kwa makusudi au la inaweza kuhamasishwa bila ridhaa, iwe dhidi ya watu au jamii. Chuki hizi zinaweza kuwalenga watu binafsi au kikundi fulani ikizingatia umri wao, jinsi, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, asili yao ya kijamii au uwezo wao kiuchumi, itikadi yao ya kisiasa au asili yao ya kikabila au imani ya dini zao au viashiria vingine vyovyote vile vya utambulisho wa kijamii.

➢ **Badiliko la Mkakati**

Pindi mgogoro unapoongezeka –makundi yanayohusika kwa kawaida yanaachana na mikakati chanya ya utatuzi wa matatizo, majadiliano na ya maridhiano na kuelekea kwenye vitisho na udanganyifu. Ikiwa makundi hayo yatafanya kazi kwa hisia kali (hasira au kuvunjika moyo) mikakati ya kushambuliana itaongezeka. Sanjari na hayo jeshi la polisi linatakiwa kuhakikisha kwamba jamii inahimizwa kushiriki kwa kutumia mbinu zinazojenga za utatuzi wa matatizo na uingiliaji kati wa hali iliyodorora. Ili kufanikiwa ni muhimu kwa wajumbe kujua na kuelewa jamii ya eneo husika. Ujuzi huu unaweza tu kuhakikishiwa kupitia mawasiliano yasiyokatika na jamii.

➢ **Mabadiliko ya kundi na jumuiya**

Katika vita dhidi ya ujambazi daima kuna kundi kubwa linaloshiriki. Watu wanaungana na kusahau tofauti zao binafsi na kundi linatarajia wajumbe wake kuunda umoja. Mtindo wa uongozi unabadilika kutoka mfumo wa kidemokrasia na kuwa wa kiimla na kundi linaweka mkazo hasa juu ya kazi inayotakiwa kufanyika. Chanzo cha mgogoro kinakuwa lengo la pamoja na vita vinapamba moto. Katika jamii ambamo kuna vita dhidi ya ujambazi, kuna mwelekeo wa kawaida kuona jamii inaegemea upande mmoja kupinga vitendo vya ujambazi. Kwa namna hii jamii inagawanyika na hali ya kutopendelea upande wowote inatoweka. Maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa mapema kuwa na uwezo wa kubaini ishara hizi ili kuzuia mgogoro mkubwa zaidi. Kwa hivyo basi maofisa wa polisi wanaweza kutenda kama wasuluhishi kati ya makundi husika au hata kuongea na kundi maalumu ili kuzuia mgogoro usishike kasi zaidi.

## 5.3. Mgogoro na Vurugu

Mgogoro kama mgogoro siyo lazima uwe hasi, ila ikiwa hautashughulikiwa unaweza kusababisha vurugu ya umma au hata vurugu zilizoratibiwa. Kwa hiyo ni muhimu kwamba (maofisa wa jeshi

la polisi) kuelewa vipengele hivyo vinavyoweza kubadili mgogoro na kuwa vurugu. Vurugu ni tabia inayolenga kuumiza watu na kuleta madhara au kuharibu mali. Kwa hiyo ni vema ikiwa mtu atakuwa na uwezo wa kuelewa mapema ishara za mgogoro unaoweza kugeuka kuwa vurugu na kutenda ipasavyo, vurugu inaweza kuzuilika. Baadhi ya ishara hizo ni:

- Ongezeko la manug'uniko na tishio.
- Kutokuwepo kwa majukwaa ya usuluhishi, taratibu na msuluhishi wa mgogoro anayeweza kuaminika.
- Kukubali itikadi ya vurugu ("vurugu inaweza kutumika ").
- Udhibiti hafifu wa jamii (jamii haizuii mgogoro wenye kuleta madhara) Kudorola kwa kanuni za kikundi.
- Kutokuwepo kwa suluhu mbadala za kueleweka katika kutatua matatizo.
- Mtazamo kwamba kunaweza kusitendeke haki.
- Mtazamo kwamba uwajibikaji binafsi haupo.
- Katika mtazamo wa upande mmoja, "Upande mwingine" unatenda kikatili.
- Historia ya vitendo vya kutumia nguvu

Kwa kubaini dalili hizi ofisa wa jeshi la polisi anaweza kuzuia uhalifu mkubwa na kuweka wavu wa kinga. Ofisa wa jeshi la polisi asiyekuwa na maarifa inawezekana akachangia kwa manung'uniko na kukuza vurugu.

## 5.4. Kushughulikia mMogoro

Maofisa wa jeshi la polisi ni, kama matokeo ya asili ya kazi yao, wanakinzana na mtu anayevunja sheria. Ofisa wa polisi hawezi kudiriki kuweka mkazo juu ya tabia ya mtu aliyevunja sheria kwa namna hiyo atakuwa anashughulika mgogoro unaoweza kujitokeza. Ni muhimu pia kubaini mgogoro usiojitokeza, na kuchukua hatua za kinga na kwa kufanya hivyo kutapunguza uwezekano wa mgogoro unaoonekana bayana.

Kinadharia kuna njia mbalimbali (mitindo) za kudhibiti mgogoro. Kila mtu ana tabia na silika yake kwa hiyo atapendelea mtindo wake maalumu. Ni muhimu kujua na kuelewa mtindo anaoupendelea.

## 5.5. Mitindo ya Mgogoro

Watu huwa wanatumia njia tofauti katika kudhibiti mgogoro katika hali fulani. Hakuna njia inayofaa zaidi ili kushughulikia mgogoro. Inategemea na hali iliyopo. Yafuatayo ni njia kuu walizowahi kutumia watu katika kushughulikia mgogoro.

- Uepuke. Jidai kwamba mgogoro haupo au uupuuze. Tumia mbinu hii ikiwa mgogoro ni rahisi na hakuna haja ya kujibishana naye. Kwa kawaida mtazamo huu unaelekea kuzidisha mgogoro kadiri muda unavyokwenda.

- Uuzoee. Uutoe kwa wengine, wakati mwingine kwa kuhatarisha nafsi yako. Tumia njia hii kwa nadra sana na siyo mara kwa mara, kwa mfano, katika hali fulani ukiwa unajua kwamba una njia nyingine muhimu katika siku za usoni. Kwa kawaida njia hii inaelekea kuharibu zaidi pindi muda inavyokwenda, inasababisha mgogoro ndani ya nafsi yako.

- ➢ Kushindana. Tafuta nji ya kujiokoa, badala ya kufafanua na kushughulikia tatizo. Washindani huwa wanawapenda watu wanaokubali kuzoea hali fulani. Tumia njia hii ikiwa una imani kubwa kuhusu msimamo wako.

- ➢ Muafaka. Kutoa na kupokea kwa pande zote mbili. Tumia mbinu hii pindi lengo ni kufanya tatizo lipite na kusonga mbele.

- ➢ Ushirikiano. Unasisitiza kufanya kazi kwa pamoja. Tumia mbinu hii ikiwa lengo ni kumudu mahitaji ya sasa iwezekanavyo kwa kutumia rasilimali za pande zote mbili. Njia hii kuna wakati inaibua mahitaji ya pande zote mbili. Tumia mbinu hii pindi lengo likiwa ni kukuza na ushirikishaji wa pande zote mbili.

Mitindo ya migogoro inaweza pia kufafanuliwa kwa kutumia tabia ya wanyama ili kuelewa zaidi. Ufafanuzi unaofuata utahakikisha na kukuwezesha kubaini na kutumia mitindo tofauti ya migogoro.

**Kobe (kuondoka**). Huwa kobe wanarudi ndani ya magamba yao ili kuepuka migogoro. Wanakubali kuachia malengo na mahusiano yao binafsi. Wanabaki mbali na matatizo ambako mgogoro unaendelea kuchemka mbali na watu. Kobe wanaamini kwamba haina haja ya kujaribu kutatua migogoro. Wanajihisi hawana msaada wowote wa kutoa. Wanaamini ni rahisi kurudi nyuma (kimaumbile na kiakili) mbali na mgogoro kuliko kukabiliana nao.

**Papa (kulazimisha).** Huwa papa wanajaribu kushinda kwa nguvu wapinzani wao kwa kuwalazimisha wakubali suluhu zao katika mgogoro. Malengo yao ni ya muhimu, na hivyo kwao mahusiano hayana umuhimu sana. Wanapania kufanikisha malengo yao kwa gharama yoyote ile. Hawajali mahitaji ya watu wengine. Hawajali ikiwa wengine wanapenda au hawapendi suluhu zao. Papa wanadhani kwamba migogoro inadhibitiwa kwa mtu mmoja kuwa mshindi dhidi ya yule anayeshindwa. Wanataka kuwa washindi. Kushinda kunawapa papa hisia ya ufahari na kufanikiwa. Kushindwa kunawapa hisia ya udhaifu,upungufu na kuanguka kabisa. Wanajaribu kushinda kwa kushambulia, kwa nguvu, kwa kuzonga na kwa kuwatishia wengine.

**Paka (utulivu).** Kwa paka mahusiano yana umuhimu wa juu ilihali malengo yao yana umuhimu mdogo. Paka huwa wanatamani kukubaliwa na kupendwa na watu wengine. Wanadhani kwamba mgogoro unatakiwa kuepukwa kwa manufaa ya upatanifu na kwamba watu hawawezi kujadili migogoro bila kudhuru mahusiano. Wanahofia kwamba ikiwa mgogoro utaendelea, kuna mtu atakayeumia, na hali hiyo inaharibu mahusiano. Wanaachilia mbali malengo yao ili kuokoa mahusiano. Paka huwa wanasema, “Nitaachia malengo yangu na kukuachia kile unachokitaka, ili wewe uweze kunipenda.” Paka huwa wanajaribu kuleta hali tulivu dhidi ya mgogoro wakihofia kudhuru mahusiano.

**Sungura (muafaka).** Sungura huwa kwa wastani wanajali malengo na mahusiano yao na watu wengine. Sungura huwa wanapania muafaka: wanatoa sehemu ya malengo yao na kumshawishi mtu mwingine katika mgogoro naye pia atoe sehemu ya malengo yake. Wanatafuta suluhu ya mgogoro ambapo pande zote mbili wanaambulia chochote – msimamo wa kati baina ya misimamo miwili tofauti kabisa. Wako tayari kusamehe sehemu ya malengo na mahusiano yao ili kupata muafaka kwa ajili ya faida ya pande zote mbili.

**Bundi (kukabiliana).** Bundi wanathamini sana malengo na mahusiano yao. Wanachukulia

migogoro kama matatizo yanayotakiwa kusuluhishwa na wanatafuta suluhu inayofanikisha malengo yao na malengo ya mtu mwingine. Bundi wanachukulia migogoro kama njia ya kuboresha mahusiano yao kwa kupunguza hisia kali baina ya watu. Wanajaribu kuanzisha mijadala inayobaini mgogoro kama tatizo. Kwa kutafuta suluhu zinazowaridhisha wao na watu wengine, bundi huwa wanaendeleza mahusiano. Bundi huwa hawaridhiki hadi pale suluhu itakapopatikana ili kufanikisha malengo yao na yale ya mtu mwingine. Na hawaridhiki hadi pale hisia kali (za moyoni) na dhana hasi zimetatuliwa kikamilifu.

*Tafiti ikiwa mnyama mmoja ni mzuri kuliko mwingine, au ikiwa kuna mnyama ambaye sote tunatakiwa kujaribu kumuiga. Licha ya kuwa makundi yanaweza kubaini mbweha au bundi kama mnyama anayefaa, hakikisha kwamba tunatakiwa kuwa wepesi vya kutosha ili tuweze kumpenda kila mnyama. Kwani kila mnyama ana thamani yake ya kipekee katika mazingira tofauti.*

Utatuzi wa tatizo na miafaka iliyojadiliwa kwa umahiri ndiyo njia inayoweza kuondoa vyanzo halisi vya mgogoro. Ni mbinu pekee za usuluhishi inayosaidia kuboresha kwa muda mrefu hali ya mambo. Njia zingine ni hatua za muda mfupi tu na watu waliotekwa nyara katika njia hizo wanaepuka mkakati thabiti na wanalikimbia tatizo. wakati mwingine muda hautoshi kwa ajili ya majadiliano na kulazimisha na mbinu ya utulivu itatumika ili kupata ushirikiano.

## 5.6. Hatua za kudhibiti Mgogoro katika Nafsi yako

## (USHAURI KWA WAKUFUNZI: INAPENDEKEZWA KWAMBA SEHEMU YA 4.6-4.8 IJUMUISHE MAZOEZI YA KIVITENDO YA MAIGIZO KWA WASHIRIKI)

"*Aghalabu ni katika kujaribu ndiko tunapata tulizo, siyo kupata suluhu bora*". Katika hali hii hatua zifuatazo zitakusaidia.

Hatua ya 1: Taja mgogoro, au baini tatizo, pamoja na kile unachokitaka ambacho hujakipata.
Zingatia:
Andika fikra zako ili ufikie hitimisho.
Ongea na mtu, pamoja na kuwauliza kukusaidia kutoa muhtasari wa mgogoro katika sentensi 5 na upungufu.

Hatua ya 2: linganisha kwa kujadili tatizo na rafiki yako au kwa kuandika tatizo. Zingatia:
Je, tatizo lina umuhimu gani?
Je, tatizo linaonekana kuwa mbaya zaidi kwa sababu umechoka, una hasira juu ya kitu kingine, n.k?
Una jukumu gani katika tatizo hili?

Hatua ya 3: chukua angalau kitu kimoja unachoweza kufanya kuhusu mgogoro.
Baini angalau mitiririko mitatu ya hatua.
Kwa kila mtiririko, andika angalau mitatu unayoiunga mkono na mitatu usiyoiunga mkono.
Chagua hatua – ikiwa hakuna mtiririko wa hatua unaoeleweka, chukua hatua mbadala ambao hautakuumiza, hautakuumiza sana wewe na watu wengine.
kwa muhtasari jadili mtiririko wa hatua na rafiki.

Hatua ya 4: Kisha fanya jambo lolote.

Subiri angalau siku moja kabla ya kufanya jambo lolote kuhusu mgogoro. Hali hii inakupa fursa ya kipindi cha kutulia.
Kisha chukua hatua.
Zingatia akili, tarehe utakapochukua tena hatua ikiwa hujaona maboresho bayana.

## 5.7. Hatua ya kudhibiti Mgogoro na Mtu mwingine

Hatua ya 1: Kujua kile ambacho hupendi kuhusu nafsi yako mwenyewe, mapema katika kazi yako. Aghalabu kuna vitu ambavyo hatutaki kuviona kwa wengine ambavyo hatutaki kuona ndani ya nafsi zetu.
Andika tabia 5 zinazokughadhibisha unazoziona kwa wengine.
Kumbuka ya kwamba hizi ndizo tabia zako "zenye kuelekea kuleta mabishano".

Hatua ya 2: Kudhibiti nafsi yako. Ikiwa wewe na/au mtu mwingine mna hasira kali, ni vema kudhibiti nafsi na kutulia kwa kuongea na mtu mwingine kama vile mtu yule hana hasira – hali hii inaweza kuwa jambo la kufaa!
Epuka kutumia neno "wewe" – hatua hii itaepusha lawama. Tingisha kichwa chako kwa ishara ya kuwadhihirishia watu kwamba unawasikiliza.
Waangalie machoni.

Hatua ya 3: hamishia majadiliano katika eneo la faragha, ikiwezekana.

Hatua ya 4: Mpe mtu mwingine muda wa kutoa mawazo yake bila woga.
usiwakatishe kauli au kuwahukumu kwa kile wanachokisema.
Hakikisha kwamba munasikilizana kwa ufasaha. Pindi wanapomaliza kuzungumza:}
mwombe mtu mwingine akuruhusu kupangilia maneno upya (bila kukatizwa) kile unachosikia toka kwao ili kuhakikisha kwamba unawasikiliza.
ili kuwaelewa zaidi, uliza maswali yasiyohitaji kukatiwa kauli. Epukana na maswali ya "kwa nini" – maswali kama haya yanawafanya watu kujitetea.
Rudia hatua hapo juu, mara hii ili waweze kuchunguza kwamba wanakusikiliza.
Unapowasilisha msimamo wako
Tumia neno "Mimi", siyo "wewe".
Ikiwezekana tumia wakati wa sasa.
Taja hisia zako.

Hatua ya 7: Tambua mahali ambako hamkubaliani na pale mnapokubaliana.

Hatua ya 8: Shughulikia tatizo, na siyo mtu. Pindi unapoamini kwamba unawaelewa:
Uliza "Ni kitu gani tunaweza kufanya ili kutatua tatizo?" Wataelekea kutoa tena lawama.
Kisha uliza tena swali hilo hilo. Weka pia mkazo juu ya vitendo wanavyoweza kufanya.

Hatua ya 9: Ikiwezekana, baini angalau hatua moja inayoweza kufanyika na mmoja wenu au nyote wawili.
Uliza yule mtu mwingine ikiwa ataunga mkono hatua.
Ikiwa hawataunga mkono, halafu omba "kipindi fulani cha kutulia ".

Hatua ya 10: Mshukuru mtu yule kwa kufanya kazi nawe.

Hatua ya 11: Ikiwa hali inabaki kuwa ya mgogoro, halafu:
Hitimisha ikiwa tabia ya yule mtu inahasimiana na sera na taratibu za mahali pa kazi na ikiwa ndivyo hivyo, wasilisha tatizo hilo kwa msimamizi wako.
Zingatia ikiwa unakubali au haukubali.
Zingatia kumtafuta mtu wa tatu kwa ajili ya usuluhishi.

## 5.8. Ni tabia zipi zinasaidia kudhibiti mgogoro?

- **Tumia kauli za "mimi".** Mwache mtu mwingine ajue kile **unachokihisi** pindi mgogoro unapotokea. Mruhusu mtu mwingine ajue jinsi gani **unavyojibu** pindi mgogoro unapotokea. Mwache mtu yule ajue ni zipi haki zako unadhani zilipuuzwa katika mgogoro.

- **Jiamini, na siyo mwenye tabia ya kuanzisha ugomvi.** Zungumzia hisia zako na jinsi unavyojibu. Hakikisha kauli zako zinaweka mkazo jinsi unavyoonyesha tabia yako, fikra zako, na hisia zako kuliko jinsi mtu mwingine anavyojibu.

- **Ongea kwa utulivu, bila taharuki na kwa umakini.** Kwa namna hiyo utasikilizwa, na utaweza kudhibiti nafsi yako kikamilifu. La sivyo unaweza kumfanya mtu mwingine kuwa na msimamo wa kujitetea.

- **Epuka lawama.** Hali hii itahakikisha mtiririko wa mawasiliano kuendelea. Inakuza uelewano na uwezo wa kutambua hisia za mtu mwingine. Inatoa utambuzi wa kutambua kwamba ili mgogoro uwepo inatakiwa kuwe na angalau pande mbili kinzani zilizoathirika na mgogoro.

- **Buni mazingira ya uponyaji.** Katika jaribio la kutibu vidonda vinavyotokana na mgogoro, pande zote zinatakiwa kuhisi kwamba zinasikilizwa na kueleweka; na kwamba haki zao zinaheshimika. Watu wana hamu ya kuona mambo yanarekebishwa na utashi wa kuona mchakato wa kutatua matatizo unafana. Wanatakiwa kuhisi wanahitajika na kuangaliwa na pande zote zinazoshiriki.

- **Kuwa na nia ya kusamehe.** Msamaha ni nyenzo yenye nguvu kubwa katika uponyaji. Unatoa fursa kwa ustawi binafsi kwa kusamehe wengine kwa yote walioweza kukuumiza moyoni na maumivu waliyowahi kukusababishia. Wakati wote, ni njia pekee ya kutatua mgogoro.

- **Kuwa na nia ya kusahau.** Mara ``unaposuluhisha" mgogoro na kuhisi kwamba ulisikilizwa, watu walikujali na kukuelewa, ni vema "ukaachilia" mbali mgogoro. Uuweke pembeni. Uuondoe katika fikra zako. Uusahau. Usiuibue tena siku za baadaye kama vile haujawahi kusuluhishwa. Ikiwa utaandika maazimio ya mgogoro, uliandika ushahidi kwamba umekwisha na unatakiwa kusahaulika.

- **Kuwa mkweli.** Katika usuluhishi wa mgogoro ni jambo la lazima kuwa mkweli kwa nafsi yako na kwa wengine kuhusu hisia zako, jinsi unavyojibu dhidi ya mgogoro na kwa maazimio ya mgogoro. Ikiwa unahisi kwa mtindo ambao unadhani unatakiwa kuwa au kwa namna ambayo watu wengine wanataka usiwe kama wewe``jinsi unavyotakiwa kuwa mwenyewe," inamaana maazimio ya mgogoro ni batili. Kwa

uhakika mgogoro utaibuka tena. Hupati chochote kwa kudanganya katika usimamizi wa mgogoro. Unapoteza muda na nguvu zako na unaishia kujihisi umeanguka kabisa au kujisuta kuliko kuwa na ustawi.

- **Weka mkazo juu ya hisia kuliko maudhui.** Usikilizaji unaofaa na kujibu ni vipengele muhimu katika usuluhishi wenye tija katika mgogoro. Kusikiliza hisia na jazba za mtu mwingine na kufanya tafakari kwa kuelewa na kuguswa na jambo lililomsibu mwenzako. Jambo hili linaandaa mazingira ya kuonekana watu wanakujali na kukusikiliza. Inapunguza hali ya kujitetea. Hali hii inaweka mkazo juu ya mchakato unaoendelea kuliko kuzingatia matatizo, na kusukuma pande zote husika kutambua halisi ya upekee na ubinadamu wao. Kuweka mkazo juu ya hisia unafafanua matatizo, na kuondoa vipengele visiyvokuwa na umuhimu.

- **Onyesha heshima kwa nafsi yako na kwa watu wengine.** Utavuna mengi kwa kutatua mgogoro kwa kuonyesha heshima (*asali*), badala ya kuonyesha utovu wa heshima (*siki*), kwa mfano, kulipiza kisasi, kutoa vitisho, kulalamika, kulaumu, kudhalilisha, kugoma, kupuuza. Ikiwa wewe ndiye uliyekosewa heshima, ondoka haraka iwezekanavyo. Pindi wengine watakapotulia, labda mjadala unaweza ukaendelea kwa namna ya heshima. Ikiwa utataharuki na kutokuwa na heshima, sitisha mjadala haraka iwezekanavyo kwa kuondoka au kwa kukaa kimya. Kuhakikisha mazingira ya heshima ni muhimu sana katika utatuzi wa mgogoro. Jambo hili linajumuisha heshima kwa watu wote bila kujali umri wao, jinsi, uwezo wao au hali yao ya ulemavu, asili yao ya kijamii au uwezo wao wa kiuchumi, itikadi zao za kisiasa na imani zao za kidini au viashirio vingine vya utambulisho wa kijamii na kutowabagua kutokana na sifa zilizotajwa. Pia ni muhimu kutoonyesha chuki au mitindo isiyobadilika
Kwa wajumbe wa makundi mbalimbali kuhusu mahitaji na madhaifu yao maalimu.

- **Uwe na nia ya kuomba msamaha au kukubali kosa.** Ni muhimu kukubali makosa yako na kuomba msamaha kutokana na tabia fulani kabla ya kukwama kwa usuluhishi wa mgogoro. Jambo hili linahitaji ujasiri, tabia ya kipekee, na ushupavu ili kukubali kosa: kutotoa hukumu; hatua isiyostahili; tabia ya kutokuwa na heshima, au kutokujali au kuelewa. Mahusiano imara yanaweza kutokea pindi utashi kama huo wa kukubali kosa unadhihirishwa.

- **Kuwa tayari kufikia muafaka.** Ikiwa unashikilia msimamo wako kwamba ndio unatakiwa kuzingatiwa, unawafungia njia watu wengine. Ili kufanikisha katika utatuzi wa mgogoro, pande zote zinatakiwa kuhisi kwamba walishinda katika maazimio. Ili kusuluhisha mgogoro ambako pande kinzani zinatofautiana kabisa kuhusu jambo fulani, kuna umuhimu wa kuwa na msimamo wa kati ikiwa pande zote zinatakiwa kuwa katika mkao wa "ushindi". Ni kwa kupitia tu muafaka kila upande unaweza kuwa mshindi katika usuluhishi wa mgogoro. Bila muafaka, nyote mtakuwa mnajitoa na kushindwa, au mmoja anashinda na mwingine kushindwa. Kimsingi pande zote mbili zinatakiwa kuhisi zimeshinda.

## 5.9. Upatanishi na Usuluhishi wa Mgogoro

Usuluhishi unatakiwa wakati watu wawili au zaidi wanawasiliana na angalau mmoja wao ana

lengo maalumu akilini. Maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kujifunza stadi za upatanishi, kwa sababu maofisa wote wa polisi wanatumia muda wao mwingi katika upatanishi na usuluhishi baina ya pande zenye mgogoro. Mfano ni pale mume na mke waliooana wanapokuwa na matatizo ya ndoa na mwanamke anatoa malalamiko kwa jeshi la polisi kwamba mume wake anamtishia kumuumiza. Ofisa wa jeshi la polisi anatarajia kutoa msaada na kushughulikia mgogoro.

Ujuzi wa upatanishi, kama ujuzi mwingine wowote ule muhimu wa mawasiliano, unahitajika kuendelezwa kupitia mafunzo yenye juhudi na ya kivitendo. Ni jambo la muhimu kwa kila mpatanishi kuwa msikivu na mjuzi wa mawasiliano.

## 5.10. Majukumu walionayo Wasuluhishi wa Mgogoro

Kuanzia hatua ya kabla ya upatanishi na hatua za baada ya upatanishi, watu wanaoshiriki katika mchakato wa uingiliaji kati wana majukumu kadha wa kadha. Wawakilishi wa maeneo husika, wa kikanda na kimataifa wa mashirika ya kiserikali na yasiyokuwa ya kiserikali wanajikuta wakisaidia katika juhudi za kuleta amani kupitia njia mbalimbali,zikiwemo (iliyo rekebishwa toka kwa Mitchell, mwaka 1993):

- **Mchunguzi:** Anapeleka ujumbe baina ya pande husika na kuwahakikishia kuhusu nafasi ya upatanishi na anabainisha maeneo ya maelewano.

- **Mwiitishaji:** anaanzisha mchakato wa usuhulishi kwa kuzitia moyo pande husika kushiriki na kushughulika jinsi ya kuondoa vikwazo vinavyozuia shughuli za kuleta amani.

- **Mchambuzi:** Anafanya uchambuzi wa kisiasa, kijamii au kiuchumi wa mgogoro ili kusaidia waingiliaji kati wengine kutambua sababu za mgogoro na mtiririko wa hatua.

- **Mbunifu:** Anasaidia pande husika na waingiliaji kati wengine kubuni mchakato wa usuluhishi utakaoshughulikia kwa ukamilifu na ufasaha matatizo ya mgogoro.

- **Bingwa wa mawasiliano:** Anachukua jukumu la kuwa daraja la mawasiliano baina ya pande husika katika mchakato na wale walioko nje ya mchakato, mathalan vyombo vya habari, umma kwa ujumla na jamii ya kimataifa.

- **Mtenganishi:** Anatafuta njia ya kuwashawishi wadau wa nje waonashiriki katika mgogoro kujiondoa katika mgogoro kwa heshima na anajaribu kuwashirikisha wadau wengine wa nje ambao watashirikishwa pasipo na upendeleo kiasi katika kupitisha mchakato au kuzitia moyo pande zinazohusika katika mgogoro kushiriki katika usuluhishi.

- **Muunganishi:** Anasadia katika majadiliano kati ya pande husika kurekebisha migawanyiko yao na kuwasaidia kubuni maelewano ya pamoja kuhusu mgogoro, malengo na azma zao.

- **Stadi:** Anaziwezesha pande husika na ujuzi unaohitajika katika upatanishi, anawasilisha maslahi, anachanganua matukio na kutafiti vipengele vya mgogoro.

- **Mwalimu:** anatoa maoni ya kitaaluma au taarifa za kiufundi kwa pande husika kuhusu vipengele vya matatizo ya mgogoro.

- **Anayeona mbele:** anasaidia pande husika kufikiria kuhusu mgogoro na suluhu zinazowezekana kupitia njia mpya kwa kutumia michakato bunifu za kutoa chaguo au kuingiza taarifa zinazofaa.

- **Anayetathmini:** anasaidia pande husika kutathmini suluhu zinazowezekana na athari zake katika maazimio ya mgogoro.

- **Mdhamini:** anahakikisha pande husika haziingii gharama zisizokubalika iwe kupitia ushirikishwaji katika mchakato au ikiwa mchakato utavunjika.
- **Anaye halalisha:** anahimiza pande husika kukubali mchakato kwa kutoa idhini yao ya uadilifu, ya kisiasa na ya kifedha.

- **Mwezeshaji:** Anasaidia pande husika kufanya mawasiliano baina yao kwa kubuni mchakato salama kwa ajili ya majadiliano, kwa kuunda au kuzuia masuala na kurahisisha uelewa wa pande husika kuhusu mgogoro na kuimarisha jukwaa la kusikiliza kwa ufasaha na utatuzi wa matatizo.

- **Mboreshaji:** Analeta rasilimali ili kupanua chaguo za upatanisho au anatoa zawadi kwa tendo la kushiriki katika mchakato.

- **Mtekelezaji:** anafuatilia maafikiano na kanuni za tabia njema ili kasi ya mchakato iweze kuendelezwa.

- **Msuluhishi:** anaandaa pande husika kusanifu shughuli za mahusiano ya muda mrefu zilizobuniwa ili kupunguza vielelezo vya tabia hasi, mitindo ya kubomoa isiyobadilika inayofuatwa na takriban kila mtu na mawasiliano yasiyoeleweka.

Orodha hii ndefu ya majumu inaonyesha ugumu wa kuanzisha na kuendeleza michakato ya amani. Mlolongo wa ujuzi, maarifa, rasilimali na uwezo unaohitajika kuwa madhubuti katika majukkumu haya yasiyoelekea kupatikana katika mtu mmoja au katika shirika moja linaloingilia kati. Iwe kwa ubunifu au kwa kujiri, pindi kunapokuwepo idadi ya wadau wanaposhiriki katika vipengele mbalimbali vya kazi ya uingiliaji kati, kuna changamoto kadha wa kadha zinazokuatana.

Kwa wale wanaoshiriki katika juhudi za usuluhishi, kuna mambo matatu muhimu ya kuzingatia kuhusu majukumu ya wadau wengine:

- Hakikisha kwamba mujumu ya lazima inayohusiana na kila aina ya shughuli (kwa mfano mwiitishaji, anayeona mbele, au mwezeshaji) yanajazwa.

- Hakikikisha kwamba majukumu aliyonayo mdau maalumu hayaendi kinyume na kanuni na malengo.

- Hakikisha kwamba kazi ya nafasi ya wadau inafanyika kwa ushirikiano ili kufanikisha malengo ya pamoja.

## 5.11. Majukumu ya Uadilifu

Ili mchakato wa upatanishi uweze kusonga mbele kunahitajika mlolongo wa majukumu. Jukumu la uadilifu linahusiana na kuhakikisha kwamba mtu anatekeleza majukumu mengi, kusikuwepo na jukumu linalokwenda kinyume na lingine. Baadhi ya majukumu yanafanya kazi chini ya misingi ya kukinzana. Kwa mfano, moja ya sifa ya wajibu wa mtu wa tatu mwezeshaji ni kutopendelea upande wowote. Ikiwa mwezeshaji anaonekana pia kama wakili au bwana mkubwa kikazi wa upande mmoja ulioko katika mgogoro, pande zingine zinaweza kuhisi kwamba mchakato unaegemea upande mmoja. Kuna mchanganyiko wa majukumu mengine, mathalan mtekelezaji na msuluhishi, majukumu haya yanaweza kuhatarisha uaminifu wa kuwa kiungo cha kati au kuendelea kushiriki.

Hoja kuu ni kwamba watu au mashirika yanayotoa msaada mkubwa au wa kiutaratibu kwa pande husika za msingi zinazoshiriki katika mgogoro yanatakiwa kufanya tathmini bila kikomo kuangalia ikiwa au la majukumu yao yanahatarisha kuendelea kushiriki kwao katika mchakato. Pindi masikitiko yanayohusu majukumu yanaibuliwa na kutishia mchakato, hatua madhubuti zinatakiwa kuchukuliwa. Hatua hizi zinaweza kujumuisha kutenganisha watu na majukumu waliyopewa au hata kuwaondoa katika mchakato.

Udhibiti wa mgogoro na wataalamu wa haki za binadamu wanaweza kuwa na majukumu kadhaa wanapofanya kazi katika mfumo wa mgogoro, kwa wakati fulani kwa makupuo. Wakati wowote majukumu ya wadau wanaosimamia haki za binadamu na usimamizi wa mgogoro yanaweza kukamilishana. Hata hivyo kuna wakati hali huwa ndivyo sivyo. Wadau katika medani hizi mbili wanatakiwa kuelewa mchanganyiko wa majukumu yanayokuza michakato ya usuluhishi na zile ambazo zinaleta mkanganyiko. Pindi majukumu fulani hayaeleweki au hayafafanuliwi kwa ufasaha, pande husika zinaweza kupoteza imani katika mchakato wa usuluhishi. Hali hii pia inazuia uwezo wa wadau katika medani hizo mbili kufanya kazi kwa ufanisi.

Kutatua hisia kali zinazohusiana na majukumu ya wadau wanaoshugulika na haki za binadamu na usuluhishi wa mgogoro unajikita katika kuhakikisha wajibu wa uadilifu. Kwa timu ya uingiliaji kati, jambo hili linahitaji kubuni mchakato unaohakikisha kwamba majukumu yote haya yanatekelezwa, na kukamilishana, na kwamba shughuli zao zinaratibiwa ili kufanikisha malengo na azma ya pamoja.

**Wajibu wa ushirikiano**

Ikiwa juhudi za wadau wanaoshiriki katika maeneo mbalimbali ya mgogoro hazitaratibiwa na, wakati wana nia nzuri, vitendo vyao vinaweza kuzuia au kusitisha shughuli zingine. Ni jambo la muhimu kwa wasanifu wa mchakato wa amani kutambua kwamba kuna watu kadha wa kadha ambao wana majukumu tofauti. Mchakato wa amani unatakiwa kuhakikisha kwamba watu hawa wanafahamu matukio makubwa na maamuzi yaliyochukuliwa na pande husika ili watu wote wanaoshiriki katika juhudi za amani wanakufanya kazi kwa ushirikiano ili malengo ya pamoja ya amani, haki na muafaka.

## 5.12. Muhtasari

Mgogoro unaweza kutafsiriwa kama uhusiano wa pande mbili zenye mahitaji yasiyoafikiana au kinzani. Chanzo cha mgogoro kinaonekana katika ngazi mbalimbali, mathalani katika kweli,

michakato, malengo na tunu kadha wa kadha. Maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kufahamu kwamba kuna vipengele vinavyoweza kuchochea mgogoro baina ya pande husika. Kweli hizi ni matamanio ya wajumbe mbalimbali, kuvunjika kwa mawasiliano, utambuzi, mabadiliko ya kimkakati, mabadiliko ya makundi na kujiunga na makundi.

Watu huwa wanachukua njia tofauti ili kudhibiti mgogoro katika hali fulani. Hakuna njia moja tu katika kushughulikia mgogoro. Njia kuu zinazotumiwa na watu ni kuepuka, kulazimisha, kutulia, muafaka na makabiliano. Utatuzi wa matatizo na miafaka ya upatanishi mahiri ndiyo njia pekee zinazoondoa vyanzo halisi vya mgogoro. Ni mbinu za usuluhishi zinazoboresha mambo kwa muda mrefu.

Vyanzo vya mgogoro katika mchakato wa uchaguzi:

- ➢ Ukosefu wa ratiba nzuri ya kampeni za uchaguzi.
- ➢ Uchelewashaji wa nyaraka/nyenzo katika vituo vya kupigia kura.
- ➢ Ukosefu wa baadhi ya majina ya wapiga kura waliojiandikisha katika vituo vya kupigia kura.
- ➢ Ucheleweshaji wa kutangaza matokeo ya uchaguzi baada ya uchaguzi
- ➢ Watu au makundi kadha wa kadha kutopata fursa ya kutumia haki yao ya kupiga kura.
- ➢ Dhulma za maneno/kimaumbile, bughudha, vitisho vya kutumia nguvu na vinavyotumika dhidi ya watu na makundi, kwa kuzingatia umri wao, jinsi, uwezo wao au ulemavu wao, asili yao ya kijamii au uwezo wao wa kiuchumi, maoni yao ya kisiasa au imani yao ya kidini au kwa kuzingatia viashirio vingine vya utambulisho wa kijamii,

## 5.13. Maswali ya kujipima

- ➢ Jadili mitindo mitano tofauti ambamo mgogoro unadhibitiwa.
- ➢ Fafanua majukumu mabalimbali ya watu katika hali ya mgogoro.
- ➢ Toa mifano ya mgogoro uliowahi kutokea sehemu unayofanyia kazi na jinsi ulivyoweza kuushughulikia.
- ➢ Elezea hatua za kudhibiti mgogoro katika nafsi yako.
- ➢ Elezea hatua za kudhibiti mgogoro na mtu mwingine mnayehitilafiana.

Maswali ya ziada

- Jadili mgogoro unaoweza kutokea katika uchaguzi wa kidemokrasia
- Jadili jinsi gani utambulisho wa kijinsia wa mtu, asili yake ya kikabila/imani yake ya dini,umri wake, au uwezo wake, hali yake ya ulemavu, au hadhi yake kijamii vinaweza vinaongeza udhaifu wake katika mgogoro
- Jadili jinsi gani mgogoro unaweza kutatuliwa?

Marejeo

Crime Prevention (Police Handbook)

# 6 SURA YA 6

## Kudumisha Utulivu wa Umma

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya sita.

**6.1. Utangulizi**

**6.2. Mikutano, Shughuli na Maandamano Nchini Tanzania**

**6.3. Viwango vya Kimataifa vinavyotumika katika kudumisha utulivu wa umma**

**6.4. Muhtasari**

**6.5. Maswali ya kujipima**


**Malengo ya mafunzo katika sura ya 6**

**Baada ya kukamilkisha sura hii washiriki wataweza:-**

-  Kujadili haki za watu kufanya maandamano, kujumuika na kujieleza
-  Kuelezea usawa kati ya haki za watu kutumia haki zao za kisheria na uhuru wao bila kuvunja sheria za wengine na utii wa sheria kwa pande zote
-  Kufafanua majukumu ya maofisa wa Polisi katika kudumisha utulivu wa umma
-  Kujadili kanuni zinazotumika kutumia nguvu ili kutawanya mikusanyiko

## 6.1. Utangulizi

Ni jukumu la jeshi la polisi kuhakikisha amani, utulivu na usalama nchini. Hali hii inawekewa mkazo hasa katika kipindi cha uchaguzi wakati wananchi wanashiriki kwa hamasa kubwa katika mchakato wa kampeni za uchagazi, maandamano, mikusanyiko na shughuli zingine ambako wanajieleza na kujihusisha na makundi fulani au vyama vya kisiasa. Ni jambo la muhimu kwa jeshi la polisi kutoegemea upande wowote ule na kuwaruhusu watu kujieleza katika mipaka ya sheria. Wakati wa matukio makubwa ya shughuli za kipolisi, zikijumuisha mikusanyiko na maandamano, maofisa wa polisi wanatakiwa siyo tu kuelewa wajibu wa kisheria za washirki katika matukio hayo. Pia kunahitajika uelewa wa haki, uhuru na wajibu chini ya sheria, ya watu hao wanaoshiriki na wale wasioshiriki bila kujali umri wao, jinsi, uwezo wao au ulemavu wao, asili yao ya kijamii au uwezo wao wa kiuchumi, maoni yao ya kisiasa au imani yao ya kidini au bila kujali viashirio vingine vya utambulisho wa kijamii. Daima kunatakiwa kuwe na usawa baina ya haki za watu wanapotumia haki zao za kisheria na uhuru bila kuvunja haki za watu wengine na utii wa sheria na pande zote. Kudumisha utulivu wa umma kunahusisha haki za watu mbalimbali na uangalizi wa sheria.



Suala la watu kwenda mitaani kuelezea hisia na maoni yao hadharani kuhusu mada yoyote ile wanayozingatia ni jambo la kawaida katika nchi nyingi duniani. Matukio kama hayo, mikutano ya hadhara, maandamano, au vyovyote yatakavyoitwa, yanaonekana kuwa ni mwendelezo wenye mantiki ya uhuru na demokrasia, na pia uhuru wa mtu mmoja na wa watu wote.

Haki na uhuru vinavyotumika katika matukio ya mikusanyiko, maandamano, mikuatano ya hadhara na matukio mengine yanayoshabihiana na hayo

- Haki ya kutoa maoni bila kuingiliwa (ICCPR, Ibara ya 19.1)
- Haki ya uhuru wa kujieleza (ICCPR, Ibara ya 19.2)
- Haki ya kukusanyika kwa amani (ICCPR, Ibara ya 21)
- Haki ya uhuru wa kujumuika (ICCPR, Ibara ya 22.1)

Utumiaji wa haki hizo hauna mipaka.

Haki hizi zinaweza kupunguzwa kiasi, kwa sharti kwamba:

- Ni za kisheri; na
- lazima:
- kwa ajili ya heshima ya haki au sifa njema ya wengine; au
- kwa ajili ya ulinzi na usalama wa taifa au utulivu wa umma, au kwa
- afya au maadili ya umma (ICCPR, Ibara ya 19.3, 21 na ya 22.2)

## 6.2. Mikutano, Shughuli na Maandamano Nchini Tanzania

Nchini Tanzania kila chama cha kisiasa kilichopewa usajili kamili au wa muda kina haki ya kufanya na kuhutubia mikutano ya umma ili kusajili wanachama na kujitangaza. (Sheria ya Vyama vya siasa, Sehemu ya II)

➢ **Utaratibu wa Notisi**

Vyama vya siasa vinatakiwa kutoa notisi kwa maandishi kuhusu mkutano kwa ofisa Mkuu wa jeshi la polisi anayehusika katika eneo hilo. Barua ya notisi inatakiwa kuwasilishwa katika kipindi kisichopungua saa 48 kabla ya mkutano. Barua ya notisi inatakiwa kuwa na vipengele vifuatavyo:

- Jina la chama cha kisiasa kinachowasilisha barua ya notisi
- Mahali na muda wa mkutano kufanyika
- Ajenda na azma za jumla za mkutano
- Vipengele vingine vinavyoweza kuanishwa na Waziri kwa nyakati tofauti, na kuchapishwa katika gazeti la Serikali.

Ikiwa chama cha kisiasa kinafuata utaratibu sahihi wanaweza kuendelea kufanya mkutano isipokuwa na hadi pale ofisa wa jeshi la polis wa eneo hilo atatoa amri inayoelekeza ya kwamba mkutano hauwezi kufanyika.

➢ **Ni wakati gani amri ya kusimamisha mkutano inaweza kutolewa na jeshi la polisi**

Mkuu wa polisi wa eneo husika anaweza katika mazingira yafuatayo kutoa amri ya kusitisha mkutano kwa chama cha kisiasa kilichoandika barua ya notisi.

- Ikiwa chama kingine cha kisiasa au watu wengine waliwahi kutoa notisi ya kuomba kufanya mkutano au shughuli nyingine au maandamano katika eneo hilo hilo na muda huo huo.
- Ikiwa mkutano au maandamano yanalenga kutekeleza, au kutumika kwa azma zisizokuwa za kisheria.
- Ikiwa mkutano unaelekea au una nia ya kuvunja amani au kuhatarisha usalama wa umma katika eneo hilo.
- Ikiwa chama cha kisiasa au kundi la watu wanaoandika barua ya notisi ya kuomba kufanya mkutano siyo chama cha kisiasa kilichosajiliwa au hawatambuliki kuwa wawakilishi walioruhusiwa wa chama cha kisiasa husika.

Amri ya kusitisha mkutano inatakiwa kuwa kwa maandishi na kwa namna hiyo ni rahisi kutoa sababu za kusitisha mkutano na kubainisha au la chama cha kisiasa husika kinaweza kufanya mkutano wakati mwingine au tarehe nyingine inayofaa katika eneo hilo.

Ni muhimu ikumbukwe kwamba amri ya kusitisha mkutano inatakiwa kutolewa ikiwa mambo mengine yote yatashindikana.

➢ **Wajibu wa jeshi la polisi wakati wa maandamano, makusanyiko na misafara**

Jeshi la polisi lina jukumu muhimu sana la kuhakikisha amani, utulivu na usalama nchini katika kipindi cha kampeni za uchaguzi, katika kipindi cha uchaguzi na pia baada ya uchaguzi. Wakati wa maandamano, mikutano na misafara pia, jeshi la polisi linajukumu la:

- Kurahisisha mikutano ya amani na ya utulivu na kuimarisha ulinzi kwa wajumbe wa vyama vya kisiasa na pia kwa viongozi wao.
- Kuhakikisha kwamba vyama vyote vya kisiasa na wagombea wanafaidi haki sawa kuhusu kampeni za uchaguzi.
- Kuhakikisha haki ya kila mtu inakuwa salama na bila bughubha majumbani mwao, ikijumuisha uhuru wa kutobaguliwa, dhulma za maneno/kimaumbile, bughudha na ukatili, ukijumuisha ule wa kingono au kijinsia ambazo zinaweza kumwathiri mtu bila kujali jinsi yake ya kike/kiume.
- Kuwashughulikia watu waosumbua mkutano au wanaojaribu kuleta fujo.

## Hatua za Jeshi la Polisi

Pindi maofisa wa jeshi la polisi wanapotakiwa kuchukua hatua wakati wa maandamano, mikutano, misafara na mikusanyiko ni muhimu kuzingatia kanuni zifuatavyo:

- UHALALI
- ULAZIMA
- UWIANO

Ni muhimu pia kwa maofisa wa jeshi la polisi daima kutenda kwa kuzingatia maadili na wakikumbuka kwamba watawajibika kwa hatua wanazochukua.

***Uhalali***

Kabla ya jeshi la polisi kuchukua hatua yoyote ile, kamanda wa operesheni atauliza ikiwa ana amri kisheria kuingilia kati. Kwa maneno mengine, ikiwa jeshi la polisi lina agizo la kutosha kulingana na sheria za nchi. Mamlaka ya kuingilia kati na mipaka ya hatua hizo za uingiliaji kati zinatakiwa kueleweka na jeshi la polisi *kabla* ya kuchukua hatua yoyote ile. Kanuni ya uhalali inahitaji mfumo wa kisheria unaoeleweka *ukithibitisha* hatua za uingiliaji kati na jeshi la polisi.

***Ulazima (hali inayofaa)***
Kanuni hii ya pili inahitaji kutathmini hali fulani ili kuweza kujibu kulingana na mfumo wa uhalali. Hali inayoendelea ya hali fulani itaiongoza jeshi la polisi kuamua hatua zitakazochukuliwa. Kanuni hii inathibitisha dhana ya kwamba katika kila hali ambako kunatakiwa kudhibiti mikusanyiko ya watu, hali zinatofautiana na maamuzi ya opresheni yanatakiwa kuzingatia matendo ya kundi lile kuliko taratibu zilizoamriwa. Kanuni ya kungalia hali inayofaa inahitaji kwamba hatua za jeshi la polisi zinatakiwa kuwa zenye *mantiki na zilizothibitishwa* na kwamba vipengele vyote vinatakiwa kuzingatiwa.

***Hali ya Kufaa kabisa***
Kanuni ya kufaa kabisa inahusu matumizi ya hali ya juu ya vifaa na watumishi ili kukamilisha au kufikia malengo yaliwekwa katika ngazi ya kupanga. Matumizi ya bora ya vifaa na watumishi yanatakiwa kuwezekana pindi mchanganuo uliokamilika utafanyika katika hali fulani. Mchanganuo huo utajumuisha mazingatio na utafiti wa vipengele vyote vinavyoweza kutoa ushawishi kwa mafanikio thabiti ya hatua inayofaa ili kudhiti hali hiyo.

***Uwiano***
Kanuni ya uwiano inatoa sharti kwa jeshi la polisi kuzingatia azma ya kujiwekea ukomo wa wa mambo, asili yake na kiwango na pia *uhusiano* baina ya ukomo na azma yake. Inahusu uhusiano baina ya njia zinazotumiwa na jeshi la polisi katika hali ya utulivu wa umma, na azma ya mwisho inayotakiwa kukamilishwa. Jeshi la polisi linatakiwa kuwapa watumishi vifaa vyenye kiwango kulingana na mazingira kabla hawajatawanywa. Tayari katika hatua ya kupanga, jeshi la polisi linatakiwa kuchunguza ni mbinu zipi na vifaa vipi vinavyoweza kutumia nguvu ya chini kabisa katika hali fulani. Mchakato huu unatakiwa kutoa muongozo kwa namna ya kimantiki uamuzi wa kutumia mbinu *zenye nguvu kiasi kidogo sana* (za kuzuia) ili kufikia lengo la kisheria la kudumisha utulivu wa umma. Wakati matumizi ya nguvu yataonekana hayaepukiki, yanatakiwa kusitishwa mara moja na maofisa wa jeshi la polisi watakapofikia malengo ya operesheni.

***Shauri za Ukatili wa kingono na kijinsia (SGBV) na Ukatili dhidi ya mtoto (CA)***

Maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kuwa na uelewa unaohusiana na miongozi ya Jeshi la Polisi Tanzania kuhusu namna ya kushughulikia mashauri ya SGBV na zile za CA zinazoweza kutokea katika kipindi cha michakato ya uchaguzi na baada ya uchaguzi, jinsi ya kuripoti kesi hizi na kwa maofisa waliopata mafunzo wa Dawati la Kijinsia na Watoto na wanatakiwa kushughulikia kesi hizi haraka iwezekanavyo.

## Matumizi ya Nguvu ili kutawanya mikusanyiko

Kanuni za Msingi kuhusu Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto zenye Umuhimu maalumu kwa ajili ya “shughuli za kipolisi” kuwatawanya mikusanyiko na maandamano:

Kanuni ya Msingi ya 14 inatamka kwamba:

- Katika kutawanya mikusanyiko ISIYOKUWA HALALI lakini ISIYOKUWA NA VURUGU maofisa wa utekelezaji wa sheria wataepuka kutumia nguvu au ikiwa jambo hili haliwezekani, watatumia kiasi cha nguvu kidogo sana ikiwa kuna ulazima;
- Katika kutawanya mikusanyiko yenye VURUGU watumishi wa utekelezaji wa sheria wanaweza kutumia silaha za moto pale tu njia zisizokuwa za hatari haziwezi kutumika;
- NA kwa kiwango cha chini kabisa cha ulazima;
- NA kwa masharti TU yaliyotamkwa katika Kanuni ya Msingi ya 9 yaani:

Watumishi wa utekelezaji wa sheria hawatatumia silaha za moto dhidi ya watu isipokuwa:

- Katika kujilinda au kwalinda watu wengine dhidi ya tishio linaloelekea kutokea la kifo au la jeraha kubwa,
- Kuzuia kitendo la utendaji uhalifu fulani mkubwa kinachotishia maisha,
- Kumweka chini ya ulinzi mtu anayeonyesha tishio kama hilo na anapinga mamlaka yao,
- Kuzuia kutoroka kwa mtu, na pale tu njia za kutumia nguvu kiasi kidogo zilikuwa hazitoshi ili kufanisha malengo hayo.

Katika kila tukio, matumizi ya makusudi ya kuua kwa kutumia silaha za moto yanaweza kutumika pindi tu hali isiyoepukika kabisa ya kulinda maisha.

- Kanuni ya Msingi ya 14 hairuhusu ufyatuaji wa risasi usiobagua katika kundi lenye vurugu kama mbinu inayokubalika ili kuwatawanya makutano.

## 6.3. Viwango vya Kimataifa vinavyotumika katika kudumisha Utulivu wa Umma

**Viwango vya Haki za Binadamu**

- ➢ Hatua zote za kurejesha utulivu zinatakiwa kuheshimu haki za binadamu
- ➢ Urejeshaji wa utulivu utafanikiwa bila ubaguzi
- ➢ Upunguzaji wa kiasi cha haki utafanyika tu kwa haki zilizoamualiwa na sheria
- ➢ Hatua yoyote ile itakayochukuliwa na kizuizi chochote cha haki kiasi utafanyika tu kwa lengo la kuhakikisha heshima ya haki na uhuru wa watu wengine na kwa azma ya kufikia tu masharti ya uadilifu, utulivu wa umma na ustawi wa jumla
- ➢ Hatua yoyote itakayochukuliwa ya ubinyaji haki utakuwa tu kwa ajili ya haki zenye umuhimu katika masharti ya jamii ya kidemokrasia
- ➢ Hakuna vikwazo vitakavyoruhusiwa kuhusu haki ya kuishi; haki ya uhuru ya kutoteswa; marufuku ya utumwa; marufuku ya kufungwa jela kwa kushindwa kukamilisha wajibu wa kimkataba; marufuku ya kumnyima mtu haki ya kujitetea; utambuzi wa kila mtu mbele ya sheria; au haki ya uhuru wa mawazo, dhamira na dini
- ➢ Njia zisizokuwa za kutumia nguvu zitajaribiwa kwanza kabla ya matumizi ya nguvu
- ➢ Nguvu itatumika tu katika mazingira ya lazima sana
- ➢ Nguvu itatumika tu kwa ajili ya azma za utekelezaji wa sheria halali
- ➢ Nguvu itakayotumika itawiana na malengo ya utekelezaji wa sheria halali
- ➢ Kila jitihada zitafanyika ili kupunguza madhara na majeraha
- ➢ Kutakuwepo na mlolongo wa njia za kutofautisha matumizi ya nguvu

- Hakutokuwepo na ubinyaji wa haki usiokuwa wa lazima kuhusu haki za kujieleza, kujumuika, kukusanyika au wa kuvinjari
- Hakutokuwa na kizuizi cha haki kuhusu uhuru wa maoni
- Uhuru wa kiutendaji wa mfumo wa mahakama utadumishwa
- Watu wote walijeruhiwa kuumizwa kisaikolojia wanatakiwa kupata uanaglizi wa haraka

**Utendaji wa Haki za Binadamu**

*Maofisa wa jeshi la polisi*

- Wanakubali mikakati ya shughuli za kipolisi na kufuatilia viwango vya hisia kali za kijamii baina ya makundi mbalimbali katika jamii na baina ya makundi hayo na mamlaka
- Wanahakikisha wananchi wote wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika michakato ya uchaguzi na kwamba wana kuwa huru dhidi ya ubaguzi, dhulma ya maneno/kimaumbile, bughudha, na vurugu, zikijumuisha ukatilia wa kingono au za kijinsia
- Wako macho kuhusu maandalizi yoyote yale ya maandamano yasiyokuwa halali
- Watakuwa wavumilibvu kwa mikusanyo isiyokuwa halali, ila ya amani, mikusanyiko isiyotoa vitisho, ili hali isije ikawa mbaya zaidi isiyohitajika
- Kufanya mawasiliano na wawakilishi na watu katika mikusanyiko
- Ikiwa kunahitajika kutawanya mikusanyiko, acha daima sehemu ya kutokea
- Shughulikia mikusanyiko kama kundi la watu wenye fikra binafsi na siyo mikusanyiko yenye fikra moja
- Epukana na mbinu zenye kuunga mkono uchochezi wa hasira usiohitajika
- Endeleza mbinu za kudhibiti mikusanyiko zinazopunguza hitaji la kutumia nguvu
- Kujiandikisha katika programu ya mafunzo ili kuboresha stadi za huduma ya kwanza; kushughulikia ukatili wa kijinsia na watoto; kujilinda; matumizi ya vifaa vya wenye mwelekeo wa kujilinda;
- Matumizi ya vifaa visivyosababisha kifo; matumizi ya silaha za moto; tabia ya mikusanyiko; usuluhishi wa mgogoro; na usimamizi binafsi wa msongo wa mawazo
- Kupata na kufanyia mazoezi matumizi ya ngao, mavazi ya kujilinda, kofia ngumu ya kujilinda na vifaa visivyosababisha kifo
- Kupata, kufanyia mazoezi mlolongo wa njia za matumizi mbalimabli ya nguvu, zikijumuisha silaha za kuondoa nguvu zisizokuwa za kusababisha kifo
- Kujifunza na kutumia mbinu za kushawishi, usuluhishi na upatanishi
- Kupanga mapema matumizi ya hatua kwa hatua ya nguvu, ukianzia kwa njia zisizokuwa za matumizi ya nguvu

*Maofisa wa Polisi wanaotoa amri na wasimamizi*

- Toa taratibu za kudumu zinazoeleweka zinazohusiana na mikusanyiko ya amani na huru
- Anzisha mikakati ya polisi jamii na fuatilia viwango vya hisia kali za kijamii kati ya makundi mbalimbali katika jamii, na baina ya makundi hayo na viongozi
- Toa agizo kwa maofisa wa polisi kuwa wavumilivu kwa mikusanyiko isiyokuwa halali, ila ya amani, isiyotishia amani, ili kutofanya hali kuwa mbaya zaidi bila sababu. Malengo makuu ya kukumbuka katika kuendeleza mikakati ya kudhibiti mikusanyiko ni kudumisha utulivu na usalama na ulinzi wa haki za binadamu,

siyo utekelezaji wa ufundi wa kisheria kuhusu vibali au tabia zisizokuwa halali ila zisizotoa vitisho

- Weka na tekeleza taratibu za kudumu zinazoeleweka kuhusu matumizi ya nguvu na silaha za moto
- Toa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu huduma ya kwanza; mbinu za kujilinda; matumizi ya vifaa vya kujilinda; matumizi ya silaha zisizosababisha kifo; matumizi ya silaha za moto; tabia ya kundi kubwa la watu; usuluhishi wa mgogoro; usimamizi wa msongo wa mawazo; na ushawishi, upatanishi na majadiliano
- Kupata na kutoa vifaa vya kujilinda, vikijumuisha kofia ngumu, ngao, mavazi ya kuzuia risasi, barakoa ya kuzuia gesi na magari ya kuzuia risasi za moto
- Kupata na kutoa vifaa vya kuondoa nguvu visivyokuwa vya kusababisha kifo na vifaa vya kutawanya mikusanyiko
- Kupata mlolongo mrefu wa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi tofauti ya nguvu
- Weka miongozo inayoeleweka ya kuripoti kwa kila tukio la matumizi ya nguvu au la silaha za moto
- Fanya udhibiti madhubuti wa ukaguzi, uhifadhi na utoaji wa silaha za moto, ukijumuisha taratibu za kuhakikisha maaoisa wa polisi wanawajibika kuhusu silaha na risasi zinazotolewa kwao
- Kataza matumizi ya silaha na risasi zinazosababisha majeraha bila sababu, madhara au hatari
- Kuza mikakati ya kupunguza hatari kwamba maofisa wa polisi watalazimika kutumia silaha za moto

## 6.4. Muhtasari

Maofisa wa polisi wana jukumu muhimu sana katika kudumisha utulivu wa umma. Wanatakiwa kuhakikisha usawa baina ya haki za watu ili watu hao waweze kutumia haki zao za kisheria na uhuru bila kuvunja haki za watu wengine na utii wa sheria na pande zote. Wakati maofisa wa polisi wanaposhughulika kudumisha utulivu wa umma vitendo vyao daima vinatakiwa kuwa vya kisheria, vya muhimu, sawa na wanatakiwa kutenda kwa mtindo wa kuheshimu maadili.

## 6.5. Maswali ya kujipima

- Je, watu wana haki ya kuandamana, kukusanyka na kujieleza? Jadili.
- Elezea usawa baina ya haki za watu kutumia haki zao za kisheria na uhuru bila kuvunja haki za watu wengine na utii wa sheria wa pande zote.
- Je, maofisa wa polisi wana majukumu gani katika kuhakikisha haki za waandamaji wakati wanapolinda haki za umma?
- Je, ni wakati gani ofisa wa polisi anaweza kusitisha mkutano?
- Maofisa wa polisi wana majukumu gani katika kudumisha utulivu wa umma?
- Ni kanuni zipi zinatumika katika matumizi ya nguvu ili kutawanya mikusanyiko?

# CHAPTER 7
## UKAMATAJI

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya saba.


**7.1.** **Utangulizi**

**7.2.** **Tafsiri**

**7.3.** **Kusudi la Ukamataji**

**7.4.** **Sababu za Ukamataji**

**7.5.** **Ni wakati gani Ukamataji unaruhusiwa?**

**7.6.** **Ukamataji holela**

**7.7.** **Ni zipi haki za watu waliokamatwa?**

**7.8.** **Haki wkati wa ukamataji**

**7.9.** **Ni wajibu za maofisa wa polisi wakati wa kukamata?**

**7.10.** **Mapendekezo ya Umoja wa Mataifa katika kutekeleza Viwango Vya Kimataifa vinavyotumika katika Ukamataji**

**7.11.** **Muhtasari**

**7.12.** **Maswali ya kujipima**

**7.13.** **Nyaraka muhimu na vyanzo vya kujisomea vilivyopendekezwa**

## Malengo ya nmafunzo ya sura ya 7

**Baada ya kukamilisha sura hii washiriki wataweza:-**

- Kutoa tafsiri ya msingi ya dhana ya Ukamataji
- Kudadavua kusudi la Ukamataji
- Kujadili jinsi ya Ukamataji
- Kujadili ni wakati gani ukamataji unaruhusiwa
- Kujadili kwa nini maofisa wa jeshi la plisi hawawezi kukamata bila sababu
- Kujadili haki za watumuhumiwa wakati wanapokamatwa
- Kutoa mifano ya wajibu wa maofisa wa jeshi la polisi katika kumkamata mtu

## 7.1. Utangulizi

Tendo la ukamataji ni muhimu katika mchakato wa kutekeleza sheria na utawala wa haki. Ukamataji ni moja ya ukiukwaji mkubwa wa haki za watu. Kwa hiyo ukamataji kunatakiwa kutumika pale tu kunapokuwepo na ulazima wa kufanya hivyo na kulingana na sheria. Katika sura hii mada ya ukamataji itajadiliwa.

## 7.2. Tafsiri

Hakuna tafsiri dhahiri kuhusu sheria za ndani za ukamataji nchini Tanzania zinaongoza wajibu na utendaji wa jeshi la polisi. Sheria ya Utaratibu wa Makosa ya Jinai, (Na. 9 ya mwaka 1985) hata hivyo inafafanua jinsi gani ukamataji unavyotakiwa kufanyika.

Kabla ya kuendelea na mada hii ya ukamataji ni muhimu kutoa tafsri za msingi kuhusu dhana ya ukamataji, kutia kizuizini na kutia kifungoni katika muktadha wa kimataifa. Tafsiri zifuatazo zimetolewa katika Chombo cha kanuni kwa ajili ya Ulinzi wa watu wote waliotiwa chini ya aina yoyote ile ya kizuizi au ya kifungo. Licha ya kuwa zinaweza kutofautiana nchi baina ya nchi, tafsiri hizi zitakuwezesha kueleawa haki za msingi katika michakato ya kisheria zinazofuatwa wakati wa kutekeleza sheria.

### ➢ Ukamataji

Ukamataji unamaanisha kumshika mtu kwa tendo linalodaiwa kuwa kosa au kwa tendo linalofanyika na mamlaka halali. Ukamataji ni mbinu halali ya kuhakikisha uwepo wa mtuhumiwa wa shauri la jinai kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka.

### ➢ Tafsiri

Mtu aliyewekwa kizuizini kunamaanisha mtu yeyote aliyenyimwa uhuru wake binafsi isipokuwa kwa sababu ya matokeo ya kupatikana na hatia baada ya kutenda kosa.

Kizuizi kinamaanisha hali ya watu waliotiwa kizuizini kama ilivyoainishwa hapo juu.

- ➢ **Kifungo**

Mtu aliyefungwa inamaanisha mtu yeyote aliyenyimwa uhuru wake binafsi kwa sababu ya matokeo ya kupatikana na hatia baada ya kutenda kosa.
.Kifungo kinamaanisha hali ya watu waliofungwa kama ilivyoainishwa hapo juu.

## 7.3. Sababu za Ukamataji

"Hakuna mtu yeyote atakayenyimwa uhuru wake isipokuwa kwa misingi ya sababu hizo kwa mujibu wa utaratibu huo kama ulivyowekwa na sheria" (ICCPR, Ibara ya 9.1).

Masharti yanaonyesha dhahiri kwamba sababu za ukamataji na taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika tendo la ukamataji, zinatakiwa kupatikana katika sheria za Dola. Nchini Tanzania masharti hayo yanapatikana katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na. 9/1985 kuanzia sasa na kuendelea zitatajwa kama Sheria za Mwenendo wa Makosa ya Jinai (C.P.A).

Katika utekelzaji wa sheria, sababu za kawaida za ukamataji ni:

- ➢ Kuzuia mtu kutenda, au kuendelea kutenda, kitendo kisichokuwa halali;
- ➢ Kuwezesha uchunguzi kufanyika unaohusu tendo linalosadikiwa kutokuwa halali lililofanywa na mtu aliyetiwa mbaroni; au
- ➢ Kumpeleka mtu mahakamani kwa ajili ya kumfungulia mashtaka.

Ni muhimu kwa watumishi wa utekelezaji wa sheria kuzingatia ukweli kwamba hatua zote za ukamataji zinatakiwa kuwa za kisheria. Kanuni hii ya kisheria itakiukwa ikiwa mtu ama alitiwa mbaroni au kizuizini kutokana na sababu zisizokuwa dhahiri, au zinakwenda kinyume na sheria za ndani ya nchi. Kwa hiyo kitendo cha ukamataji kiholela siyo cha kisheria na kinatakiwa kuepukwe.

Mtu aliyekamatwa daima anadhaniwa kutokuwa na hatia hadi pale atakapothibitishwa kuonekana na hatia na mahakama inayotambulika kisheria. Kwa sababu hiyo basi kila mtu aliyekamatwa anatakiwa kuangaliwa kwa kufuata misingi ya ubinadamu na kwa mujibu wa sheria. Kutia mbaroni siyo adhabu au mbinu ya kuwaondoa kwa muda watu wasiotakiwa katika jamii ili kusafisha eneo hilo, ila ni kwa makusudi ya kuwaleta watuhumiwa mbele ya mamlaka ya mahakama kwa azma ya kuwa na uhalali wa kumtia mtu mbaroni au kizuizini, na mtu huyu ataachiwa ikiwa kutiwa kwake kizuizini kutaonekana kutokuwa halali.

## 7.4. Jinsi ya Kukamata

Sehemu ya 11(1) ya C.P.A. inatamka kwamba:
"Katika kumkamata mtu ofisa wa polisi au mtu yeyote mwingine yule anayemtia mtu mbaroni kimsingi atamgusa au kumfungia mwili ya yule mtu aliyekamatwa, isipokuwa kumshurutisha mtu kwa kumweka chini ya ulinzi kwa maneno au kwa vitendo."

Kukamata kunaweza kufanyika kwa idhini ya hati au la.

- ➢ **Kukamata kwa kutumia Hati**

  Mamlaka kuliko yote ya udhibiti ni yale yanayoruhusiwa chini ya kibali cha kukamata. Kibali ni hati ya kisheria rasmi, inayomruhusu mtu kuchukua hatua. Nchini Tanzania Hakimu yeyote anaweza wakati wowote ule kutoa kibali kinachoagiza mtu yeyote kukamatwa ambaye

anaaminika kwamba kuna sababu za kutosha mtu alitenda kosa katika mipaka ya mamlaka yake ya kisheria (Sehemu ya 17 ya C.P.A.).

➢ **Kukamata bila Hati**

Kukamata bila hati kwa kawaida kunatokea wakati mtu akitenda kosa la jinai mbele ya ofisa wa polisi. Pia kuna mambo yasiyokuwa ya kawaida kuhusu sheria za ndani. Ni muhimu kuzingatia kanuni za uhalali, ulazima na uwiano wakati wa kumkamata mtuhumiwa bila hati.

Sehemu ya 31(1) ya C.P.A. inatamka kwamba " Ofisa wa polisi anayefanya kitendo cha kumkamata mtu, atampeleka mbele ya mahakama yenye mamlaka ya kisheria ya eneo la kituo cha polisi bila kuchelewa wala kutoa sababu zisizokuwa za lazima na kwa kutegemea masharti yanayotajwa katika dhamana".

Kwa mujibu wa Sehemu ya 16 ya C.P.A. mtu yeyote binafsi anaweza pia kumkamata mtu ikiwa mtu yule atatenda makosa yaliyotajwa katika Sehemu ya 14 ya C.P.A.

## 7.5. Wakati gani tendo la kukamata linaruhusiwa?

Wakati wowote mtu anapokamatwa, lazima iwe kuwa kwa kutuhumiwa kufanya kosa au kwa mamlaka (Baraza la Kanuni Kwa Ajili ya Ulinzi Wa Watu Wote Waliokuwa Chini ya Kizuizi au Kifungo, Kanuni ya 36.2).

Katika utekelezaji wa sheria siyo kila tuhuma za kosa litasababisha (au litasababisha) kukamatwa kwa mhusika. Kuna mlolongo wa vingele vinavyotoa msukumo katika maamuzi ya kukamata au la. Ukubwa na matokeo ya kosa lililotendeka, yakijumuishwa na haiba na tabia, wakati wa kukamata watuhumiwa yatakuwa mazingatio ya msingi. Kwa namna isiyoepukika ubora na uzoefu (ikimaanisha ujuzi) wa maofisa wa utekelezaji wa sheria wanaoshiriki katika kutia mbaroni vinauhusiano na matokeo ya hali maalumu ambako busara ya kukamata inatumika.

## 7.6. Kukamata bila sababu

Ofisa wa polisi kamwe hataweza kumkamata mtu bila sababu au bila maelezo ya kweli. Ukweli huu unatiliwa mkazo katika Sheria za Tanzania na pia katika viwango vya hati za binadamu vya Kikanda na vya Kimataifa.

➢ **Ibara ya 15 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** inatamka kwamba:

(1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu

(a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, au
(b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.
**Ibara ya 9 Tamko la Watu wote la Haki za Binadamu**

“Hakuna mtu yeyote atakayekamatwa bila sababu, kuwekwa kizuizini au kupelekwa uhamishoni.”

➢ **Ibara ya 6 ya Mapatano ya Kiafrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu**

“Kila mtu anayo haki ya uhuru na usalama wa utu wake. Hakuna mtu yeyote anayeweza kunyimwa uhuru wake isipokuwa kwa sababu na masharti yaliyoainishwa hapo awali na sheria , hasa, hakuna mtu yeyote atakayekamatwa bila sababu au kutiwa kizuizini.”

## 7.7. Ni haki zipi walizonazo watu waliokamatwa?

Kuna baadhi ya haki za msingi anazotakiwa kuwa nazo kila mtu aliyekamatwa. Jambo hili linawalazimu maofisa wa polisi la Tanzania kuheshimu na kulinda haki za msingi za watu waliokamatwa. Watu waliokamatwa wana haki kadha wa kadha mara tu wanapokamatwa na baada ya kutiwa mbaroni.

### Haki walizonazo watu mara tu wanakamatwa

➢ **Haki ya mtu kuwa na uhuru na usalama na uhuru wa kuvinjari**
Mtu anaweza tu kukamatwa kutokana na sababu hizo na kwa mujibu wa utaratibu huo kama ilivyoainishwa na sheria. Hii ni kanuni ya uhalali. Kanuni hii ya uhalali itakiukwa ikiwa mtu atakamatwa au kutiwa kizuizini kwa sababu zisizokuwa dhahiri, au ambazo zinakwenda kinyume na sheria za ndani ya nchi. Mtu hatakamatwa au kutiwa kizuizini bila sabau za msingi (bila sababu za uhalali).

➢ **Haki ya kuangaliwa kwa utu na heshima**
Mtu aliyekamatwa ana haki ya kuangaliwa kwa utu na heshima. Maofisa wa polisi wanatakiwa kwa mfano kutoapa au kutumia lugha chafu kwa watuhumiwa, kwa sababu jambo hili linavunja hadhi ya utu.

➢ **Haki ya kupewa taarifa kuhusu sababu za kukamatwa**

Kila mtu aliyekamatwa ana haki ya kujulishwa wakati anapokamatwa sababu za yeye kutiwa mbaroni. (Sehemu ya 23(1) ya C.P.A.)

➢ **Haki ya kukaa kimya. (Hali hii inaungana na haki dhidi ya kujitia hatiani)**
Mtu aliyekamatwa anatakiwa kuwa na haki ya kukaa kimya. Hakuna mtu yeyote atalazimishwa kukiri au kuthibisha dhidi yake mwenyewe. Kila mtu ana haki ya kutojitia mwenyewe hatiani. Haki hii inathibitishwa na ukweli kwamba maofisa wa polisi wanaweza kutamka kwamba mtu ana haki ya kukaa kimya na kwamba kila jambo litakalosemwa linaweza kuandikwa na baadaye kutumika kama ushahidi mbele

ya mahakama ya sheria. Hata hivyo haimaanishi kwamba mtuhumiwa hatakiwi kutoa maelezo mathalan jina, anuani na sababu za kumfanya kuwa mahali fulani.

- **Haki ya kupewa taarifa za mashtaka dhidi ya mtu**
  Mtu aliyetiwa mbaroni pia ana haki ya kupewa haraka taarifa ya mashtaka dhidi yake. Hakuna tafsiri dhahiri kuhusu hasa nini maana ya "haraka" na kipindi hiki kinawweza kutofautiana na sheria za ndani.

- **Haki ya kupewa taarifa kuhusu haki zote**
  Licha ya kuwa watuhumiwa wana haki ya kupata taarifa kuhusu haki hizi toka kwa maofisa wa polisi waliowakamata. Mtu yeyote atapewa taarifa na ufafanuzi wa haki zake na jinsi ya kuzipata haki hizo na kiongozi mhusika wakati anapokamatwa na anapotiwa kizuizini au kifungoni, au haraka kuanzia kipindi kile.

- **Kudhaniwa kutokuwa na hatia**
  Kila mtu aliyetiwa mbaroni ana haki ya kudhaniwa na kwamba hana hatia hadi pale itakapothibitisdhwa kuwa ana hatia kwa mujibu wa sheria kupitia shauri la umma litakalosiokilizwa katika mahakama ambako mtuhumiwa ana hakikisho la kutosha la kujitetea. Ni jukumu la mahakama kuamua kwamba mtuhumiwa ana hatia. Jambo hili linaweza kufanyika tu baada ya vielelezo vyote vya ushahidi kusikilizwa na mtuhumiwa akathibitishwa kuwa ana hatia pasipo na shaka lolote.

## 7.8. Haki alizonazo Mtuhumiwa mara baada ya kukamatwa

Maofisa wa Jeshi la Polisi wanatakiwa kuelewa kwamba kuna miongozo maalumu ya Kitaifa na ya Kimataifa kwa ajili ya uangalizi wa wanawake na vijana wadogo waliotiwa kizuizini (kwa mfano Kanuni za Wastani kwa ajili ya uangalizi wa Wafungwa (Standard Minimum Rules, SMR) na Kanuni za Wastani za Viwango vya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya hatua zisizokuwa za kifungo, UN Standard Minimum Rules for Non-custodial Measures ('Kanuni za Tokyo') na Kanuni za Umoja wa Mataifa zenye maelezo ya kina kwa ajili ya uangalizi wa wafungwa wanawake na hatua zisizokuwa za kifungo kwa watuhumiwa wanawake, vinginevyo zikijulikana kama "Kanuni za Bangkok" (za mwaka 2010). Kwa taarifa zaidi kuhusu kanuni hizi, tazama marejeo mwishoni mwa sehemu hii, ambako kuna vyanzo vya vitabu viwili kuhusu swala hili. Nyingi ya kanuni hizi zinatumika kwa maeneo ya Magerezani ila pia zina mahusiano na maofisa wa polisi wakati wanapotia mbaroni, zikijumuisha kuwa na nyenzo tofauti kwa wanaume na wanawake, pia watu wazima na vijana wadogo wasiosindikizwa.

Katika sheria za Tanzania, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Kanuni ya Adhabu zina masharti ya jumla kuhusu haki za binadamu kwa watu waliowekwa kizuizini. Taratibu za kudumu za kiutendaji za Jeshi la Polisi Tazania zina miongozo maalumu kuhusu kanuni za kutia mbaroni, wakati wanawake wanapotiwa mbaroni au kupekuliwa na maofisa wa polisi wa kike. Maofisa wanatakiwa kuhakikisha kwamba wakati vijana wadogo wanapotiwa mbaroni, masharti ya Sheria ya Mtoto yanapaswa kuzingatiwa.

- **Haki ya kupelekwa mahali pa kifungo**

  Watu wanatakiwa kuwekwa kizuizini mahali pa kifungo palipokubaliwa kisheria.

- **Haki ya kuomba dhamana**
  Watu wana haki ya kuomba dhamana wakati wanaposhtakiwa kwa kutenda kosa linaloweza kupewa dhamana.

- **Haki ya kupelekwa haraka mbele ya Hakimu au Ofisa mwingine aliyeruhusiwa Kisheria**
  Mtu yeyote aliyekamatwa atapelekwa haraka mbele ya Mamlaka ya kisheria. Kupelekwa mahali pa kifungo na kupelekwa haraka mbele ya Hakimu au Ofisa mwingine aliyeruhusiwa Kisheria kutumia nguvu ya kimahakama atakayeamua kuhusu uhalali na ulazima wa kukamata, (ICCPR, Ibara ya 9.3; Baraza la Kanuni, Kanuni ya 11 na ya 37. Kipindi cha muda kinachohitajika ili mtu aweze kupelekwa mahakamani kinatofautiana kati ya nchi na nchi. Kipindi hiki kinatajwa kwa kawaida na kujulikana kama Kifungo cha Polisi. Kipindi kinachofuata ni kile kinachojulikana kama kizuizi cha kabla ya mashtaka.

- **Haki ya kutoteswa au kuwekwa chini ya uangalizi usiokuwa wa kibinadamu au wa kudhalilishwa**
  Marufuku ya kutesa inatumika kwa watu wote walio katika hali yoyote ya kutiwa mbaroni, kizuizini au kifungoni. Maofisa wa polisi kinagaubaga wanakatazwa kuchulia hali ya mtu aliwekwa kizuizini kupata tamko la kukiri, kumtia hatiani au kutoa ushahidi dhidi ya watu wengine.

- **Haki ya kupata mashtaka ya haki katika kipindi kinachotosha**
  Mtu aliyewekwa kizuizini kutokana na mashtaka ya jinai atakuwa na haki ya mashtaka ya haki katika kipindi cha kutosha au kuachia mashtaka ya kiporo.

- **Haki ya kuwaarifu ndugu na watu wengine muhimu kuhusu kutiwa kizuizini**
  Mara baada ya kutiwa mbaroni na baada ya kila hamisho toka sehemu moja ya kizuizini au ya kifungoni kwenda ehemu nyingine, mtu aliyetiwa kizuizini au kifungoni atapewa haki ya kuwaarifu au kuomba kiongozi anayefaa kuwataarifu ndugu zake au watu wengine wanaofaa kutaarifiwa kuhusu chaguo lake akiwa ametiwa mbaroni, kizuizini au kifungoni au hamisho lolote na mahali alipowekwa kizuizini.

- **Haki ya kupata msaada wa kisheria na kuwasiliana na mawakili**
  Mtu aliyetiwa mbaroni ana haki ya kupata msaada wa kisheria toka kwa wakili na anatakiwa kurahisishiwa nyenzo za kutosha kunufaika na haki hii. Anatakiwa kupewa wakili na mamlaka ya kimahakama au mamlaka nyingine ikiwa mtu aliyetiwa mbaroni hana wakili wa chaguo lake, na asiyepokea malipo ikiwa mtu aliyetiwa mbaroni hana uwezo wa kutosha wa kumlipa.

  Vfuatavyo ni vipengele vinavyounga mkono haki ya kumpata mwakilishi wa kisheria. Watu waliotiwa mbaroni na wawakilishi wao wa kisheria wana haki zifuatazo:

  - Kupokea mawasiliano ya haraka na timilifu ya amri yoyote ya kuwekwa kizuizini, pamoja na sababu zinazoambatanishwa;
  - Kuwasiliana miongoni mwao na kuwa na muda na nyenzo za kutosha kwa ajili ya mashauriano katika usiri na bila kucheleweshwa au kukaguliwa;
  - Kuwasiliana miongoni mwao wakiwa wanaonekana na siyo kusikilizwa na mtumishi

wa utekelezaji wa sheria; mawasiliano hayo hayatakubalika kama ushahidi dhidi ya mtu aliyewekwa kizuizini isipokuwa ikiwa yatakuwa na mahusiano na uhalifu unaoendelea au unayokusudiwa;

- ➢ Kufikia taarifa zilizorekodiwa katika muda wowote ule wa mahojiano, mida baina ya mahojiano na utambulisho wa watumishi walioendesha mahojiano na ule wa watu wengine waliokuwepo wakati wa mahojiano;
- ➢ Kuwa na fursa ya kusikilizwa na mamlaka ya kimahakama au mamlaka nyingine
- ➢ Kuchukua mwenedno wa mashtaka kwa mujibu wa sheria za nchi mbele ya mamlaka ya kisheria au mamlaka nyingine ili kuchagiza uhalali wa kizuizi kwa lengo la kupata hati ya kuachiliwa kwa mtu aliyetiwa kizuizini, ikiwa siyo halali;
- ➢ Kutoa malalamiko kuhusu uangalizi wa mtu aliyewekwa kizuizini, hasa kuhusu kesi ya utesaji au ya kinyama, usiokuwa wa kibinadamu au hali ya udhalilishaji, kwa uongozi au mamlaka ya juu waliopewa mamlaka ya kupitia au ya kurekebisha mashtaka.

## 7.9. Nini wajibu wa maofisa wa polisi wakati wanapowakata watuhumiwa?

Pamoja na haki, kuna wajibu kwa maofisa polisi kuheshimu na kutimiza haki hizo. Kwa hiyo maofisa wa polisi wana wajibu zifuatazo wakati na baada ya kuwakamata watuhumiwa.

➢ **Kumtaarifu mtuhumiwa kuhusu haki zake**

Inamaanisha kwamaba maofisa wa polisi wanatakiwa kuwataarifu watu waliotiwa mbaroni juu ya haki zao na namna ya kuzipata haki hizo. Haki mahsusi anazotakiwa kuwaarifu watu waliokamatwa ni kama ifuatavyo:

- o Haki ya kukaa kimya na kutokubali kuwa na hatia na hali hii haitafsiriwa kuwa kukubali kosa
- o Haki ya kuwa na mawasiliano na ndugu au rafiki wa karibu na ya kutembelewa na ndugu huyo
- o Haki ya kuwasiliana na wakili na kwa siri
- o Haki ya kwamba mwanasheria atateuliwa ikiwa mtuhumiwa hana uwezo wa kumlipa wakili
- o Haki ya kufikishwa mbele ya mahakama katika muda unaokubalika (kama inavyotamkwa katika sheria za kila nchi)
- o Haki ya kuhojiwa mwanasheria akiwepo, isipokuwa ikiwa haki hiyo imebatilishwa; na
- o Ikiwa mtuhumiwa ni raia wa taifa la kigeni, ana haki ya kuwasiliana na maofisa wa ubalozi wa nchi yake au wa ubalozi mdogo wa taifa lake

➢ **Kurekodi taarifa zifuatazo**

Maofisa wa polisi wanatakiwa kurekodi taarifa zifuatazo:

- o Sababu za kumkamata
- o Muda wa kumkamata
- o Muda wa kupelekwa mahabusi
- o Muda wa kufikishwa mbele ya mamlaka ya kimahakama au mamlaka nyingine
- o Utambulisho wa watumishi wa utekelezaji sheria husika

- o Taarifa kamili kuhusu mahali pa kifungo
- o Maelezo ya mahijiano.
- o Mali ya mtu aliyewekwa kizuizini na jeshi la polisi.

Katika orodha hiyo kunatakiwa kuongezwa:

- o Tarehe na muda mtu alipongizwa mahali pa kifungo
- o Hali ya kiafya
- o Kila anapotembelewa iwe ofisa wa mahabusi, wanasheria, madaktari ndugu wa familia na marafiki
- o Mida ya mazoezi
- o Muda na tarehe ya uhamisho kwenda eneo lingine la kifungo au kuachiwa.

- ➢ Taarifa ya kumbukumbu ya kukamatwa inawasilishwa kwa mtu aliyetiwa kizuizini, au kwa mwanasheria wake
- ➢ Pale panapohitajika, patatolewa huduma ya ukalimani wakati wa mahojiano

## 7.10. Mapendekezo ya Umoja wa Mataifa ili kutekeleza Viwango vya Kimataifa vinavyotumika katika Ukamataji

Kwa mujibu wa Kanuni Za Viwango vya Wastani kwa ajili ya Uangalizi wa Wafungwa (mwaka 1955), Magereza yanapaswa, pamoja na masuala mengine:

- Kuwaweka kizuizini wanawake na wanaume katika sehemu tofauti,
- Kuwatenganisha wafungwa vijana na watu wazima, na
- Kutumia maofisa wa kike kuwasimamia na kuwahudumia wafungwa wa kike.

Haya yote yaliwahi kufanyiwa marekebisho katika Kanuni za Bangkok kuhusu Uangalizi wa Wafungwa wa kike.

*Kwa Maofisa polisi wote:*

- ➢ Kupitia mara kwa mara, ili kuwa na uelewa dhahiri kuhusu mamlaka yao ya kukamata, na taratibu za kufuata wakati wa kukamata

- ➢ Kushiriki katika mafunzo ili kuendeleza na kudumisha ujuzi baina ya mtu na mtu, na hasa ujuzi wa mawasiliano, ili kuwawezesha kufanya tendo la ukamataji kwa uweledi, kwa busara na kwa heshima kwa utu wa binadamu

- ➢ Wakati hali ya upinzani siyo bayana, wanatakiwa kujaribu kwa utulivu, heshima, lugha iliyopoa wakati wanapowakamata watuhumiwa, na kutumia sauti ya mamlaka pale tu inapoonekana kuna umuhimu

- ➢ Kuendeleza na dumisha ujuzi wa kiufundi na wa kimkakati utakaowawezesha kutekeleza tendo la ukamataji kwa uweledi, busara na kwa heshima ya utu wa binadamu

- ➢ Endeleza na dumisha ujuzi wa matumizi ya pingu na njia zingine kwa ajili ya kumzuia mtu
- ➢ Endeleza kujiamini, kukijumuishwa na ujuzi wa kina wa kujilinda.
- ➢ Hakikisha unapata kibali cha kutkamata, pale inapowezekana
- ➢ Kuhifadhi kadi ndogo mifukoni mwa sare, ikiwa inaorodhesha haki za mtu unayetiwa mbaroni, na usome haki hizo, kwa kunukuu, kwa mtu aliyekamatwa pindi atakapohifadhiwa
- ➢ Jifunze mbinu za usuluhishi wa mgogoro kupitia mafunzo yanayotolewa kazini, au kupitia programu ya elimu ya kijamii
- ➢ Weka kwa uangalifu wa juu rekodi za ukukamataji, zikiwa na maelezokwa kina ikiwa kwako kanuni ya dole gumba

*Kwa watumishi wa kutoa amri na wa usimamizi:*

- ➢ Toa na tekeleza taratibu za kudumu kuhusu kanuni za ukamataji
- ➢ Toa mafunzo ya kudumu kwa maofisa wa polisi wote kuhusu kanuni za ukamataji, haki za watu wanaokamatwa, na mbinu za ukamataji ili kutekeleza tendo la ukamataji salama na lenye kuheshimu ubinadamu
- ➢ Toa mafunzo ya ujuzi wa mtu binafsi, mbinu za usuluhishi wa mgogoro, kujilinda, na mbinu za matumizi ya kuzuia
- ➢ Andaa fomu za kawaida za kurekodi taarifa za tendo la ukamataji, zikizingatia maelezo ya sura hii, na sheria na taratibu za ukamataji katika himaya yako kisheria
- ➢ Ikiwa ukamataji unaweza kuandaliwa mapema, hakikisha kwamba kunakupwepo mlolongo wa chaguo, na kwamba kupanga huko, maandalizi, kupeana taarifa muhimu, na mbinu zinazofaa katika mazingira na hali ambpo ukamataji utafanyika
- ➢ Kupokea taaria ya zoezi zima la ukamataji uliyoagiza kwa maofisa wote walioshiriki, na kwa uangalifu mkubwa chunguza kumbukumbu za ukamataji ili kuwa na uhakika kwamba limekamilika
- ➢ Weka taratibu za kuhakikisha kwamba watu waliokamatwa hawazuiwi kuwafikia wanasheri wao

## 7.11. Muhtasari

Tendo la ukamataji ni la ukiukwaji mkubwa wa haki za mtu yeyote. Kwa hiyo maofisa wa polisi wanatakiwa kuhakikisha wanaheshimu na kulinbda haki za kila mtu aliyetkamatwa.

## 7.12. Maswali ya kujipima

- ➢ Toa tafsiri ya maneno ukamataji, kizuizini na kifungoni
- ➢ Ni nini azma ya ukamataji?
- ➢ Jinsi gani mtu anaweza kukamatwa?
- ➢ Ni wakati gani ukamataji kunaruhusiwa?
- ➢ Ni zipi haki za watu waliokamatwa?
- ➢ Ni mambo gani mahsusi maofisa wa polisi wanatakiwa kuzingatia wakati wanapowakamata wanawake au vijana wadogo?
- ➢ Toa mifano 5 ya wajibu wa mafisa wa polisi wanapomkamata mtuhumiwa?

Marejeo:

AdvocAid (2011) "United Nations Rules for the Treatment of Female Prisoners - Bangkok Rules Training Booklet," http://www.advocaidsl.com/wp-content/uploads/2011/03/AdvocAid-Bangkok-Rules-training-booklet-Nov-11.pdf

DCAF (2012) "Penal Reform and Gender: Update on the Bangkok Rules" http://www.dcaf.ch/Publications/Penal-Reform-and-Gender-Update-on-the-Bangkok-Rules

# SURA YA 8

## Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto

8

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya nane.


**8.1.** **Utangulizi**

**8.2.** **Kanuni Za Msingi Za Kimataifa Kuhusu Matumizi ya Nguvu Na Silaha Za Moto Na Watumishi Wa Utekelezaji Wa Sheria (LEO's)**

**8.2.1.** **Matumizi ya Nguvu**

**8.2.2.** **Uwajibikaji katika matumizi ya nguvu na silaha za moto**

**8.2.3.** **Mazingira yanayoruhusiwa kutumia sihala za moto**

**8.2.4.** **Taratibu za kutumia silaha za moto**

**8.2.5.** **Baada ya kutumia silaha za moto**

**8.3.** **Mbinu za kufafanua uwiano**

**8.4.** **Matumizi ya nguvu mwendelezo**

**8.5.** **Kanuni ya Dhahabu**

**8.6.** **Muhtasari**

**8.7.** **Maswali ya kujipima**

## Malengo ya mafunzo katika sura ya 8

**Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-**

- Kufafanua Kanuni za msingi katika matumizi ya nguvu na silaha za moto na maofisa wa polisi
- Kutoa mifano ili kuelezea uwiano wakati wa matumizi ya nguvu.
- Kufafanua ngazi tofauti za nguvu zinazoweza kutumika
- Kuelezea taratibu za kufuatwa kabla, wakati na baada ya kutumia silaha za moto

## 8.1. Utangulizi

Matumizi ya nguvu ni moja ya vipengele vya kutekeleza sheria ambapo maofisa wa polisi wanaweza kudhulumu haki za binadamu. Wakati maofisa wa polisi wanapotakiwa kutumia nguvu na silaha za moto, kipengele cha muhimu kabisa cha kukumbuka ni kanuni ya uwiano kwa kutumia nguvu ***kadiri ilivyo ndogo iwezekanavyo***. Inamaanisha ikiwa hakuna haja ya kutumia nguvu wakati wa ukamataji, hutakiwi kutumia nguvu kabisa na ikiwa utatumia nguvu unatakiwa tu kutumia nguvu kiasi inayohitajika wakati wa kumkamata mtuhumiwa. Kanuni ya uwiano daima inatakiwa kuwa chaguo na inategemea mbinu inayotumia nguvu kiasi iwezekanavyo ili kufikia lengo. Jambo la muhimu la kukumbuka wakati unamkamata mtuhumiwa ni kwamba kunatakiwa kuwe na uwiano baina ya tendo la kutenda wajibu wako vizuri na kuheshimu haki za mtuhumiwa. Wakati watuhumiwa wanapokamatwa bado hawajaonekana kuwa na hatia na mahakama ya sheria. Ni muhimu kukumbuka kwamba maofisa wa polisi hawawezi kukamata au kutumia nguvu za ziada kumuadhibu mtuhumiwa na kwamba mtuhumiwa hana hatia hadi pale mahakama itakapothibitisha kuwa ana hatia.

Pamoja na vizuizi yote ya haki za msingi za binadamu, vipengele muhimu vyaokuzingatia wakati unapotumia nguvu ni kanuni za uhalali, ulazima na uwiano. Daima maafisa wa polisi wanatakiwa kutenda kwa namna ya kuheshimu maadili na kuelewa kwamba watawajibika kwa matendo yao.

Matumizi ya makusudi ya kuua kwa kutumia nguvu yanaweza tu kufanyika wakati kunapotokea hali isiyoepukika ili kuokoa maisha.

Katika sura hii matumizi ya nguvu na silaha za moto yatajadiliwa.

## 8.2. Kanuni Za Msingi Za Kimataifa Kuhusu Matumizi Ya Nguvu Na Silaha Za Moto Na Watumishi Wa Utekelezaji Wa Sheria (LEO's)

Umoja wa Mataifa uliwahi kuandaa kanuni za msingi za kimataifa kuhusu matumizi ya nguvu na silaha za moto kama ifuatavyo;

### 8.2.1. Matumizi ya Nguvu

Katika matumizi ya nguvu kanuni zifutazo zinatumika kama miongozo kwa maofisa wa polisi.

- Kila mtu anayo haki ya kuishi, usalama wa mtu, na uhuru dhidi ya utesaji na vitendo vingine vya kidhalimu, visivyokuwa vya kibinadamu na vya kudhalilisha au vya kuadhibu.
- Njia zisizokuwa za kutumia nguvu zitajaribiwa mwanzo.
- Nguvu itumike pale penye ulazima mkubwa.
- Nguvu itumike tu kwa madhumuni ya kutekeleza sheria.
- Hakutoruhusiwa mambo yasiyokuwa ya kawaida au visingizio katika matumizi yasiyokuwa ya halali ya nguvu.
- Matumizi ya nguvu daima yanatakiwa kuzingatia uwiano kwa malengo halali.
- Matumizi ya nguvu yanatakiwa kuzuiliwa.
- Madhara na majeraha yanatakiwa kupunguzwa.
- Mlolongo wa njia kwa ajili ya matumizi tofauti ya nguvu zinatakiwa kuwepo.
- Maofisa wote wa polisi wanatakiwa kupata mafunzo kuhusu matumizi tofauti ya nguvu.
- Maofisa wote wa polisi wanatakiwa kupata mafunzo kuhusu matumizi yasiyokuwa ya nguvu.

## 8.2.2. Uwajibikaji katika matumizi ya nguvu na silaha za moto

Matumizi ya nguvu na ya silaha za moto ni ukiukwaji mkubwa wa haki za msingi za binadamu. Maofisa wa polisi daima wanatakiwa kuwajibika kutokana na matendo yao. Kuhusu swala la uwajibikaji kanuni zifuatazo zinatumika kama miongozo.

- Matukio yote ya matumizi ya nguvu na ya silaha za moto yatafuatiwa na ripoti na kupitiwa upya na maofisa wa ngazi ya juu.
- Maofisa wa ngazi ya juu watawajibika kutokana na matendo ya askari walio chini ya himaya zao ikiwa ofisa wa ngazi wa juu alikuwa anajua kuhusu dhulma ila akashindwa kuchukua hatua madhubuti.
- Mafisa wa polisi waliokataa amri isiyokuwa halali kutoka kwa maofisa wao wa ngazi ya juu watapewa kinga.
- Maofisa wa polisi waliokiuka miongozo hii hawatasamehewa kwa minaji ya kwamba walikuwa wanatekeleza amri toka kwa wakuu wao.

## 8.2.3. Mazingira yanayoruhusu matumizi ya Silaha za Moto

Mazingira yanayoruhusu matumizi ya nguvu yanaweza kutofautiana baina ya nchi na nchi. Mazingira yafuatayo yaliwahi kubainika kwa ajili ya matumizi ya nguvu iliyoruhusiwa.

- Silaha za moto zinatakiwa kutumika tu katika mazingira ya ulazima sana.
- Silaha za moto zinatakiwa kutumika tu kwa ajili ya kujilinda au kuwalinda watu wengine dhidi ya tishio la kifo linaloelekea kutokea au majeraha makubwa.
- Kuzuia uhalifu mkubwa unaoshirikisha tishio kubwa dhidi ya maisha.

au

- Kumkamata au kuzuia kutoroka kwa mtu anayeonyesha tishio hilo na anayekaidi juhudi za kusimamisha tishio hilo.

na

- Katika kila kesi, ikiwa tu hatua za mwisho hazitoshi.
- Matumizi ya makusudi ya nguvu na silaha za moto yanayosababisha kifo yataruhusiwa tu katika mazingira yasiyoepukika ili kulinda maisha ya binadamu.

### 8.2.4. Taratibu za kutumia Silaha za Moto

- Ofisa anatakiwa kujitambulisha kama ofisa wa polisi.

na

- Ofisa anatakiwa kutoa onyo dhahiri.

na

- Ofisa anatakiwa kuruhusu muda wa kutosha ili anayeonywa aweze kutii.

ila

- Jambo hili haliitaji ucheweleshaji ikiwa linaweza kusababisha kifo au majeraha wakubwa ya ofisa au watu wengine.

au

- Ikiwa ni dhahiri kwamba jambo hili halina maana au umuhimu wowote katika hali husika kufanya hivyo.

### 8.2.5. Baada ya kutumia Silaha za Moto

- Msaada wa kimatibabu unatakiwa kutolewa kwa watu wote waliojeruhiwa.
- Ndugu na marafiki wa watu walioathirika wanatakiwa kupewa taarifa.
- Uchunguzi unatakiwa kuruhusiwa ikiwa utaombwa au ikiwa kuna umuhimu wa kufanya hivyo.
- Ripoti yenye maelezo ya kina ya tukio inatakiwa kutolewa.

## 8.3. Mbinu ya kufafanua Uwiano

Ili kujua mbinu gani itatumia nguvu kiasi kidogo, uwezo kiasi wa kila mbinu kwanza unatakiwa kubainika. Kupima mbinu kwa kuzingatia vipimo vya ulinganisho wa alama kutasaidia.

Viwango vya uwezo wa "mbinu za nguvu ya maumbile" vinaweza, kwa mfano, kupimwa kwa ulinganisho wa alama 1-10. Alama inayohusiana na mbinu iliyo na hitilafu kwa jamii, kwa mfano 1, na alama ya juu itatolewa kwa mbinu iliyo na madhara kwa mtuhumiwa, kwa jamii na kwa ofisa wa polisi.

**Mfano huu utafafanua kanuni ya uwiano na kuonyesha viwango tofauti vya matumizi ya nguvu inyoweza kutumika wakati wa kumkamata mtuhumiwa.**

## VIWANGO VYA UWEZO WA NGUVU WAKATI WA KUMKAMATA MTUHUMIWA

### I. UWEPO WA MAOFISA WA POLISI: UTAMBULISHO WA MAMLAKA

Hatua ya kwanza ni pindi ofisa wa polisi anajitambulisha kama ofisa wa polisi (kwa kuonekana au kwa mdomo) – Ukiwa katika sare yako ya kipolisi na kumwambia mtuhumiwa kwamba wewe ni Ofisa wa jeshi la polisi.

### II. MAELEKEZO YA MDOMO

Kwa kutoa maelekezo ya mdomo, amri ya kumkamata mtuhumiwa. Pindi ofisa wa polisi anamwambia mtuhumiwa kwamba yuko chini ya ulinzi au anapotoa amri au maagizo kwa mdomo kwa mtu kufanya jambo fulani. (Kwa mfano: wakati mtuhumiwa anajaribu kukimbia na ofisa wa polisi anampigia kelele ili asimame.)

## III. UDHIBITI WA MIKONO MITUPU

- **UDHIBITI LAINI WA MIKONO MITUPU**

Hizi ni mbinu anazoweza kutumia ofisa wa polisi zilizo na matokeo ya kusababisha kiasi cha majera madogo sana. (Kwa mfano: Wakati ofisa wa polisi anapomgusa mabegani mtuhumiwa na kumwagiza amfuate, au anamshika mkono akimvuta mtuhumiwa ili atembee)

- **UDHIBITI WA MKONO MTUPU NA MGUMU**

Hizi ni mbinu anazoweza kutumia ofisa wa polisi na zina uwezekano wa kusababisha majeraha. (Kwa mfano: Ikiwa kuna ukaidi kadha wa kadha upande wa mtuhumiwa mbinu hizi zinaweza kutumika, kama kutoa shinikizo mwilini katika maeneo nyeti, mbinu za kufuatana, mbinu za kudhibiti chini na ustadi wa kucheza na maungo ya mwili mathalan kukunja mikono na vidole.)

## IV. USTADI WA KUDHIBITI MISULI KUFANYA KAZI

Hizi mbinu zinazoweza kutumiwa na jeshi la polisi ikiwa kuna ukaidi mkali na ustadi huu unaweza kusababisha majeraha kadha wa kadha. (Kwa mfano: kubinya mishipa ya shingo kwa upande—ikiwa maofisa wa polisi walipata mafunzo ya kutumia mbinu hizi—au kupiga miguu/mikono kama shinikizo juu ya maneo ya mishipa ya fahamu ili kusababisha kutofanya kazi kwa muda kwa viungo vya mikono na miguu na wakati huo huo kuziraisha; mapigo mengine yanasababisha mtu kutotembea au kutotenda (Karate, Taikodo, n.k.).

## V. MBINU ZA KUTUMIA KEMIKALI

Matumizi ya kemikali mathalani gesi ya CO/OC (gesi ya kutoa machozi) au gesi ya pilipili itatumika tu ikiwa itaidhinishwa na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi na kwa mujibu wa taratibu za usalama na kupuliziwa na maofisa wa Jeshi la Polisi waliopata mafunzo na kufuatana na maagizo ya kisheria yanayodhibiti matumizi ya kemikali hizi. (Kwa mfano gesi ya kutoa machozi haitakiwi kutumika katika maeneo yaliyofungwa au yasiyopitisha hewa.)

## VI. RUNGU NA SILAHA ZA KUGONGA

Silaha hizi za kugonga zinatakiwa kutumika tu pale zinapopata idhini ya idara na kutumiwa na maofisa wa polisi waliopata mafunzo.

## VII. MATUMIZI YA SILAHA ZA MOTO

Silaha za moto zinatakiwa kutumika tu kama hatua ya mwisho. Silaha za moto zitatumika tu wakati panapoonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo ili kujilinda menyewe na kuwalinda watazamaji wasiokuwa na hatia na pindi unapomkamata mtu. Ikiwa utaamua kutumia silaha yako ya moto wakati wa kukamata, ni jambo la muhimu kwanza kufyatua risasi ya onyo ikiwa hali inaruhusu. Ikiwa utafyatua risasi, jaribu kufyatua risasi maeneo ya mwili ambayo hayatasababisha kifo kwa mtu yule. Kumbuka azma ya kukamata ni kumfikisha mtuhumiwa mbele ya mahakama.

Kwa kawaida silaha za moto zinatakiwa tu kutumika kwa ajili ya kujilinda au kuwalinda watu wengine dhidi ya tishio linayoelekea kusababisha kifo au majeraha makubwa. Unapofyatua risasi kwa madhumuni ya kujilinda (kulinda maisha yako au ya mtu mwingine), azma ya kufyatua

risasi inakuwa tofauti.


**Dokezo lenye thamani** ni kwamba "alama inayopewa mbinu" pia inamaanisha kuwa makini tunapoitumia. Kwa maneno mengine, jinsi alama za mbinu zinavyokuwa za juu zaidi ndivyo ofisa wa polisi anatakiwa kuwa makini zaidi anapotaka kutumia mbinu hiyo. Kama kanuni huwa mtu anatakiwa kuwa makini pindi anapotaka kufanya kitendo cha kufyatua risasi kuliko wakati anapotaka kumkamata mtuhumiwa, na kuwa makini zaidi wakati anapotaka kumkamata mtu kuliko wakati anapoandika notisi ya maandishi.

Kanuni Ya Matumizi Ya Nguvu Kwa Uwiano daima yanatakiwa kuzingatiwa. Kwa sababu zaidi ya matokeo mathalan **msongo wa mawazo wa baada ya tukio la kuua kwa kutumia silaha ya moto** upande wa ofisa polisi kwa sababu aliua mtu, **madai makubwa ya kiraia** yanaweza pia kuelekezwa kwa ofisa wa polisi. Na kwa kiwango kikubwa zaidi hali hii inaweza kuharibu mahusiano na jamii.

## 8.4. Kutumia Nguvu kwa namna ya Mwendelezo

Wakati wa kutumia nguvu maofisa wa polisi daima wanatakiwa kuzingatia uwiano. Jambo hili linamaanisha kwamba ikiwa hakuna haja ya kutumia nguvu kwa mfano ili kumkamata mtu, hutakiwi kutumia nguvu yoyote kabisa na ikiwa unahitajika kutumia nguvu unatakiwa kutumia kiasi cha nguvu cha lazima ili kumkamata. Mtu anapozidi kuwa kaidi ndivyo unavyotakiwa kutumia nguvu zaidi. Jambo hili linatajwa kama uendelezaji wa matumizi ya nguvu. Kwa upande mwingine ikiwa mtu atatii amri, wewe kama ofisa wa polisi hutatumia nguvu au nguvu hafifu. Hali hii inatajwa kama upunguzaji wa nguvu.

Nguvu inayotumiwa na maofisa wa jeshi la polisi inatakiwa kulandana na tabia ya mtuhumiwa katika kila hali.



**Ili kuwawezesha maofisa wa polisi kutumia nguvu yenye kulingana na hali halisi na kupunguza nguvu katika hali inayodhibitiwa, maofisa hawa wanahitaji kupata mafunzo stahiki na vifaa madhubuti. Daima maofisa wa jeshi la polisi wanatakiwa kufanya kwa vitendo mbinu tofauti kwa mfano mbinu laini na ngumu za kutumia mikono mitupu.**

## 8.5. Kanuni ya Dhahabu

Kanuni ya dhahabu inaweza kufupishwa katika sentensi moja, ambayo ni **"Watendee wengine jinsi wewe ungependa utendewe."** Kanuni hii ni rahisi: Maofisa wote wa polisi, kama watu wengine, wanatamani kutendewa kwa heshima, kwa kutambulika na usawa. Kwa hiyo inamaanisha kwamba maofisa wa polisi wanatakiwa kuwatendea wengine kwa heshima, kwa kuwatambua na kwa usawa, kama wao pia wanata watendewe kwa namna hiyo.

Daima kanuni hii inatakiwa kuzingatiwa wakati wa kuchukua maamuzi. Kwa sababu kuna ukweli unaofahamika kwamba kila tendo linazaa majibizano sawa au kinzani. Hali hii pia inaonekana katika mahusiano ya mtu baina ya mtu. Mtu anayeonyesha tabia ya kirafiki dhidi ya wengine ataona watu hao pia wanajibu kwa namna ya kirafiki dhidi yake. Kinyume chake, ofisa polisi mwenye mbwembwe, asiyekuwa na urafiki na mhasimu atarajie majibizano ya uhasimu toka kwa jamii.

Matokeo ya kila ofisa polisi anayetumia Kanuni hii ya Dhahabu katika kazi yake ya kipolisi ya kila siku, kazi yake inafa na inakuwa ya kiweledi.

## 8.6. Maswali ya kujipima

- Toa mifano kwa kufafanua uwiano wakati wa kutumia nguvu.
- Nini maana ya kutumia nguvu kadiri ilivyo ndogo iwezekanavyo?
- Fafanua viwango tofauti vya kutumia nguvu vinavyoweza kutumika wakati wa kukamata, kwa kuanzia na nguvu kadiri ilivyo ndogo iwezekanavyo na kumalizia na nguvu kubwa.
- Eleza taratibu zinazotakiwa kufuatwa kabla, wakati na baada ya kutumia silaha za moto
- Ni maana ya mwendelezo na kupunguza matumizi ya nguvu?

9

# SURA YA 9

## Wajibu wa Polisi Katika Chaguzi

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya tisa.


**9.1. Utangulizi**

**9.2. Nini wajibu wa maafisa wa polisi wakati wa chaguzi?**

**9.2.1. Kabla ya uchaguzi**

**9.2.2. Siku ya uchaguzi**

**9.2.3. Baada ya uchaguzi**

**9.3. Wajibu wa mashirika na taasisi zingine**

**9.3.1. Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**9.3.2. Msajili wa Vyama vya Siasa**

**9.4. Makosa ya kuangaliwa katika kipindi cha uchaguzi**

**9.5. Muhtasari**

**9.6. Maswali ya kujipima**

> **Malengo ya mafunzo katika Sura ya 9**
>
> Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-
>
> - Kujadili wajibu wa polisi wakati wa chaguzi za kidemokrasia
> - Kueleza umuhimu wa polisi kutokuwa na upande wakati wa mchakato wa uchaguzi
> - Kujadili wajibu asilia wa Jeshi la Polisi katika jamii ya kidemokrasia
> - Kujadili wajibu wa polisi kabla ya kipindi cha uchaguzi
> - Kujadili wajibu wa maafisa wa polisi siku ya uchaguzi
> - Nini wajibu wa maafisa wa polisi baada ya siku ya uchaguzi
> - Kujadili umuhimu wa viwango vya kimataifa kwa Jeshi la Polisi la Tanzania

## 9.1. Utangulizi

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalinda Haki za Binadamu za kila mtu katika nchi hii. Hii inajumuisha haki ya kupiga kura, uhuru wa kujieleza na uhuru wa kujumuika. Chaguzi ni moja ya misingi muhimu ya demokrasia. Wananchi wote bila ubaguzi wana haki ya kuamua na kuchagua viongozi na wawakilishi wao katika vyombo mbalimbali vya serikali. Hii hufanyika kupitia kampeni za uchaguzi ambapo vyama vya siasa hunadi mipango na ajenda zao kwa wapiga kura. Kwa kupiga kura wananchi wanachagua miongoni mwa vyama vinavyoshindana viongozi kulingana na mipango na ajenda zao. Katika uchaguzi ulio huru na haki matokeo ya uchaguzi huakisi dhamira ya wapiga kura kama walivyotekeleza kupitia haki yao ya kupiga kura bila ya ubaguzi, vitisho, matusi, fujo au unyanyasaji wa kingono au kijinsia.

Maafisa wa polisi wana wajibu muhimu sana wakati wa uchaguzi. Wana jukumu muhimu la kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru na haki na bila vurugu wala vitisho na kuzingatia demokrasia.

Kwa kuongezea:-
Wajibu wa jumla wa polisi ni kama ifuatavyo:-

- Kudumisha utulivu na kuhakikisha utii wa sheria katika mchakato wote wa uchaguzi.
- Kuhakikisha usalama wa watu na mali zao katika kipindi cha kampeni na uchaguzi.
- Kuhakikisha usalama wa wasimamizi wa uchaguzi na wasaidizi wao kabla, wakati na baada ya uchaguzi.
- Kutoa ulinzi kwa wagombea wakati wa kampeni na uchaguzi.
- Kuhakikiisha kwamba kampeni zinafanyika kwa amani.
- Kuhakikisha mazingira wezeshi kwa uchaguzi ulio huru na haki, utii wa sheria na kanuni bila ubaguzi wa aina yoyote.
- Kuhakikisha usalama wa vituo vya kupigia kura.
- Kuhakikisha ulinzi na usalama wa vifaa vya kupigia kura katika vituo vya kupigia kura, wakati wa kupiga kura, wakati wa kuhesabu kura na usafirishaji wa masanduku ya kura.
- Kuhakikisha kwamba wapiga kura hawatishwi au kusumbuliwa katika vituo vya kupigia kura.

- ➢ Kuhakikisha kuwa hakuna mtu mwingine anayeruhusiwa kuwa katika eneo la kupigia kura isipokuwa wapiga kura tu. Mtu mwingine hataruhusiwa kuwepo isipokuwa kwa idhini ya Tume ya Uchaguzi.
- ➢ Kuhakikisha amani na usalama kabla, kipindi cha ucahguzi na baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

  **Kumbuka:-** Polisi wanapotekeleza majukumu haya wanatakiwa kuzingatia maadili, kuheshimu haki za binadamu na kuepuka matumizi makubwa ya nguvu yasiyokuwa ya lazima.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza polisi kuwa wanachama wa vyama vya siasa.

Haki za binadamu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zillingizwa mwaka 1984 na zinatoa haki za kidemokrasia kama vile:

- ➢ Uhuru wa kujieleza,
- ➢ Uhuru wa kuabudu na fikra,
- ➢ Uhuru wa kujumuika,
- ➢ Uhuru dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote, n.k

Katika sura hii tutajadili wajibu wa polisi katika kuhakikisha haki hizi katika kipindi cha uchaguzi.

## 9.2. Nini wajibu wa maafisa wa polisi wakati wa uchaguzi?

Maafisa wa polisi ni wawakilishi wa Serikali na siyo vyama vya siasa. Wajibu wao ni kulinda amani katika kipindi cha uchaguzi. Wajibu wao ni kusaidia kuwepo uchaguzi tulivu, huru na wa haki. Wanatakiwa pia kusaidia kulinda usalama na uadilifu katika mchakato wa uchaguzi, washiriki wote katika uchaguzi, taasisi zinazohusika na matokeo ya uchaguzi. Kuna baadhi ya miongozo kuhusu matendo ya polisi wakati wa uchaguzi, ambayo ni:

- ➢ Kuheshimu haki za binadamu za kila raia

Wakati wa kutekeleza majukumu yao, polisi wanapaswa kuheshimu na kulinda haki za binadamu za kila raia bila kujali itikadi zao za kisiasa. Kwa hiyo polisi wanapaswa kujua haki za kila raia.

- ➢ Weledi

Maafisa wa polisi wanapaswa kutimiza wajibu wao kwa weledi, na hii inajumuisha kuwa na mwonekano na haiba zinazozingatia weledi.

- ➢ Kuwa tayari

Polisi wanavyoweza kushughulikia tatizo dogo haraka iwezekanavyo ni muhimu kuzuia tatizo hilo kuwa kubwa. Kwa maana hiyo, polisi wanapaswa kuwa tayari wakati wowote katika kutambua na kushughulikia jambo lolote linaloweza kuharibu mchakato wa uchaguzi.

- ➢ Ukaribu

Maafisa wa polisi wanapaswa kuwa karibu na wananchi na kuwa tayari kusikiliza mpiga kura yoyote anayehitaji msaada.

- ➢ Kutokuwa na upande

Maafisa wa polisi wanatakiwa siyo tu kutoegemea upande wowote na kutompendelea mtu yeyote bali wanatakiwa kuonekana kutoegemea upande wowote na kutompendelea mtu yeyote. Hawapaswi kubagua mtu yoyote au kundi lolote la watu wanapotekeleza wajibu wao kwa misingi ya aina yoyote ile ya ubaguzi kama vile umri, jinsia, ulemavu, hali ya kijamii au kiuchumi, maoni ya kisiasa, kabila, dini au sababu nyingine zozote zile.

- ➢ Usawa

Kwa kawaida chaguzi huwa na mivutano ya kisiasa. Maafisa wa polisi wanapaswa kuwa waangalifu jinsi wanavyoshughulikia matukio mbalimbali hususan mivutano baina ya vyama vya siasa. Maafisa wa polisi wanapaswa kuepuka matendo yanayoweza kutafsiriwa kwamba ni ya upendeleo, yasiyozingatia usawa, uonevu na yenye shinikizo la kisiasa.

- ➢ Matumizi ya nguvu

Maafisa wa polisi wanapaswa kutotumia nguvu kubwa kupita kiasi. Nguvu inaweza kutumika pale tu ambapo ni lazima, kuna sababu za msingi za kufanya hivyo na kwa kutumia nguvu zenye uwiano na kosa. Matumizi ya nguvu kupita kiasi hususan katika kipindi cha uchaguzi na hasa siku ya kupiga kura ni jambo linaloweza kutafsiriwa vibaya.

Kuna kazi maalum kwa  polisi katika mchakato wa uchaguzi na hususan siku ya uchaguzi. Majukumu ya polisi kipindi hiki yatajadiliwa kwa undani.

### 9.2.1. Ufahamu Mzunguko/Duara la Uchaguzi

Uchaguzi ni mchakato wa kumchagua mtu au kundi la watu kwa ajili ya nafasi za kisiasa kupitia kura. Chaguzi za kitaifa Tanzania na Zanzibar zinafanyika kumchagua Rais wa Muungano, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani. Viongozi hawa huchaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano. Katika uchaguzi wa urais, mgombea anayeshinda ni yule anayepata kura nyingi zaidi. Katika uchaguzi wa wabunge na wajumbe wa baraza la wawakilishi, wagombea wanashindana katika majimbo yao, ilihali madiwani wanagombea katika kata. Mgombea anayepata kura nyingi zaidi ndiye mshindi wa uchaguzi. Kwa upande wa wabunge na madiwani kuna viti maalum vya wanawake. Wanawake wanapata nafasi hizi kulingana na uwiano wa kura za urais ambazo vyama vimepata. Kila chama cha siasa kinapaswa kuandaa orodha yenye majina ya wanawake ambao wanaweza kuteuliwa katika viti maalum.

Mzunguko wa uchaguzi maana yake ni shughuli zote zinazofanyika kuhusiana na uchaguzi. Mzunguko huu una hatua mbalimbali kuanzia uandikishaji wa wapiga kura, upigaji wa kura, uhesabuji wa kura na utangazaji wa matokeo. Hatua hizi mbalimbali ndio hujulikana kama duara la uchaguzi.  Hatua hizi hutegemeana na kwa pamoja huunda duara kamilifu. Kwa maana hiyo ni muhimu kwa maafisa wa polisi kuelewa na kufuatilia shughuli za kila hatua katika duara ili  kuhakikisha usalama.

### 9.2.2. Kabla ya uchaguzi

Kipindi cha kabla ya uchaguzi ni kipindi muhimu sana katika mchakato wowote wa uchaguzi wa kidemokrasia. Hiki ni kipindi ambapo vyama vya siasa vinapewa fursa ya kujisajili na kisha kujitangaza na kujiimarisha. Kipindi hiki huwa ni kigumu kwa upande wa polisi kwa sababu kunakuwa na msuguano kati ya vyama vya siasa au wafuasi wao. Wakati wa kampeni za uchaguzi kuna shughuli za kisiasa kama vile mikutano, mikusanyiko na maandamano ambapo polisi wanatarajiwa kudumisha amani na kuhakikisha usalama wa washiriki, wananchi wote kwa ujumla pamoja na mali zao.

Michakato ya kipindi cha kabla ya uchaguzi inaweza kuleta athari kwa usalama wa jamii. Vijana na watoto wanaweza kulazimishwa au kushawishiwa kujiunga na jumuiya/vikundi vya vijana vya vyama vya siasa. Vikundi hivi vinaweza kutumika katika kuleta fujo, na bugudha kwa wananchi wengine wakiwa katika shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Wagombea wanawake wanaweza kutukanwa, kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji na fujo ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia na kingono. Watu wenye ulemavu, wanawake na vijana wengine wanaweza kutishwa na hivyo kukata tamaa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi. Hata hivyo ikumbukwe kwamba vitendo hivi vinaweza kufanyika kwa wanaume pia.

Maafisa wa polisi ni binadamu na wakati mwingine inaweza kuwawia vigumu kutopendelea upande wowote wakati vyama vinapokuwa katika migongano. Hata hivyo maafisa wa polisi wenye weledi wanatakiwa kutoegemea upande wowote na kushughulikia migogoro katika namna ambayo itaheshimu haki za binadamu za kila mtu.

Wajibu wa polisi ni kudumisha utulivu na kuhakikisha utii wa sheria. Kipindi cha kabla ya uchaguzi jukumu kubwa la polisi ni:

- Kulinda uadilifu katika mchakato wa uchaguzi na matokeo ya uchaguzi
- Kulinda usalama wa watu na mali zao wakati wa kampeni na wakati wa kupiga kura
- Kuhakikisha usalama wa maafisa wa uchaguzi kabla, wakati na baada ya uchaguzi
- Kutoa ulinzi kwa wagombea wakati wa kampeni na wakati wa uchaguzi
- Kuhakikisha na kudumisha hali itakayoruhusu kampeni za uchaguzi kwa vyama vyote vya siasa, wagombea, wanachama wao na umma wote kwa ujumla kufanyika katika mazingira yaliyo ya haki, huru na salama na bila ubaguzi wa aina yoyote.

Hata kipindi cha uchaguzi polisi wanalazimika kutekeleza majukumu yao ya kiasili. Kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Polisi Tanzania lina majukumu yafuatayo :

- Kulinda maisha ya watu na mali zao
- Kuzuia na kugundua uhalifu unapotokea
- Kuzuia machafuko ya ndani
- Kudumisha amani,usalama na utulivu
- Kukamata wahalifu
- Kuwafikisha wahalifu mbele ya sheria, na
- Kusimamia utekelezaji wa sheria

### 9.2.3. Uandikishaji wa mpiga kura

Sheria za uchaguzi zimeanzisha mfumo wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Wasimamizi wa uchaguzi husimamia uandikishaji wa wapiga kura. Kila mwananchi mwenye sifa ya

kuandikishwa anapaswa kufika mbele ya mwandikishaji wa wapiga kura katika eneo analoishi ili kuandikishwa. Ili mtu aandikishwe anatakiwa;

- ➢ Kufika yeye mwenyewe kwenye kituo cha unadikishaji
- ➢ Kujaza fomu ya maombi
- ➢ Kujibu maswali atakayoulizwa na mwandikishaji

Mkazi wa eneo husika ambaye maombi yake yamekubaliwa ataandikishwa na kupewa kitambulisho cha kupiga kura. Maombi ya mtu ambaye hana sifa hayatakubalika.

Kwa kawaida uandikishaji wa wapiga kura/uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura hufanyika miezi mitatu kabla ya uchaguzi. Baada ya daftari la kudumu la wapiga kura kuandaliwa, majina hubandikwa katika maeneo maalum kwa ajili ya wapiga kura walioandikishwa, wagombea na vyama vya siasa kukagua. Mtu yoyote anaruhusiwa kuweka pingamizi kwa msimamizi wa uchaguzi ikiwa kuna mtu aliyeandikishwa bila kuwa na sifa.

Wakati wa uandikishaji vurugu, fujo na vitisho vinaweza kufanywa na baadhi ya watu ili kuzuia watu fulani au kundi fulani kuandikishwa na hivyo kushindwa kutumia haki yao ya kikatiba. Hili laweza kutokea kwa mtu mmoja mmoja (kwa mfano mume kumzuia mke asijiandikishe au kundi moja kuzuia kundi jingine lisijiandikishe).

### 9.2.4. Makosa Dhidi ya Uandikishwaji

Ni kosa kwa mtu yeyote:

- ➢ Kutoa maelezo ya uongo kwa makusudi ili kuandikishwa na kupata kitambulisho chake yeye mwenyewe au mtu mwingine
- ➢ Kujiandikisha mara mbili au zaidi
- ➢ Kutaka kujiandikisha kama mpiga kura wakati maombi yake katika kituo kingine yamesubirishwa kwa ajili ya uchunguzi
- ➢ Kugushi au kuharibu kitambulisho cha kupiga kura
- ➢ Kudurufu kitambulisho cha kupiga kura au kughushi alama ya kitambulisho

Endapo mtu atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu ishrini au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

### 9.2.5. Uteuzi wa wagombea

Kuna hatua mbili za uteuzi yaani;

- ➢ Uteuzi ndani ya chama
- ➢ Uteuzi wa Tume ya Uchaguzi
- ➢ **Uteuzi wa chama**

Kila chama cha siasa kina wajibu wa kuteua wagombea wake. Chama kitapaswa kuwasilisha jina moja moja la mgombea aliyeteuliwa na chama kwa Tume ya Uchaguzi kugombea nafasi ya urais, ubunge au udiwani. Kila chama kina uhuru wa kufanya uteuzi wa wagombea wake pasipo kuingiliwa na Tume ya Uchaguzi

- ➢ **Uteuzi wa Tume**

Uteuzi wa Tume utafanyika kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi na pia kutokana na maelekezo

yatayotolewa na Tume ya Uchaguzi. Ili mtu aweze kuteuliwa kuwa mgombea anapaswa kuwa na sifa na kutimiza masharti yafuatayo:-

Mgombea wa urais na makamu wake:-

- Awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Awe na umri wa miaka arobaini au zaidi
- Awe mwanachama wa chama cha siasa na kuteuliwa na chama hicho
- Awe na sifa za kuwa mbunge au mjumbe wa Baraza la Wawakilishi
- Asiwe amepatikana na hatia na mahakama yoyote kwa kosa la kukwepa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi
- Anapaswa kuungwa mkono/kudhaminiwa kwa maandishi na wapiga kura wasiopungua 200 kutoka angalau mikoa kumi, na kati ya mikoa hiyo miwili iwe ya Zanzibar
- Alipe ada ya Shilingi 1,000,000/=
- Awasilishe fomu za uteuzi zilizojazwa kikamilifu kabla ya saa kumi jioni ya siku ya uteuzi iliyowekwa na Tume ya Uchaguzi. Fomu ya uteuzi inapaswa kuonyesha:

    - Jina, anuani na kazi ya mgombea
    - Majina na anuani za wadhamini
    - Namba za vitambulisho vya kupiga kura vya wadhamini
    - Uthibitisho wa mgombea kwamba yuko tayari na ana sifa za kugombea
    - Picha nne za paspoti.

Baada ya Tume ya Uchaguzi kupokea fomu za wagombea itazibandika katika eneo lililo wazi ili kuwezesha wagombea wengine waweze kuona na kuhakiki usahihi wa taarifa na kama kuna pingamizi waweze kufanya hivyo.

- **Mgombea wa Ubunge**

Mtu anayetaka kugombea nafasi ya ubunge lazima awe na sifa na kutimiza masharti yafuatayo:

- Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Awe na ummri wa miaka 21 au zaidi
- Awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza
- Awe mwanachama wa chama cha siasa na kuteuliwa na chama hicho
- Asiwe ametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa la kukwepa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi
- Awe amedhaminiwa kwa maandishi na wapiga kura wasipongua 25 katika jimbo analogombea
- Awasilishe fomu za uteuzi kwa Afisa Msimamizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi jioni ya siku ya uteuzi iliyowekwa na Tume. Fomu ya uteuzi inapaswa kuonyesha:

    - Jina, anuani na kazi ya mgombea
    - Majina, anuani na namba za vitambulisho vya kupiga kura vya wadhamini
    - Uthibitisho wa mgombea kwamba yuko tayari na ana sifa za kugombea
    - Picha nne za paspoti
    - Na malipo ya ada ya shilingi 50,000/=

Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kupokea fomu za wagombea atazibandika katika eneo lililo

wazi ili kuwezesha wagombea wengine waweze kuona na kuhakiki usahihi wa taarifa na kama wana pingamizi waweze kufanya hivyo.

- **Mgombea wa Udiwani**

Mtu anayetaka kugombea nafasi ya udiwani anapaswa kuwa na sifa na kutimiza masharti yafuatayo:

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na umri wa miaka 21 au zaidi
- Awe anaishi eneo analotaka kugombea
- Awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza
- Awe mwanachama wa chama cha siasa na kuteuliwa na chama hicho
- Awe na njia halali za kujipatia kipato
- Asiwe ametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa la kukwepa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi
- Awe amedhaminiwa kwa maandishi na wapiga kura wasipongua 10 katika kata anayogombea
- Awasilishe fomu za uteuzi kwa Afisa Msimamizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi jioni ya siku ya uteuzi iliyowekwa na Tume. Fomu ya uteuzi inapaswa kuonyesha:

    - Jina, anuani na kazi ya mgombea
    - Majina, anuani na namba za vitambulisho vya kupiga kura vya wadhamini
    - Uthibitisho wa mgombea kwamba yuko tayari na ana sifa za kugombea
    - Picha nne za paspoti
    - Na malipo ya ada ya shilingi 5,000/=

Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kupokea fomu za wagombea atazibandika katika eneo lililo wazi ili kuwezesha wagombea wengine waweze kuona na kuhakiki usahihi wa taarifa na kama wana pingamizi waweze kufanya hivyo.

- **Makosa na adhabu zinazohusiana na Uteuzi**

Yafuatayo ni makosa yanayohusiana na uteuzi:

- Kughushi au kuharibu fomu ya uteuzi
- Kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi fomu za uteuzi zilizoghushiwa
- Kuteua, hali akijua, mgombea zaidi ya mmoja katika nafasi ya urais, ubunge au udiwani
- Kutoa tamko au kufanya kitu chochote kwa nia ya kukatisha tamaa mtu yoyote anayetaka kuteuliwa au kushawishi mtu aliyeteuliwa kujitoa, wakati mtu huyo anayeshawishi akiwa ni mtumishi wa umma.

Endapo mtu huyo atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi 20,000/= au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Makosa mengine ni:

- Mtu yeyote hali akijua akitamka, kuchapisha, kutangaza na kusambaza taarifa yoyote kwamba mgombea fulani kajitoa kugombea kwa nia ya kumsaidia mgombea mwingine.

Endapo atapatikana na hatia atafungwa kifungo kisichozidi miaka miwili.

- Mtu yeyote akitoa rushwa au akiahidi kutoa rushwa ili kumshawishi mtu mwingine kujitoa kama mgombea katika uchaguzi, na mtu yeyote atakayejitoa baada ya ushawishi huo atakuwa anatenda kosa la rushwa na endapo atapatikana na hatia atafungwa kifungo kisichozidi miaka mitano.
- Mtu yeyote hali akijua akatoa kauli ya uongo katika fomu ya kugombea au uthibitisho unaotolewa kwa msimamizi wa uchaguzi atakuwa anatenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi 10,000/= au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.

## 9.2.6. Kampeni za Uchaguzi

Kampeni za uchaguzi huandaliwa na mgombea, chama chake cha siasa au mawakala. Wataandaa ratiba ya kampeni na kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi. Baada ya kupokea ratiba, Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha mkutano na wagombea wote, vyama vyao au mawakala ili kupanga ratiba za wagombea na hivyo kuepusha migongano. Baada ya mkutano, Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba iliyokubaliwa kwa mkuu wa polisi wa wilaya ambapo jimbo la uchaguzi lipo ili kupanga ulinzi. Ratiba iliyokubaliwa itatumika kama notisi ya mikutano ya kampeni.

- **Mbinu za kampeni**
- Mikutano ya kampeni
- Kampeni za mlango kwa mlango
- Kampeni kupitia vyombo vya habari. Vyama vyote vya siasa vina haki sawa katika kutumia vyombo vya habari vya umma
- Kutumia mabango, fulana na machapisho.

Kampeni haziruhusiwi siku ya uchaguzi

- **Makosa na adhabu**
- Kuuza au kutangaza kutaka kuuza kitambulisho cha kupiga kura
- Kununua au kutangaza kutaka kununua kitambulisho cha kupiga kura
- Kutoa rushwa kwa wapiga kura ili wamchague mgombea fulani
- Kupokea rushwa ili kumchagua mgombea fulani
- Kuficha kitambulisho cha kupiga kura cha mtu mwingine
- Kutumia rasilimali za umma kwa ajili ya kampeni za mgombea fulani

## 9.2.7. Siku ya Uchaguzi

Wajibu wa msingi wa polisi siku ya uchaguzi ni kutimiza wajibu wao wa kiasilia wa kuhakikisha kuwa amani, utulivu na utii wa sheria unakuwepo. Zaidi ya wajibu wao wa kawaida wanatarajiwa kusaidia kuhakikisha kwamba uchaguzi unaendeshwa kwa utulivu. Kunatakiwa kuwe na ushirikiano mzuri baina ya Jeshi la Polisi na vyama vyote vya siasa ili kuhakikisha upigaji kura unakuwa wa amani na utulivu na wapiga kura wanakuwa huru ili waweze kutumia haki yao bila bughudha au kuzuiliwa. Kwa maana hiyo, kazi ambazo zinapaswa kufanywa na polisi siku ya uchaguzi ni:

- Kutoa ulinzi kwa maafisa wa uchaguzi katika vituo vya upigaji kura
- Kudumisha hali ya amani, utulivu na utii wa sheria katika vituo vya kupigia kura
- Kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote isipokuwa mpiga kura anayeingia katika kituo cha kupigia kura bila idhini ya Tume

- ➢ Kuhakikisha kwamba wapiga kura wanapiga kura kwa uhuru bila vikwazo ikijumuisha kutobaguliwa, kutukanwa, kushambuliwa, kunyanyaswa ikiwemo unayanyasaji wa kingono na kijinsia. Ifahamike kuwa baadhi ya wananchi kama vile watu wenye ulemavu, wazee na wajawazito wanapaswa kupewa upendeleo wakati wa kupiga kura ili kuepuka kusimama katika mistari mirefu na wakati wa jua
- ➢ Kuhakikisha kwamba hakuna mtu anatishwa wala kubughudhiwa wakati wa kupiga kura
- ➢ Kuhakikisha kwamba wapiga kura wanaingia na kutoka kwa uhuru katika kituo cha kupigia kura
- ➢ Kusaidia kushughulikia watu wanaoleta fujo katika kituo cha kupigia kura
- ➢ Kuhakikisha kwamba kunakuwa na usalama wa vifaa vya kupigia kura, eneo la kuhesabu kura na wakati wa kusafirisha vifaa vya kupigia kura
- ➢ Kusindikiza masanduku ya kupigia kura kwenda na kutoka katika vituo vya kupigia kura
- ➢ Kuhakikisha kwamba vifaa vya kupigia kura haviibwi, kutekwa, kuharibiwa au kugushiwa na mtu yeyote au kundi lolote.

Wanapofanya kazi katika vituo vya kupigia kura polisi wanapaswa:-

- ➢ Kutokuwa na upande wala kubagua mtu yeyote
- ➢ Kutambua kwamba hawapaswi kutumikia utawala fulani au chama fulani bali wao ni taasisi ya kitaifa na wanawakilish maslahi ya nchi.
- ➢ Kutambua kwamba wanavyofanya kazi katika vituo vya kupigia kura wanapaswa kuwa marafiki, kutoingilia majukumu yasiyokuwa ya kwao na kutenda kazi kwa weledi.
- ➢ **Uchaguzi na taratibu za upigaji kura**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na wasimamizi wa uchaguzi watapanga idadi na maeneo ya kupigia kura. Kwa kawaida vituo vya kupigia kura huwa ni majengo ya umma kama vile shule, ofisi za umma, zahanati, vituo vya afya, majengo ya mahakama na kumbi mbalimbali ambazo zinaweza kufikiwa kwa urahisi na wapiga kura.

Watu wafuatao wataruhusiwa katika kituo cha kupigia kura:
- ➢ Mkurugenzi wa Uchaguzi
- ➢ Kamishna wa Tume
- ➢ Msimamizi wa uchaguzi
- ➢ Msimamizi msaidizi wa uchaguzi
- ➢ Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura
- ➢ Msaidizi wa Afisa wa kituo cha kupigia kura
- ➢ Maafisa wa polisi
- ➢ Maafisa wengine wa vituo vya kupiga kura
- ➢ Mawakala wa vyama vya siasa
- ➢ Waangalizi wa kimataifa
- ➢ Waangalizi wa ndani
- ➢ Mpiga kura
- ➢ Mgombea
- ➢ Mtu anayemsaidia mpiga kura mwenye kuhitaji msaada.

Maafisa wote waliopo katika kituo cha kupigia kura ni lazima waruhusiwe kuwa hapo na Tume ya Uchaguzi. Tume huwapa vitambulisho vikionesha majukumu yao katika kituo.

- **Upigaji kura**

Upigaji kura huanza saa moja asubuhi na kuisha saa kumi jioni. Wapiga kura wanatarajiwa kupiga kura katika vituo walivyojiandikisha. Upigaji wa kura huwa ni wa siri. Kituo cha kupigia kura hakipaswi kuwa na alama zozote za kampeni. Kama kuna mabango ya wagombea au alama za kampeni vinapaswa kuondolewa kabla ya upigaji kura kuanza.

Kabla ya kuanza kupiga kura, vifaa vyote vya kupigia kura vinapaswa kukaguliwa na Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura mbele ya maafisa wote wanaosimamia uchaguzi, polisi, mawakala na waangalizi. Afisa anayesimami uchaguzi lazima aoneshe masanduku ya kura yakiwa wazi kuonesha kuwa hakuna kitu chochote. Baada ya hapo afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura sharti afunge masanduku ya kupigia kura kwa lakiri (seal). Masanduku ya kupigia kura hupaswa kuweka katikati ya chumba cha kupigia kura ambapo kila mtu aweza kuyaona.

Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura anapofungua kituo, upigaji wa kura huanza. Mpiga kura anapaswa kufika katika kituo cha kupigia kura yeye mwenyewe. Anapaswa kuwa na kitambulisho cha kupiga kura. Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura lazima ahakikishe kuwa watu wanaokuja kupiga kura ni wapiga kura halali na hawajapiga kura sehemu nyingine. Endapo afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura anaridhika, atampatia mpiga kura karatasi za kupiga kura. Mpiga kura mwenye kuhitaji msaada anaweza kuchagua mtu wa kumsaidia wakati wa kupiga kura. Baada ya kupiga kura mpiga kura anapaswa kuchovya kidole chake kidogo cha mkono wa kushoto katika wino usiofutika kirahisi. Wino huu hauwezi kufutika kwa maji na hutumika kama alama kuwa mtu amekwisha kupiga kura.

Kituo cha kupigia kura hufungwa saa kumi jioni. Hata hivyo ikiwa kuna watu waliosimama katika mstari afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura atawaruhusu kupiga kura. Na afisa wa polisi anayelinda kituo cha kupigia kura atasimama nyuma ya mtu wa mwisho katika mstari.

- **Mwisho wa Upigaji kura**

Mara baada ya upigaji kura kumalizika, afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura atafunga masanduku ya kupigia kura mbele ya maafisa wa uchaguzi, polisi, mawakala na waangalizi. Mawakala waliopo wanaweza kutoa mtazamo wao kuhusiana na namna ambavyo upigaji kura umeendeshwa katika kituo cha kupigia kura. Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura ataandaa ripoti.

- **Makosa ya Upigaji kura**

Ni kosa kwa mtu yeyote:

- Kugushi au kuharibu karatasi ya kupiga kura au alama maalum katika karatasi ya kupiga kura
- Kwa msimamizi wa uchaguzi au afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura kuacha kwa uzembe au kwa makusudi kuweka alama ya muhuri katika karatasi za kupiga kura
- Kumpa karatasi ya kupiga kura mtu yeyote pasipokuwa na mamlaka ya kufanya hivyo
- Kuweka kwa udanganyifu katika sanduku la kupigia kura karatasi yoyote mbali na zile karatasi rasmi za kupiga kura
- Kuondoa karatasi yoyote ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura pasipo kuwa na mamlaka

- Kuharibu, kuchukua au kufungua masandaku ya kupigia kura bila kuwa na mamlaka. Na endapo mtu atapatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 20,000/= au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja
- Kutoa ushahidi wa uwongo au kutoa maelezo ya uongo katika tamko la kuthibitisha kwamba ni mpiga kura. Endapo mtu atapatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 10,000/= au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja
- Kutoa siri kinyume cha kiapo cha kutunza siri. Endapo mtu atapatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 20,000/= au kifungo kisichozidi miaka minne au vyote kwa pamoja
- Kupiga kura au kujaribu kupiga kura zaidi ya mara moja au kushawishi mtu mwingine kupiga kura zaidi ya mara moja. Endapo mtu atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 500, 000/= au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja
- Kumpa mtu mwingine kitambulsiho cha kupigia kura ili aweze kupiga kura. Endapo atapatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi 500,000/= au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

- **Kuhesabu kura**

Jambo la muhimu baada ya kupiga kura ni kuhesabu kura. Kwa mujibu wa sheria, kura huhesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Polisi wana wajibu muhimu kuhakikisha usalama wa watu wanaohesabu kura na kulinda eneo hilo.

Kabla ya kuanza kuhesabu kura, Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura mbele ya mawakala na watu wengine wanaoruhusiwa kuwepo anapaswa kuhakikisha na kurekodi kura zote zilizopigwa, karatasi za kura ambazo hazijatumika, kukagua lakiri katika masanduku na kuhakikisha kwamba hayajafunguliwa. Baada ya hapo, anapaswa kukata lakiri na kuyafungua. Msimamizi wa kituo cha kupigia kura ataanza kuhesabu idadi ya karatasi za kura zilizopo katika kila sanduku bila kufungua karatasi hizo na kisha atarekodi idadai yake. Msimamizi wa kituo cha kupigia kura au msaidizi wake atafungua kila karatasi ya kupigia kura, ataionesha na kusoma mgombea aliyechaguliwa na kisha kuweka kwa mgombea aliyepata kura hiyo.
Karatasi ya kupigia kura haitakuwa halali ikiwa;

- Haina alama rasmi
- Kuna chochote kilichoandikwa au kutiwa alama inayoonyesha utambulisho wa mpigakura
- Haijatiwa alama yoyote
- Imetiwa alama katika namna ambayo chaguo la mpiga kura halipo dhahiri.

Baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika, Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura atarekodi matokeo. Kura zilizo halali, kura zinazobishaniwa na kura zilizoharibika na zitawekwa katika bahasha tofauti na ripoti kuhusiana na kura hizo za urais, ubunge au udiwani zitaandaliwa. Watu walioruhusiwa kuwepo katika kituo wanaruhusiwa kutoa malalamiko yao au kuthibitisha taarifa katika fomu maalum. Kila wakala hupewa ripoti. Afisa anayesimamia kituo cha kupigia kura huifunga ripoti yake katika bahasha na kuweka lakiri na kuipeleka kwa Msimamizi wa Uchaguzi pamoja na vifaa vyote vya kupigia kura kutoka katika kituo cha kupigia kura.

- **Ujumlishaji wa kura na utangazaji wa matokeo**

Ujumlishaji wa kura huwa katika ngazi tatu:

- Ngazi ya kata kwa ajili ya wagombea wa udiwani
- Ngazi ya jimbo kwa ajili ya wagombea wa Ubunge

- ➢ Ngazi ya Taifa kwa ajili ya ujumlishaji wa matokeo ya Urais

Kabla ya zoezi la ujumlishaji kuanza, msimamizi wa uchaguzi au msaidizi wake atashughulikia malalamiko yaliyotolewa na baada ya hapo zoezi la ujumlishaji wa matokeo kutoka kila kituo cha kupigia kura katika jimbo hilo litafanyika. Kama kuna sababu za msingi, msimamizi wa uchaguzi au msaidizi wake anaweza kuthibitisha kura zilizopigwa kwa kuhesabu tena au kujumlisha vizuri matokeo ya kituo kinacholalamikiwa. Baada ya ujumlishaji wa matokeo yote endapo wagombea watapata kura zinazolingana Msimamizi wa Uchaguzi atatoa taarifa kwa Tume ya Uchaguzi ili uchaguzi wa marudio uweze kufanyika ndani ya siku thelathini. Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo ya mgombea wa ubunge aliyeshinda katika jimbo husika na atapeleka ripoti na matokeo ya ubunge pamoja na matokeo ya urais ya jimbo hilo kwa Tume ya Uchaguzi. Tume nayo baada ya kupokea matokeo kutoka majimboni itajumlisha, kuhakiki na hatimaye kutangaza mgombea wa urais aliyeshinda.

### 9.2.8. Baada ya Uchaguzi

Kipindi kinachofuata baada ya kupiga kura, matokeo kutangazwa na rais kuapishwa ni kipindi muhimu sana katika mchakato wa kidemokrasia. Katika kipindi hiki maafisa wa polisi wanapaswa kuendelea kulinda amani na kuhakikisha utii wa sheria.

Katika kipindi hiki pia vurugu yaweza kutokea na kama ilivyo katika hatua za awali baadhi ya makundi yanaweza kuathirika kutokana na vurugu. Makundi haya yaweza kuwa ya wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo polisi wanapaswa kuwa macho na kutoa ulinzi wa kutosha katika kipindi hiki.

## 9.3. Wajibu wa mashirika na taasisi nyingine

Kuna wahusika mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi. Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Taasisi za Kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa, Asasi zisizokuwa za kiserikali za kitaifa na kimataifa, zote zina wajibu fulani katika kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Kwa hiyo basi, ni muhimu kwa polisi kuwa na uhusiano mzuri na wadau wote katika mchakato wa uchaguzi.

### 9.3.1. Vyombo vya Uchaguzi

Kuna vyombo viwili vinavyosimamia uchaguzi hapa nchini:

- ➢ Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo husimamia uchaguzi wa Muungano na wa Tanzania Bara. na
- ➢ Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ambayo husimamia uchaguzi wa Zanzibar.

Majukumu ya Tume ni kama ifuatavyo:

- ➢ Kusimamia chaguzi za kitaifa
- ➢ Kusimamia uandikishaji wa wapiga kura
- ➢ Kutunza na kuboresha daftari la wapiga kura
- ➢ Kupanga na kuamua idadi ya majimbo ya uchaguzi
- ➢ Kutoa elimu ya mpiga kura
- ➢ Kusimamia ratiba ya uchaguzi

### 9.3.2. Msajili wa vyama vya siasa

Msajili wa Vyama vya Siasa naye husimamia mchakato wa uchaguzi. Kwanza, hakuna chama kinachoruhusiwa kushiriki katika uchaguzi kama hakijapata usajili wa kudumu. Pili, Msajili wa Vyama vya Siasa husimamia Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

### 9.3.3. Mashirika ya Kimataifa

Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi zinaruhusiwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchaguzi na kuwa waangalizi katika uchaguzi. Taasisi hizi zaweza kuwa asasi zisizokuwa za kiserikali, wawakilishi kutoka nchi mbalimbali, jumuiya za kimataifa na kikanda kama vile Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola na Umoja wa Afrika. Wajumbe wanaowakilisha taasisi hizo wanapaswa kupewa utambulisho maalum kutoka Tume ya Uchaguzi na wakati wote wanapaswa kubeba vitambulisho vyao.

## 9.4. Muhtasari

Kuna makosa yanayohusiana na uchaguzi ambayo maafisa wa polisi wanapaswa kuyaangalia. Makosa hayo ni kama vile:

- Kugushi au kuharibu karatasi ya kupigia kura au alama maalum katika karatasi ya kupigia kura
- Kwa msimamizi wa uchaguzi au afisa anayesimamia kituo cha kupigia kuacha kwa uzembe au kwa makusudi kuweka alama ya muhuri katika karatasi za kupigia kura
- Kumpa karatasi ya kupigia kura mtu yeyote pasipo kuwa na mamlaka ya kufanya hivyo
- Kuweka kwa udanganyifu katika sanduku la kupigia kura karatasi yoyote mbali na zile karatasi rasmi za kupiga kura
- Kuondoa karatasi yoyote ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura pasipo kuwa na mamlaka
- Kuuza au kutangaza kutaka kuuza kitambulisho cha kupiga kura
- Kununua au kutangaza kutaka kununua kitambulisho cha kupiga kura
- Kutoa rushwa kwa wapiga kura ili wamchague mgombea fulani
- Kupokea rushwa ili kumchagua mgombea fulani
- Kuficha kitambulisho cha kupiga kura cha mtu mwingine
- Kutumia rasilimali za umma kwa ajili ya kampeni za mgombea fulani.

## 9.5 Maswali ya kujipima

- Nini wajibu wa maafisa wa polisi katika uchaguzi wa kidemorasia?
- Kwa nini ni muhimu kwa maafisa wa polisi kutoegemea upande wowote katika mchakato wa uchaguzi?
- Nini wajibu wa asili wa polisi katika jamii ya kidemokrasia?
- Je, polisi wana wajibu ya ziada kabla ya siku ya uchaguzi? Jadili.
- Nini wajibu wa maafisa wa polisi siku ya uchaguzi?
- Nini wajibu wa maafisa wa polisi baada ya siku ya uchaguzi?
- Je, polisi wanawakilisha chama chochote cha siasa?
- Je, kuna aina gani ya mahitaji maalum ambayo yaweza kujitokeza katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi zinazotokana na umri, jinsi, ulemavu, kabila,dini, maoni ya kisiasa, hali ya kijamii au kiuchumi, au sababu nyingine zozote zile?

# 10 SURA YA 10

## Ukiukwaji wa Haki za Binadamu

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya kumi.

**10.1. Utangulizi**

**10.2. Maana ya Ukiukwaji wa haki za binadamu**

**10.3. Wajibu na jukumu la Serikali katika kulinda haki za binadamu**

**10.4. Taratibu za kutoa malalamiko na nafuu za kisheria zinazoweza kupatikana pindi haki za binadamu zinapokiukwa**

**10.5. Waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu**

**10.6. Nani ni waangalizi wa haki za binadamu?**

**10.7. Viwango vya Umoja wa Mataifa na hatua zinazochukuliwa endapo polisi wanakiuka haki za binadamu**

**10.8. Matokeo ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi**

**10.9. Muhtasari**

**10.10. Maswali ya kujipima**

**Malengo ya mafunzo katika Sura ya 10**

Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-

- Kueleza nini maana ya ukiukwaji wa haki za binadamu
- Kujadili matokeo ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na polisi
- Kutoa mifano ya ukiukwaji wa haki za binadamu
- Kueleza wajibu na jukumu la serikali katika kulinda haki za binadamu
- Kujadili kinachoweza kutokea endapo wasimamizi wa sheria wanapokiuka haki za binadamu
- Kueleza haki za waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu
- Kujadili nini maana ya utesaji
- Kujadili matokeo ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi

## 10.1. Utangulizi

Maafisa wa polisi wana jukumu la kuwatumikia na kuwalinda wananchi. Wanapaswa kusimamia na kutekeleza sheria. Hii pia ina maana kwamba wanapaswa kutekeleza majukumu yao kama maafisa wa polisi kwa nidhamu na kwa weledi, wakiheshimu, kulinda na kukuza haki za binadamu. Wakati mwingine maafisa wa polisi wanakuwa na wakati mgumu wanapofanya kazi zao. Kwa upande mmoja wanapaswa kuwa imara katika kuzuia makosa ya jinai na wahalifu na kwa upande mwingine wanategemewa kuheshimu na kulinda haki za binadamu za watuhumiwa. Wakati wa uchaguzi, vyama mbalimbali vya siasa vinatarajia kupata uangalizi maalum na upendeleo kutoka kwa polisi. Kwa hiyo wakati mwingine polisi wanakuwa katika mazingira magumu hususan wanapokuwa hawajapata mafunzo ya kutosha au kuwa na uelewa wa kutosha wa namna ya kuzingatia haki za binadamu katika kazi zao. Kwa maana hiyo, mara kwa mara polisi hukiuka haki za binadamu katika kazi zao. Vitendo hivi huchukuliwa kama ukiukwaji mkubwa wa maadili na vinapaswa kushughulikiwa kwa ukali. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaoweza kufanywa na maafisa wa polisi:

- Mauaji ya kimbari;
- Kutoweshwa (Enforced or Involuntary Dissappearance);
- Mauaji kinyume cha sheria (Extra legal/arbitrary/summary executions)
- Kukamata na kutia kizuizini mtu/watu kinyume cha sheria;
- Matumizi makubwa ya nguvu;
- Utesaji;
- Vitendo vya kutweza na vya kinyama dhidi ya watu waliokamatwa na kutiwa kizuizini;
- Ubaguzi;
- Upekuzi na ukamataji kinyume cha sheria na taratibu;
- Kutumia mbinu za upelelezi kinyume cha sheria;
- Adhabu ya viboko kinyume cha sheria;
- Vitendo vya kutweza kwa waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu;
- Kufanya vitendo vya kuzuia haki kutendeka (mfano, kulinda wahalifu)
- Aina mbalimbali za udhalilishaji wa kingono na kijinsia.

Katika sehemu ya sura hii ukiukwaji wa haki za binadamu utajadiliwa kwa undani.

## 10.2. Maana ya ukiukwaji wa haki za binadamu

Ukiukwaji wa haki za binadamu unaweza kutafsiriwa kama ukiukwaji wa sheria za jinai za kitaifa au viwango/misingi vya sheria za kimataifa kuhusiana na haki za binadamu ambayo bado haijaingizwa katika sheria za nchi.

Kimsingi, kuna njia mbili za kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa upande wa muathirika, Tamko la Kanuni za Msingi za Haki za Waathirika wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Madaraka linapendekeza tafsiri mbili kuhusu vitendo vya ukiukwaji. Tafsiri ya kwanza inasema vitendo hivyo ni "ukiukwaji wa sheria za jinai zinazotumika katika nchi husika zikiwemo sheria zinazotamka makosa ya jinai yanayotokana na matumzi mabaya ya madaraka. Kitovu cha ukiukwaji huo ni mateso au madhara kwa mtu mmoja mmoja au watu wengi, yakijumuisha madhara ya kimwili na kiakili, maumivu ya hisia, hasara za kiuchumi au ukiukwaji mkubwa wa haki za msingi kupitia vitendo vinavyofanywa au vilivyoachwa kufanywa ambavyo vinaweza kunasibishwa na serikali". Tafsiri ya pili inahusu "vitendo au kutokutenda [kunakonasibishwa na serikali] ambako hakusababishi ukiukwaji wa sheria za jinai za nchi husika lakini husababisha ukiukwaji wa sheria za kimataifa za haki za binadamu."

## 10.3. Wajibu na Jukumu la Serikali katika kulinda haki za binadamu

Sheria za kimataifa za haki za binadamu zimeweka wajibu wa kisheria kwa nchi. Wajibu huu unajumuisha sharti la kuwa na sheria za nchi zinazoendana na sheria za kimataifa, na pia kuzuia vitendo vinavyokinzana na sheria hizi. Tunapozungumzia nchi/serikali inajumuisha watu wote wanaofanya kazi kwa niaba ya nchi/serikali wakiwemo maafisa wa polisi. Serikali inawajibika kwa vitendo vya afisa mmoja mmoja wa serikali.

Taratibu za kimataifa za malalamiko na utaratibu ambao nchi/serikali zinaweza kuwajibika kwa ukiukaji wa haki za binadamu unapatikana katika vyanzo mbalimbali vya sheria ikiwemo maamuzi ya mahakama za kimataifa na kikanda, maazimio ya Baraza la Umoja wa Mataifa na kwa kupitia mikataba mahususi ya kimataifa.
Mkazo katika sura hii utakuwa katika wajibu wa nchi na serikali na taratibu za malalamiko.

Kuna wajibu wa kila afisa wa usimamizi wa sheria (law enforcer) akiwa mwakilishi wa serikali kuheshimu, kulinda na kukuza haki za binadamu za kila mtu. Kila serikali/nchi ina wajibu na jukumu la kulinda haki za binadamu za kila mtu, bila kujali umri, jinsi, ulemavu, hali ya kijamii na kiuchumi, maoni ya kisiasa au kabila na dini au hali nyingine zozote na bila ubaguzi kati ya watu mbalimbali. Baadhi ya mambo yanavyoweza kusaidia nchi au serikali kutekeleza wajibu na majukumu haya ni:

- ➢ Kuhakikisha kwamba kila afisa wa polisi anapata mafunzo na kuelimishwa katika kuzingatia haki za binadamu katika utendaji wa kazi zake za kila siku.
- ➢ Kuweka mifumo ya kufuatilia na kutathmini vitendo vya polisi na kuhakikisha kwamba vinazingatia haki za binadamu.
- ➢ Kuunda vyombo na mifumo ya kushughulikia malalamiko, kwa mfano kitengo cha ndani cha nidhamu na kushughulikia malalamiko, mfumo wa nje wa malalamiko, kama vile Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu, Mchunguzi maalum (Ombudsman) au taasisi

nyingine zinazofanana na hizi.
- Kuweka mfumo mzuri wa utaratibu wa malalamiko, na
- Kuanzisha/kuunda vyombo vya kuchunguza malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kutokana na ukweli kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu ni vitendo vinavyofanywa au kuachwa kufanywa vinavyosababisha uvunjifu wa sheria za jinai zinazotumika katika nchi husika au sheria za kimataifa za haki za binadamu, serikali/nchi zinawajibika kuweka muundo wa kimahakama kudhibiti vitendo hivyo na kulinda waathirika. Kunapokuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu ambao pia ni ukiukaji wa sheria za jinai, udhibiti kwa kutumia mahakama hutamkwa katika sheria za nchi. Hata hivyo madhumuni ya sheria za jinai ni namna ya kumshughulikia mkosaji kuliko mwathirika wa makosa hayo. Suala la fidia kwa waathirika mara nyingi huwa ni jambo linaloshughulikiwa katika kesi za madai. Pale ambapo sheria za kimataifa kuhusu haki za binadamu hazijaingizwa katika sheria za nchi husika, mahakama za nchi hizo zinapaswa kuzingatia sheria hizo hususan kama sheria hizo ni sehemu ya sheria za kimila za kimataifa (Customary International Law), au ikiwa sheria hizo ziko katika mkataba ulioridhiwa na nchi husika.

## 10.4. Matokeo ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi

Ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi unafanya kazi ya usimamizi wa sheria kuwa ngumu zaidi. Ni lazima kukumbuka kwamba msimamizi wa sheria anapokuwa ndio mvunjaji wa sheria, matokeo yake sio tu kuwa utu wa binadamu unakiukwa na sheria kuvunjwa bali pia unasababisha vikwazo katika utendaji bora wa kazi za polisi.

Athari za ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi ni kama ifuatavyo:
- Unaondoa taratibu imani ya wananchi juu ya jeshi la polisi;
- Aghalabu husababisha machafuko;
- Hutenganisha jeshi la polisi na jamii;
- Huweka vikwazo katika uendeshaji bora wa mashitaka;
- Husababisha watu wasio na hatia kuadhibiwa na watu wenye hatia kuachiwa;
- Husababisha waathirika wa makosa ya jinai kukosa haki na kupata mateso;
- Husababisha maafisa wa polisi kuwa walazimishaji badala ya kuwa wasimamizi wa sheria;
- Husababisha polisi kushindwa kuzuia makosa na badala yake kulazimika kuchukua hatua pindi makosa yanapokuwa yameshatendeka;
- Huweza kuharibu sifa nzuri ya nchi/serikali; na
- Husababisha Serikali kuwajibika katika mifumo ya kimataifa ya haki za binadamu, kama vile UN Special Rapporteur on Torture, Mahakama za Haki za Bindamu au Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika.

Tofauti na ilivyoelezwa hapo juu, polisi wanapoheshimu haki za binadamu huboresha utendaji kazi wa polisi. Kwa mantiki hiyo, polisi wanapoheshimu haki za binadamu zaidi ya kuwa ni wajibu wa kisheria na kimaadili, pia husaidia katika utendaji bora wa kazi. Pindi maafisa wa polisi wanapoonekana kuheshimu, kukuza na kulinda haki za binadamu yafuatayo hutokea :

- Imani juu ya Jeshi la Polisi inaongezeka na ushirikiano wa jamii kwa polisi huongezeka pia;

- Kuongezeka kwa usuluhishi wa migogoro na malalamiko kwa njia ya amani;
- Mashitaka dhidi ya wahalifu hufanikiwa;
- Maafisa wa polisi wanaoneka kuwa sehemu ya jamii, wakifanya kazi muhimu ya jamii;
- Haki hutendeka kwa usawa na matokeo yake imani ya wananchi hujengeka juu ya mifumo iliyopo;
- Hii huchochea watu wengine katika jamii kuheshimu sheria;
- Polisi wanakuwa karibu na jamii na kwa maana hiyo wanaweza kuzuia uhalifu vizuri zaidi;
- Vyombo vya habari huanza kuunga mkono polisi na polisi pia huungwa mkono na wanasiasa na jumuiya za kimataifa.

Maafisa wa polisi wanaoheshimu haki za binadamu hupata matokeo bora kutokana na utendaji wenye ufanisi, wakati huo huo mifumo ya usimamizi wa sheria hujengwa bila kutegemea matumizi ya nguvu na hofu bali ikitegemea heshima, weledi na utendaji unaoheshimu sheria.

## 10.5. Taratibu za kutoa malalamiko na nafuu za kisheria zinazoweza kupatikana pindi haki za binadamu zinapokiukwa

Ni jambo la muhimu kwa serikali kuwa na taratibu za kupokea malalamiko na kutoa nafuu za kisheria kwa watu ambao haki zao za binadamu zinakiukwa. Ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa usimamizi wa sheria unaharibu sifa ya taasisi nzima ya usimamizi wa sheria na unaweza kutoa taswira mbaya ya serikali. Serikali zinatakiwa kutambua kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu hutokea na unaweza kuendelea kutokea. Ukiukwaji huo waweza kuzuilika na kama inakuwa vigumu kuzuilika serikali inapaswa kujiandaa kushughulikia matukio haya kwa kuchunguza malalamiko haya haraka, vizuri na bila upendeleo.

Nafuu za kisheria zilizopo katika nchi husika zaweza kujumuisha mashitaka ya kisheria ama ya jinai au madai, usuluhishi, upatanishi, taratibu huru za malalamiko, uchunguzi maalum wa kitaifa, au Tume ya Haki za Binadamu. Majina na wajibu wa taasisi hizi zaweza kutofautiana baina ya nchi na nchi. Majukumu yao kwa kawaida hutamkwa katika sheria za nchi husika.

Ni jambo la muhimu kukumbuka kwamba makosa yanayohusiana na udhalilishaji wa kingono na kijinsia na unyanyasaji wa watoto, Jeshi la Polisi linao maafisa waliopata mafunzo maalum. Pamoja na kwamba ni vizuri kwa maafisa wa polisi kushughulikia haraka iwezekanavyo makosa yanapotokea lakini makosa yanapohusu udhalilishaji wa kingono na kijinsia au unyanyasaji wa watoto, kesi hizo zishughulikiwe na maafisa waliopata mafunzo maalum haraka iwezekanavyo katika Dawati la Jinsia na Watoto.

## 10.6. Ni nani anasimamia haki za binadamu?

Kuna makundi kadha wa kadha katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayoweza kutazama polisi wanavyofanya kazi. Utekelezaji wa haki za binadamu huangaliwa katika ngazi mbalimbali. Katika ngazi ya kitaifa, haki za binadamu zinasimamiwa na:

- Mawakala na taasisi za serikali, ikiwemo Jeshi la Polisi;
- Taasisi za kitaifa za haki za binadamu (kama vile, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora au Mchunguzi Maalum (Ombudsman);
- Mashirika ya haki za binadamu na Asasi zisizokuwa za Serikali (NGOs), yakijumuisha mashirika ya wanawake na yale ya Watu Wenye Ulemavu;

- ➢ Mahakama;
- ➢ Bunge;
- ➢ Vyombo vya habari;
- ➢ Vyama vya kitaalamu (kama vile vyama vya wanasheria, madaktari, n.k.);
- ➢ Vyama vya wafanyakazi;
- ➢ Taasisi za kidini; na
- ➢ Vitengo maalum katika vyuo vikuu.

Katika ngazi ya pili, taasisi za kikanda zimeanzisha mifumo ya kusimamia haki za binadamu katika nchi husika. Kuna mifumo mingi ya kikanda ikiwemo Inter-American Commission on Human Rights, Inter-American Court on Human Rights, European Court of Human Rights, Kamati ya mawaziri ya Baraza la Ulaya na kwa upande wa Afrika mfumo uliopo ni Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Afrika na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu iliyopo Arusha, Tanzania.

Katika ngazi ya kimataifa, haki za binadamu zinasimamiwa na taasisi mbalimbali zikiwemo asasi zisizokuwa za kiserikali za kimataifa kama vile Amnesty International na Human Rights Watch, na Umoja wa Mataifa.

Katika Umoja wa Mataifa, kuna aina nne za mifumo za kusimamia haki za binadamu:-
Mfumo wa kwanza ni kupitia kamati zilizoundwa chini ya mikataba ya kimataifa kama vile Kamati ya Kupambana na vitendo vya Utesaji, Kamati ya Haki za Binadamu, Kamati ya Haki za Mtoto, Kamati ya Kuondoa Ubaguzi dhidi ya Wanawake n.k

Mfumo wa pili ni mfumo unaoanzishwa chini ya Mkataba mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) ambapo kumeanzishwa vyombo kama vile, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa , Special Rapporteurs, Makundi Kazi (Working Groups) n.k.

Katika mfumo wa tatu haki za binadamu zinasimamiwa kupitia operesheni za kulinda amani chini ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Mfumo wa nne ni kupitia Kamishina Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa ambaye ana mamlaka ya kulinda na kukuza haki za binadamu ulimwenguni.

## 10.7. Viwango vya Umoja wa Mataifa na hatua zinazochukuliwa endapo polisi wanakiuka haki za binadamu

Taasisi za kusimamia sheria zina wajibu kupitia sheria za nchi na sheria za kimataifa kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu.

Afisa mmoja mmoja wa usimamizi wa sheria anapaswa kuwajibika kwa vitendo vyake. Kwa hiyo hii inahitaji usimamizi wa ndani na kwa kufuata taratibu zilizowekwa. Inapotokea ukiukwaji wa haki za binadamu hatua stahiki za kinidhamu na/au kisheria zinapaswa kuchukuliwa.

Umoja wa Mataifa umeweka taratibu na viwango ambavyo vinaweza kutumika kama mwongozo inapotokea polisi anakiuka haki za binadamu:

- ➢ Wasimamizi wa sheria wanawajibika kuheshimu na kulinda utu wa mtu na wanapaswa

kudumisha na kukuza haki za binadamu za watu wote.

- Taasisi za usimamizi wa sheria zitawajibika kwa jamii kwa ujumla.
- Maeneo ya matukio ya uhalifu yanapaswa kuangaliwa na kuchunguzwa vizuri.
- Maafisa wa ngazi za juu watawajibika kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwa walijua, au walipaswa kujua ukiukwaji huo na hawakuchukua hatua.
- Polisi atapata kinga ya kutoshitakiwa au ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukataa amri zisizo halali kutoka kwa maafisa wa juu.
- Utii wa maagizo kutoka kwa viongozi wa juu sio kinga endapo ukiukwaji wa haki za binadamu unafanywa na polisi.

## 10.8. Waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu

Ni muhimu kutambua kwamba waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu na hasa waaathirika kutokana na ukiukwaji uliofanywa na maafisa wa polisi ni waathirika pia kama walivyo waathirika wengine. Waathirika hawa wakati mwingine huwa katika wakati mgumu kuliko waathirika wengine kutokana na ukweli kwamba maafisa wa polisi ndiyo waliokiuka haki zao ambao walipaswa kuheshimu na kulinda haki za binadamu.

Waathirika wanapaswa kutendewa kwa huruma na heshima kutokana na utu wao. Wana haki ya kufikia mifumo ya utoaji haki na kupata nafuu ya kisheria haraka iwezekanavyo. Manusura (survivors) wa udhalilishaji wa kingono na kijinsia pamoja na unyanyasaji wa watoto wanahitaji matibabu na huduma za kisaikolojia. Pamoja na haya, kanuni na taratibu kuhusu ukusanyaji wa ushahidi unapaswa kuzingatiwa. Kesi zote zinazohusu udhalilishaji wa kingono na kijinsia pamoja na unyanyasaji wa watoto hazina budi kupelekwa haraka iwezekanavyo kwa maafisa wa polisi waliopata mafunzo maalum.

Umoja wa Mataifa umeandaa taratibu na viwango ambavyo vyaweza kutumika kama mwongozo katika kushughulikia waathirika:

- Mifumo thabiti inapaswa kuwekwa ili kuhakikisha nidhamu na usimamizi madhubuti kwa wasimamizi wa sheria ndani ya jeshi.
- Wasimamizi wa sheria ambao wana sababu za kuamini kwamba ukiukwaji umetokea, au unaelekea kutokea, wanapaswa kutoa taarifa.
- Utaratibu sharti uwekwe wa kupokea na kuchakata malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya wasimamizi wa sheria na taratibu hizo sharti zitangazwe au ziwekwe wazi ili zijulikane.
- Uchunguzi wa ukiukwaji sharti uwe wa haraka, kitaalamu, kina na usiopendelea upande wowote.
- Uchunguzi sharti uweze kubaini waathirika, upatikanaji wa ushahidi, upatikanaji wa mashahidi, kujua sababu, namna, mahali na muda wa ukiukaji ulivyotokea, na kubaini mhusika na kisha kumkamata.

## 10.9. Muhtsari

Serikali/nchi inawajibika kuheshimu, kulinda na kukuza haki za binadamu za kila mtu. Polisi ni wawakilishi wa serikali na sio chama cha siasa na kwa hiyo wanapaswa kuheshimu wajibu huo. Wajibu huo unajumuisha kutenda kwa usawa kwa watanzania wote na kushughuliki mahitaji ya waathirika wa uhalifu na utumiaji mbaya wa madaraka.

Waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na polisi nao ni waathirika kama walivyo waathirika wengine. Serikali inapaswa kuanzisha na kutekeleza mifumo na taratibu za kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Malalamiko yote ya ukiukwaji wa haki za binadamu lazima yachunguzwe kwa haraka, kitaalamu, kina na bila upendeleo.Wahusika wa ukiukwaji wa haki za binadamu wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria. Waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu wanatakiwa kutendewa kwa huruma na utu.

## 10.10. Maswali ya kujipima

- Nini maana ya ukiukwaji wa haki za binadamu?
- Ni nini wajibu na jukumu wa serikali/nchi katika kulinda haki za binadamu?
- Nafuu gani za kisheria zipo katika ngazi ya kitaifa pale panapokuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu?
- Ni nini wajibu na jukumu la Mchunguzi Maalum (Ombudsman)?
- Nini wajibu na jukumu la Tume ya Taifa ya haki za binadamu?
- Nini matokeo ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na wasimamizi wa sheria?
- Je, kuna wajibu wa kuchunguza ukiukwaji huo?
- Ni nani anawajibika kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na wasimamizi wa sheria?
- Nani anayesimamia haki za binadamu?
- Haki za waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu ni zipi?
- Jadili yanayoweza kutokea kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na maafisa wa polisi?
- Hatua gani zinapaswa kuchukuliwa na maafisa wa polisi inapotokea vitendo vya udhalilishaji wa kingono na kijinsia au unyanyasaji wa watoto?

# 11 SURA YA 11

## Taratibu za Usalama kwa ajili Vyombo vya Usalama Vinapofanya kazi na vyombo vya habari

### Mambo yaliyomo kwenye sura ya kumi na moja.


**11.1 Tafsiri pana ya wanahabari**

**11.2 Umuhimu wa usalama wa wanahabari**

**11.3 Wajibu na majukumu ya Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wa wanahabari**

**11.4 Jinsi gani Jeshi la Polisi linavyoweza kufanya kazi na vyombo vya habari katika operesheni**

**11.4.1 Mahusiano ya Jeshi la Polisi na vyombo vya habari wakati wa operesheni**

**11.4.2 Jinsi ya kuwaandaa askari**

**11.4.3 Jinsi ya kufanya kazi na wawakilishi wa vyombo vya habari mara wanapowasili**

**11.5 Jinsi ya kufanya kazi na vyombo vya habari wakati wa maandamano**

**11.5.1 Kabla ya maandamano**

**11.5.2 Wakati wa maandamano**

**11.5.2.1 Funzo**

**11.5.2.2 Mahali vyombo vya habari vinapaswa kukaa wakati wa maandamano**

**11.5.2.3 Umuhimu wa kuwa na eneo maaluum kwa vyombo vya habari**

**11.5.2.4 Jinsi ya kuweka eneo maalum kwa vyombo vya habari**

**11.5.2.5 Usimamizi wa wadau katika eneo maalum**

**11.5.3 Baada ya maandamano**

**11.6 Maswali ya kujipma**

## Malengo ya mafunzo katika Sura ya 11

Baada ya kumaliza sura hii washiriki wataweza:-

- Kutafsiri nani ni mwanahabari
- Kujadili umuhimu wa usalama wa wanahabari
- Kueleza kwa ufasaha wajibu na majukumu ya Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wa wanahabari
- Kufanya kazi na vyombo vya habari katika eneo la operesheni
- Kufanya kazi vizuri na vyombo vya habari kabla, wakati na baada ya maandamano
- Kutenga maeneo maalum ya vyombo vya habari wakati wa maandamano
- Kujibu maswali ya kujipima

# Utangulizi

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ushahidi wa kutosha kuhusu idadi ya mashambulizi dhidi ya usalama wa wanahabari na wafanyakazi wa vyombo vya habari na pia matukio yanayoathiri uwezo wao wa kutumia uhuru wao wa habari kutokana na vitisho vya kufunguliwa mashtaka, kutiwa mbaroni, kufungwa jela, kuzuiwa wasiweze kufanya kazi zao na kushindwa kabisa kuchunguza na kufungua mashtaka dhidi ya makosa ya jinai wanahabari waliyotendewa. Ushahidi huu umekuwa ukiwasilishwa mara kwa mara katika jumuiya za kimataifa na asasi za kiserikali za kimataifa, vyama vya wataalamu, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs) na wadau wengine.

Takwimu zilizokusanywa na UNESCO na pia mashirika mengine kama vile Kamati ya Kuwalinda Wanahabari (CPJ), Reporters Sans Frontières (RSF), International News Safety Institute (INSI), International Freedom of Expression Exchange (IFEX) na Inter American Press Association (IAPA) wote wanathibitisha kuhusu idadi kubwa ya wanahabari na wafanyakazi wa vyombo vya habari waliouawa wakiwa wanatekeleza wajibu wa kazi yao.

Zaidi ya hapo, kulingana na IFEX, katika kesi tisa kati ya kumi, watendaji wa makosa haya ya jinai dhidi ya wanahabari hawafunguliwi mashitaka. Kutoshitakiwa kwa wavunjaji wa haki za binadamu kunaongeza wigo wa mashambulizi dhidi ya wanahabari. Hali hii inahitaji ufumbuzi.

Usalama wa wanahabari na mapambano dhidi ya hali ya kutoshitakiwa kwa watu wanaosababisha vifo kwa wanahabari ni jambo muhimu ili kulinda haki za msingi za uhuru wa kujieleza, unaolindwa katika Ibara ya 19 ya Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Uhuru wa kujieleza ni haki ya mtu binafsi, kwa hiyo mtu hapaswi kuuawa, ila pia ni haki ya wananchi wote kwa ujumla, inayowapa uwezo wa kushiriki katika majadiliano yanayokuza demokrasia na hivyo kuwezesha upatikanaji wa maendeleo endelevu.

The 2015 World Press Freedom Index, inayotolewa na Wanahabari wasio na mipaka inaonesha kwamba Tanzania ilianguka kwa alama 6 (kutoka nafasi ya 69). Kwa sasa Tanzania ipo katika nafasi ya 75 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti mwaka 2014, ikiwa na alama 10.99 katika ukiukaji wa haki za wanahabari[10].

10 Kiwango cha mashambulizi na bughudha dhidi ya wanahabari na watoa huduma ya habari wengine katika kipindi cha mwaka 2014.

Bila uhuru wa kujieleza, na hasa uhuru wa vyombo vya habari, haiwezekani kuwa na wananchi walio na taarifa sahihi na wanoweza kushiriki vyema katika shughuli za kitaifa. Katika mazingira ambayo wanahabari wako salama, wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa urahisi na malengo mengi yanaweza kutimia, mfano: utawala bora na kupungua kwa umaskini; hifadhi ya mazingira, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, haki na utamaduni wa haki za binadamu, n.k[11]

## 11.1 Mwanahabari ni nani?

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mwaka 2010 ya Special Rapporteur wa haki ya uhuru wa kujieleza (ya tarehe 11 Agosti 2010, A/65/284), wanahabari ni watu wanaojitolea kwa ajili ya kufanya uchunguzi, uchambuzi na kusambaza taarifa kwa utaratibu unaokubalika, kupitia aina yoyote ile ya usambazaji habari kwa njia ya maandishi, urushaji wa habari kwa njia ya televisheni au radio au usambazaji wa habari kwa njia ya elektroniki.

The UNESCO Journalists Safety Indicators ya mwaka 2013 inatafsiri neno wanahabari kuwa ni wafanyakazi na mafundi wa kurekodi sauti au picha, wafasiri/wakalimani, watayarishaji na wafanyakazi wasaidizi, wahariri, mameneja na wamiliki, wakuu wa vyama vya wanahabari, mabaraza ya kitaaluma na mabaraza ya udhibiti wa habari, kutoka katika aina zote za vyombo vya habari, kama vile: kuchapisha, kurusha matangazo ya kawaida na matangazo ya mtandaoni; matangazo ya kibiashara na matangazo kuhusu umma na jamii.

Tafsiri hii pia inaweza kuwahusisha wafanyakazi wote wa habari ambao wanafanya uandishi wa habari wa jumla, wapiga picha, habari za uchunguzi, wanaotoa taarifa za uhalifu, maswala ya mazingira, n.k.

Kwa mujibu wa mikataba ya kazi, tafsiri hii inajumuisha wafanyakazi wote wa vyombo vya habari wenye mikataba ya kudumu; wale wasio na ajira rasmi (freelance); na wananchi wanaotoa taarifa (ambao wanafahamika kama waandishi wa mitandao ya kijamii wanaotoa habari nyingi zenye maslahi ya umma).

Kama unavyoona tafsiri hizo hapo juu, ugunduzi wa njia mbadala za mawasiliano umepanua wigo wa tafsiri ya uanahabari katika maeneo mapya, ikijumuisha uandishi katika mitandao ya kijamii.

## 11.2 Umuhimu wa usalama wa wanahabari

Uhuru wa habari ni haki ya msingi inayolindwa na Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa [Ibara ya 19], na kwamba haki hii huonekana kuwa msingi wa haki nyingine za kidemokrasia, mathalan uhuru wa kuunda vyama vya siasa, haki ya kubadilishana fikra za kisiasa, haki ya kuhoji vitendo vya watumishi wa umma, n.k. Kwa mantiki hii, haki hii ni muhimu kwa utawala bora na uwajibikaji katika jamii ya kidemokrasia.

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania inatamka kuwa:
kila mtu-
(a) Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza
fikra zake;
(b) Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;

11 UN Plan of Action on the Safety of Journalists and the Issue of Impunity, UNESCO, April 2012.

(c) Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na
(d) Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

*"Pale ambapo watumishi wa umma wanaposhiriki moja kwa moja katika vitendo vya mashambulizi dhidi ya wanahabari, serikali inawajibika moja kwa moja kutokana na vitendo vya watumishi wake" [Freedom of Expression and Public Order, Training Manual, UNESCO 2015]*

Kwa sababu hiyo, vyombo vya habari vinahitaji ulinzi maalumu ili kuviwezesha kutenda kazi zao kwa uhuru. Kwa hiyo wanahabari wanatakiwa kuwa huru na salama ili kutoa habari sahihi katika majukwaa ya vyombo vyao vya habari. Taarifa zinazotolewa na waandishi wa habari zinawakilisha haki ya watu wote ya kupata habari.

Katika ulimwengu wa teknolojia ya mawasiliano na habari ni muhimu kuelewa kwamba neno mwanahabari lina maana pana zaidi na kujumuisha siyo tu wafanyakazi wa vyombo vya habari ambao wanaratibiwa katika mfumo rasmi au kuajiriwa na shirika la utangazaji au uchapishaji habari bali inakwenda mbele zaidi kujumuisha waandishi katika mitandao ya kijamii.

Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanahabari wanaodhuriwa na kuuawa katika kazi zao, ulinzi wa waandishi wa habari dhidi ya vitendo hivi imekuwa ni jambo la muhimu kuangaliwa. Polisi na vyombo vingine vya usalama wanafanya kazi kwa niaba ya Serikali na wanawajibika kutenda kazi zao kulingana na wajibu wa Serikali wa kulinda usalama wa wanahabari.

*Haki ya faragha ya Polisi au haki ya kutopoteza sifa yake*
*Mipaka dhidi ya haki ya faragha ya polisi imeruhusiwa kuwekwa kwa ajili ya kuhakikisha usimamizi wa polisi na haki ya umma kujua jinsi polisi wanavyofanya kazi. Kwahiyo wakati wakitenda kazi zao Polisi hawana faragha. Hata hivyo, kuna wakati ambapo kutokana na sababu halali za kiusalama zinahitaji polisi kuchukua hatua za kuficha utambulisho wao. Sababu hizo zinapaswa kutofautishwa na sababu zinazohusu kulinda faragha, na kwa vyovyote vile tahadhari hii inapaswa kuchukuliwa pale tu ambapo kuna sababu za msingi na kwa kuwapa polisi vifaa vya kuficha sura au kutumia njia nyingine za kuficha utambulisho wao kuliko kuzuia haki ya wanahabari kuchukua taarifa kwa kurekodi.*

### 11.3 Wajibu wa polisi (kama watendaji wa dola) katika ulinzi na usalama wa wanahabari

The 2013 UNESCO Journalists Safety Indicators inaipa serikali jukumu la kwanza la kulinda wanahabari kama vile ilivyo kwa wananchi wengine. Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba sheria za nchi, taratibu za utumishi na mfumo wa mahakama zinalinda na kukuza haki ya habari na kulinda maisha na haki za kitaaluma za wanahabari. Imekubalika katika sheria za kimataifa kwamba serikali itawajibika dhidi ya vitendo vyote vya watumishi wake na vyombo vyake, hata kama vitakuwa vinafanya kazi nje ya utaratibu wa kisheria, na hata kama vyombo hivyo vinahitajika kuwa huru. Serikali pia inawajibika ikiwa watu binafsi wanavunja haki ya ulinzi wa wanahabari kutokana na maelekezo au usimamizi wa serikali, na

serikali itawajibika ikiwa itafanya uzembe katika kulinda haki za binadamu endapo haki hizo zinavunjwa na watu binafsi ambao ni wahalifu au magaidi.

Jukumu kubwa la serikali juu ya usalama wa wanahabari linatokana na wajibu mpana wa serikali wa kulinda haki za binadamu. Jambo la muhimu lililopo katika Journalists Safety Indicators ni kuwa serikali ina wajibu maalumu wa kuhakikisha kuwa waandishi wa habari wanofanya kazi katika maeneo yenye vita au migogoro wanachukuliwa kama raia na wanalindwa na sio kuchukuliwa kama wapiganaji. Ni muhimu pia kwa serikali kuchunguza vitisho na vitendo vya vurugu dhidi ya wanabahabari kikamilifu; kuhakikisha kwamba wanajeshi, mahakama na watekelezaji/wasimamizi wa sheria wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha kwamba inapambana na vitendo vya kutoheshimu sheria. Serikali inapaswa kutunga na kutekeleza sheria mahususi, kanuni na sera zinazowezesha waandishi wa habari kulindwa. Wale wote wanaoshika nafasi za kisiasa katika serikali au vyama vya siasa nao pia wanahusika katika jukumu hili.

## 11.4 Jinsi gani Jeshi la Polisi linavyoweza kufanya kazi na vyombo vya habari katika operesheni

Pindi afisa wa polisi anaposhambuliwa na kuuawa akiwa anatekeleza wajibu wake, hili linahesabika kuwa ni shambulio dhidi ya jamii kwa sababu Jeshi la Polisi linawakilisha jamii hiyo na afisa aliyeuawa alikuwa akitekeleza jukumu la kuilinda jamii. Hali kadhalika, pindi mwanahabari anaposhambuliwa na kuuawa akiwa kazini hili pia ni shambulio dhidi ya jamii, kwa kuwa alikuwa akitafuta habari ili kuihabarisha jamii hiyo. Kwahiyo, sio tu ni muhimu kutoa taarifa kwa wanahabari na kuwaongoza waandishi wa habari bali pia ni muhimu kuwalinda wakati wanapokuwa wanatekeleza wajibu wao.

Wanahabari na Jeshi la Polisi wote wana jukumu muhimu katika jamii kama walinzi wa demokrasia. Licha ya kuwa dhima na namna wanavyofanya kazi zao zinatofautiana, wote wanakutana katika maeneo wanapofanya kazi zao na wanatakiwa kushirikiana ili kufikia malengo yao husika.

Wanahabari ni daraja baina ya vyombo vya usalama na wananchi ambao husoma, kuangalia na kusikiliza vyombo vya habari. Kwa mtazamo huu basi, ni muhimu kwa vyombo vya usalama kuwa wazi, wakweli na wanaoaminika ili kukuza imani ya wananchi dhidi yao na uhalali wa uwepo wao.

Vyombo vya usalama vinatakiwa kuteua mapema wasemaji wao na kupanga ngazi ipi ya msemaji inaruhusika kutoa taarifa kuhusu jambo fulani, ili kuepuka mkanganyiko wowote na ili kuwa na uwezo wa kuwasiliana vizuri na umma au pia wakati wa kupanga maeneo maalum ya vyombo vya habari wakati wa operesheni.

> *Katika hali ya hatari na baada ya kujadiliana na vyombo vya habari:*
> *- Vyombo vya usalama vinaweza kutenga ukanda ambao wanahabari wanaruhusiwa kufika (Hii ni mipaka ambayo vyombo vya habari haviwezi kuvunja);*
> *- Kuteua msemaji katika eneo la tukio ili kutoa taarifa za wakati huo;*
> *- Zingatia kuruhusu 'kundi la wawakilishi wa wanahabari' (Mpiga picha wa video za Televisheni, mtangazaji wa Televisheni, mwandishi wa habari wa magazeti, Mpiga picha, mtangazaji wa radio), ambao wanaweza kuwapa taarifa wanahabari wenzao waliopo eneo lamembers of the press who are present..*

Kwa kuwa asilimia 80 ya mawasiliano na taarifa hayatumii njia ya mdomo, hii inamaanisha kuwa wana usalama kwa vitendo vyao na tabia zao wanaendelea kutoa taarifa bila hata kuongea na vyombo vya habari. Wana usalama wanapaswa kutambua pia kwamba wanayoyasema katika maisha yao binafsi kupitia mitandao ya kijamii yanaweza kuwa na athari katika taswira ya ufanyaji kazi wao.

### 11.4.1 Mahusiano ya jeshi la polisi na vyombo vya habari wakati wa operesheni

Vyombo vya usalama vinatakiwa kuweka sera kuhusu mahusiano na vyombo vya habari ili kutoa mwongozo kwa watumishi wao juu ya nini wakitarajie kutoka kwa waandishi wa habari na pia kwa upande wa wanahabari kuhusu jinsi wanavyoweza kupata habari.

Sera hiyo inapaswa kuenezwa ikiwa ni pamoja na kuwekwa katika za tovuti za vyombo hivyo. Sera iliyo bora inapaswa kuwa na baadhi ya mambo yafuatayo:

a) Jinsi gani vyombo vya habari vitapata taarifa? Kuna njia mbili: Aidha kwa njia ya ugatuzi ambapo wawakilishi wa vyombo vya habari wanafanya mawasiliano ya moja kwa moja na wakuu wa vitengo mbalimbali Au kwa njia ya kupitia ofisi moja kuu ambapo maombi yote ya taarifa hupitiwa na ofisi hiyo. Ni muhimu kuanzisha mfumo wa haraka na rahisi wa kutoa habari kwa vyombo vya habari, iwe kwa njia ya simu au kwa baruapepe.

b) Ngazi tofauti za wasemaji ikiwa ni pamoja na nani anapaswa kuzungumza na wakati gani.

c) Sehemu/mtu wa kuwasiliana naye endapo kunatokea ukamataji au tatizo lingine.

### 11.4.2 Jinsi ya Kuwaandaa Askari

Vyombo vya usalama vinapaswa kukuza uelewa wa watumishi wao kuhusiana na sera na mahusiano na vyombo vya habari kupitia taarifa rasmi na kwa kuingiza sera ya habari katika utendaji wa kazi wa ndani. Hii itasaidia kuwaandaa askari kufanya kazi na waandishi wa habari.

### 11.4.3 Jinsi ya kufanya kazi na wawakilishi wa vyombo vya Habari mara wanapowasili

Licha ya kuwa kuna viongozi na wasemaji, wana usalama wote wanapaswa kujiandaa kujibu namna ya kuwasiliana na wawakilishi wa vyombo vya habari wanapowasili katika eneo la operesheni. Ili kulinda na kuhakikisha usalama wa wanahabari na kuwasiliana nao vizuri, wana usalama wanapaswa:

a) Kufanya mkutano wa awali na wawakilishi wa vyombo vya habari;

b) Kuwataarifu wawakilishi wa vyombo vya habari kwamba wao siyo wasemaji, ila watawataarifu viongozi wao kwamba vyombo vya habari vimewasili;

c) Kuwataka vyombo vya habari kukaa katika eneo maalum la vyombo vya habari na kuwajulisha kuhusu kanuni za eneo hilo;

d) Kuepuka kutoa taarifa yoyote inayohusiana na operesheni, kwa kuwa jukumu hilo hufanywa na maafisa walioteuliwa; na

e) Kuwataarifu wana usalama/askari wengine kuhusu uwepo wa vyombo vya habari na eneo maalum ambalo waandishi wa habari wameruhusiwa kukaa ili kuepuka kutofautiana kuhusu jambo hili.

## 11.5 Jinsi ya kufanya kazi na vyombo vya habari wakati wa maandamano

Hili ni eneo muhimu kwa vyombo vya habari na polisi kwa kuwa maandamano yameonekana kuwa ni eneo ambalo vyombo vya habari vimekuwa vikilalamika kuhusu kubughudhiwa na polisi na vyombo vingine vya usalama hapa nchini Tanzania.

Maandamano ni njia inayotumika katika kuonesha maoni, mawazo na msimamo juu ya jambo fulani. Vyombo vya usalama vina wajibu wa kuhakikisha usalama wa kila mtu wakiwemo waandamanaji, askari na raia wengine. Maandamano yanaweza kuwa kikwazo kwa vyombo vya usalama lakini ni muhimu katika jamii iliyo huru. Vyombo vya usalama havipaswi kutoa maamuzi kuhusu kama maandamo hayo yana umuhimu au madhumuni yake yana tija. Hilo sio jukumu lao. Ili kuongeza ufanisi, vyombo vya usalama vinapaswa kuweka mipango ya awamu tatu: kabla, wakati na baada ya tukio/maandamano.

### 11.5.1 Kabla ya maandamano

Kutoa taarifa fupi kwa wanahabari ili:

a) Kufafanua jinsi gani vyombo vya usalama vitakavyo hakikisha udhibiti wa mkutano;

b) Kufafanua kile ambacho kitavumiliwa au hakitavumiliwa kwa waandamanaji;

c) Kufafanua kuhusu kanuni za kushirikiana na vyombo vya habari (Kwa mfano, nani ni wasemaji, ipi ni mipaka ya vyombo vya habari) na kuweka kanuni za operesheni kwa ajili ya jeshi la polisi na vyombo vya habari (kipi kitarajiwe kutoka pande zote mbili).

Wape taarifa fupi maafisa wote wa polisi kuhusu kazi ya wanahabari wakati wa maandamano na kanuni zilizowekwa za operesheni.

Kuweka kanuni za maadili kwa waandamanaji (kwa mfano, kitendo kipi kinaweza kuvumilika na kisichovumilika) na kusambaza kanuni hizi kupitia tovuti, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Toa tamko kupitia vyombo vya habari ukiwakumbusha waandamanaji kuhusu kanuni na kusisitiza kwamba jeshi la polisi litawapa fursa watu waweze kujieleza kwa njia ya maandamano ya amani bila vurugu wala kuvunja sheria za nchi.

### 11.5.2 Wakati wa maandamano

- Tenga eneo maalum ambapo wawakilishi wa vyombo vya habari watapewa taarifa na watakuwa na uwezo wa kuangalia tukio.
- Usitoe fursa ya kuhojiwa ukiwa katika eneo la maandamano ili kuepuka mgogoro na waandamanaji pia uwezekano wa kupigwa picha au kurekodiwa kwa picha ya video katika namna inayotoa taswira hasi, mathalani watu wanaokamatwa kwa nguvu, ishara au maneno yasiyofaa kutoka kwa waandamanaji.
- Sambaza habari kwa vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii ili washiriki wajue dhamira ya jeshi la polisi (kuwa nia yao sio kuingilia uhuru wa watu).
- Tenga eneo tulivu na lisiloonesha upendeleo wa upande wowote kwa ajili ya kushughulikia maombi ya wanahabari wakati wa tukio.

- Waruhusu wanahabari kufuatilia tukio, kama ambavyo wangeweza kufuatilia mechi ya mpira kutokea katika sehemu za pembeni na sio kati ya vyombo vya usalama na waandamanaji. Hali hii itawezesha vyombo vya habari kufuatilia matendo ya pande zote mbili.
- Wataarifu vyombo vya habari na wananchi kuhusu nia na hatua zitakazochukuliwa kupitia vyombo vya habari ili kuepuka mtu kukamatwa katika tukio (kwa mfano, pindi tukio linapokuwa limetangazwa kuwa sio halali na linapaswa kusitishwa, vyombo vya habari vinapaswa kutaarifiwa).
- Usizuie vyombo vya habari kupiga picha; vyombo vya usalama havina mamlaka wala uhalali wa kuweka vikwazo dhidi ya uhuru wa vyombo vya habari.
- Usinyang'anye vifaa; vyombo vya usalama havina mamlaka wala uhalali wa kuchukua hatua hiyo dhidi ya uhuru wa habari au uhuru wa kujieleza.

**11.5.2.1 Funzo**

- Kuwapa wanahabari kadi, kitambaa cha kufunga mkononi au utambulisho mwingine rasmi kunaweza kuhatarisha usalama wao dhidi ya waandamanaji ambao wanaweza kuwachukulia kuwa upande wa jeshi la polisi.
- Kadi za utambulisho za wanahabari zinapaswa kutumika tu kwa ajili ya kuwatambua, na siyo kutaka kuwabagua au kuwanyima fursa ya kuingia katika eneo maalum au chumba kilichotengwa kwa ajili ya vyombo vya habari.
- Wanahabari wana wajibu wa kusambaza habari kwa umma, na kuwaweka kando kunaweza kusababisha umma kupoteza imani na polisi. Kufanya kazi kwa uwazi ni kwa maslahi ya vyombo vyenyewe vya usalama. Ni vizuri kukumbuka kuwa wajibu wa wana habari ni kufikisha taarifa kwa umma.

**11.5.2.2 Mahali vyombo vya habari vinapaswa kukaa wakati wa maandamano**

Vyombo vya habari vinaweza kukaa katika maeneo matatu wakati wa maandamano:

a) **Ndani ya umati: (Wakati maandamano yanaendelea au yamesimama)**

Namna hii ina mahitaji madogo kwa upande wa maandalizi ya vyombo vya usalama kwa kuwa wanahabari wako ndani ya umati wa waandamanaji. Hata hivyo, usalama wa wanahabari hauwezi kuhakikishwa kwa kuwa wanahabari watatazama zaidi vyombo vya usalama kuliko waandamanaji (Hii husababisha, kwa mfano, waandishi wa habari kuchukua matukio yanayohusu vyombo vya usalama zaidi kuliko waandamanaji wanaopambana na vyombo hivyo ikiwa itatokea hivyo). Zaidi sana, wakati wa operesheni za kudhibiti waandamanaji, wanahabari wanaweza kujikuta katikati ya mapambano kati ya polisi na watuhumiwa.

b) **Kujichanganya (na vyombo vya usalama – wakati kunapokuwa na hatari kwa vyombo vya habari ili kuhakikisha usalama wao):**

Tofauti na pale wanahabari wanapokuwa ndani ya umati wa waandamanaji, katika utaratibu huu wanahabari wanakuwa katika nafasi ya kuangalia vitendo vya waandamanaji. Hata hivyo wanapokuwa katika nafasi hii vyombo vya usalama vina jukumu kubwa la kufanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha usalama wa wanahabari. Lakini pia katika utaratibu huu wanahabari wanaweza kuonekana kama ni sehemu ya propaganda ya jeshi la polisi.

.

c) **Katika eneo maalum la vyombo vya habari**

(Utaratibu huu ndio mzuri kwa maandamano yote kwakuwa huhakikisha wanahabari wanaweza kuripoti matukio pasipo kupendelea upande wowote). Nafasi hii inaviwezesha vyombo vya habari kuona pande zote mbili: Pindi eneo maalum linapokuwa limetengwa vizuri vyombo vya habari vinakuwa salama na pia vinakuwa katika nafasi ya kuangalia pande zote mbili. Eneo maalum linapaswa kuwa karibu vya kutosha ili kuwezesha wanahabari kuona vizuri na wakati huo huo kuhakikishiwa usalama wao.

Ili kuvihimiza vyombo vya habari kuingia katika eneo maalum, msemaji wa vyombo vya usalama anapaswa kuwa sehemu hiyo ili kutoa taarifa kwa vyombo vya habari.

**11.5.2.3 Umuhimu wa eneo maalum kwa vyombo vya habari**

- Eneo maalum linazuia wanahabari kufanya chochote wanachotaka kinachoweza kuhatarisha usalama wao kwa kutofuata maelekezo.
- Linatoa nafasi kwa vyombo vya habari kukaa eneo moja;
- Linapunguza wasiwasi wakati wa operesheni;
- Linatoa nafasi nzuri kwa wanahabari kufuatilia matukio;
- Linapunguza kazi kwa maafisa wasimamizi, kwa kuwa vyombo vya habari vimewekwa katika eneo maalum;
- Inatoa nafasi kwa maofisa wanaokuja kuzungumza na waandamanji au vikosi vya kuzuia maandamano kuingia katika eneo la tukio bila ya kuathiri utendaji wa kazi wa wanahabari;
- Linakuwa ni eneo maalum kwa ajili ya kutoa taarifa kwa vyombo vya habari; na
- Linakuwa eneo salama kwa vyombo vya habari.

**11.5.2.4 Jinsi ya kuweka eneo maalum kwa vyombo vya habari**

Kama inawezekana, au kama ikiwa eneo linafahamika mapema fanya ukaguzi wa eneo hilo;

- Chagua au tenga eneo salama
- Tumia riboni au kizuizi au alama yoyote ile kutenga eneo maalum kwa vyombo vya habari;
- Tenga njia ya kutokea au eneo la kutokea wakati wa dharura au matumizi ya mabomu ya machozi;
- Zuia watazamaji na watu wanaoweza kuleta usumbufu (Mfano, watu wanaoweza kuleta usumbufu kwa vyombo vya habari kwa kupiga kelele, kuwazuia n.k );
- Vipe nafasi vyombo vya habari kupata habari kupitia msemaji aliyeko katika eneo la tukio;
- Tenga mahali pazuri panapofaa (ambapo pana nafasi nzuri ya kufuatilia tukio kwa urahisi) panaporidhisha na kuwafanya wanahabari kubaki sehemu hiyo.

**1.1.1.5 Usimamizi wa wadau katika eneo maalum**

- Toa taarifa kwa taasisi zinazotoa huduma ya kwanza/huduma ya afya/idara ya zima moto;
- Usizungumze kwa niaba ya taasisi nyingine kama vile idara ya zima moto, watoa huduma ya kwanza, n.k;
- Usipingane na watu wanaoweza kuwa mashahidi;

- Tahadhari ya kutosha inapaswa kuchukuliwa kunapokuwa na hali tete au hali ya matumizi ya silaha. Wakati wote mawasiliano ni jambo la msingi kwa kuwa yanaweza kuleta upatanishi baina ya waandamanaji na jeshi la polisi. Kwa hiyo ni vizuri kuchunga kauli zinazotolewa.

**1.1.2 Baada ya maandamano**

- Waachie wanahabari walioshikiliwa wakati wa operesheni ya polisi mara tu wanapotambulika kuwa ni wanahabari.
- Tilia mkazo waandamanaji kuwa watulivu na epuka kuwachukulia waandamanaji wote kama wakosaji kwa kuangalia matukio yanayofanywa na watu wachache (kwa mfano, pale kundi ndogo la waandamaji wanaposababisha uharibifu wa mali).
- Pindi unapotoa taarifa au tamko (kwa vyombo vya habari), epuka kutoa maoni dhidi ya malengo ya waandamanaji; usipendelee upande wowote kwa kuwa siyo jukumu la vyombo vya usalama kutoa maoni yenye mwelekeo wa kisiasa.
- Toa taarifa kuhusu matokeo ya maandamano ndani ya vyombo vya usalama ili kuonyesha kwa vyombo hivyo kwamba maandamano yanaweza kufanyika na kusimamiwa kwa utulivu.
- Mwisho toa tathmini ya maandamano kwa vyombo vya habari.

## 11.6 Maswali ya kujipima

1. Je, unamtambua fundi mitambo kama mfanyakazi wa vyombo vya habari? Kwa nini?
2. Kwa nini usalama wa wanahabari ni muhimu?
3. Kitu gani kinaweza kusababisha kushuka kwa vigezo vya uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania kwa mwaka 2015?
4. Jinsi gani vyombo vya habari vinaweza kupata habari kutoka vyombo vya usalama?
5. Mambo gani vyombo vya usalama vinaweza kufanya kwa vyombo vya habari kabla ya maandamano?
6. Ni wakati gani vyombo vya habari vinaweza kujichanganya na vyombo vya usalama wakati wa maandamano?
7. Toa ufafanuzi mfupi kuhusu kile unachokielewa kuhusu eneo maalum kwa vyombo vya habari.
8. Mambo gani vyombo vya usalama vinaweza kufanya kwa vyombo vya habari baada ya maandamano?

## 11.7 Marejeo ya muhimu


➢ 2015 World Press Freedom Index : decline on all front, Reporters Without Borders

➢ Freedom of Expression and Public Order, Training Manual UNESCO, 2015

➢ Journalists as Human Rights Defenders are most at risk. http://www.thrd.or.tz/uploads/33.pdf

➢ Journalists' Safety Indicators: National Level, UNESCO, July 2013

➢ Resolution for the promotion and protection of human rights in the context of peaceful protests, 25th Session, Human Rights Council, March 2014 http://en.rsf.org/IMG/pdf/re_s_cdh_peaceful_protest_mars_2014_english.pdf

- Safety of Journalists Research Pack, Centre of Governance and Human Rights (CGHR), University of Cambridge, June 2012
- http://www.cghr.polis.cam.ac.uk/research-themes/right_to_life/safety-of-journalists-research-pack
- Towards an effective framework of protection for the work of journalists and an end to impunity , Seminar and Inter-regional Dialogue on the protection of journalists European Court of Human Rights, Strasbourg (PRESS ROOM), Sejal Parmar1 November 2014
- http://www.inter-justice.org/pdf/Sejal_Parmar_Protection_and_Safety_of_Journalists.pdf
- UN Plan of Action on the Safety of Journalists and the Issue of Impunity, UNESCO, April 2012.
- http://www.unesco.org/new/fileadmin/MULTIMEDIA/HQ/CI/CI/pdf/official_documents/Implementation_Strategy_2013-2014_01.pdf

United Nations
TANZANIA
Delivering as One

Mwongozo huu ulipitiwa upya na kuboreshwa kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia Mradi wa Kukuza Demokrasia (DEP)